KUTEMBEA
KATIKA
URITI WETU

Kitabu hiki kitachangamoto dhana yako na mawazo ya kanisa ni nini na sehemu yako ndani yake. Yesu alisema “nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu” Mariko 7:7

Soma kitabu hiki ufahamu:

- Kufanyika mwana
- Kuwa sehehu ya kikundi cha kitume
- Siri ya kanisa
- Kuhusiana na Yesu kama Mtume
- Kutembea katika urithi wetu
- Siku ya watakatifu;
- Kutawala na kutamalaki na Yesu Kristo

Na

Paul Galligan

DIBAJI

NINAKIPATIANA KITABU HIKI KWA BWANA YESU
NA WASHIRIKA WA MWILI WAKE

Kitabu hiki kimeandikwa katika kumtii
Bwana Yesu Kristo,
Kiongozi wa kanisa na mwokozi wa mwili.

Kimetolewa kwenu, watakatifu,
Kuwahimiza ninyi

"*Nakaza mwendo, niifikilie mende ye dhawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika kristo Yesu"*
Wafilipi 3:14

Sisi katika SHILOH tunakuombea wewe

"Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo,

Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ufunuo katika kumjua yeye;

macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo;

na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo;

na ubora wa ukuu wake ndani yetu tuaminio"

Waefeso 1:17-19a

YALIYOMO

Dibaji ya maneno

Utangulizi – kufikia kujua siri ya ufunuo …….. 7
- Ujuzi wa kubadilishwa
- Mungu anaandaa mioyo ya kuwapokea mitume
- Nyakati za urejesho

Sura ya 1 kufanyika wana wa Mungu ……. 9
Safari ya ukomavu
Akina baba wa kiroho
Ujuzi wa tatu
Roho ya kufanyika wana
Mtoto alizaliwa: Mwana alipatianwa
Wana wa Mungu ni nani
Roho na nguvu za Eliya

Sura ya 2 kuitwa kuwa kikundi cha kitume …… 18
Kikundi cha kwanza cha kitume
Kuitwa kuwa mtu wa kitume
Kuitwa kuwa kanisa la kitume
Kufikia mataifa kupitia neema na utume
Mabadiliko ya kitume ya kanisa
Kuundwa kwa vikundi vya kitume
Mfano wa Agano la Kale wa kikundi cha kitume
Vikundi vya kitume vya Agano Jipya
Mpango wa Mungu ukifanya kazi siku za mwisho

Sura ya 3a Siri ya kanisa – sehemu ya kwanza …… 27
Kanisa katika Yerusalemu
Kanisa katika Antiokia
Kanisa katika Efeso
Kubarikiwa na kila aina ya baraka
Mahali Kristo na kanisa lake wamewekwa
Nitalijenga kanisa langu
Ufunuo wa siri
Kuna MOJA
Siri ya kipawa cha huduma tano

Sura ya 3b Siri ya Kanisa – sehemu ya pili …… 35
Neema ya kukua hadi ukomavu
Kusudi la Mungu la milele
Huduma tano zinaleta kanisa katika ukomavu
Kusudi tatu za huduma tano
Ishara ya ukomavu

Sisi ni nyumba ya Mungu
Siri ya Kristo na kanisa lake
Kanisa linafunuliwa

Sura ya 4 Yesu mtume wetu …… 42
Kuhani mkuu
Yesu mtume wetu
Mahali pa Mungu pa kukaa duniani
Yesu anajenga aje nyumba ya Mungu leo
Tunampokea aje Yesu kama Mtume leo
Ni nini kinakosekana kanisani leo
Yesu kama Baba Yetu
Ni wakati wa kumpokea Yesu Mtume wetu

Sura ya 5 kutembea katika Urithi wetu …….. 51
Urithi ni hapa duniani
Yesu aliahidiwa urithi
Yesu alipokea urithi
Urithi wetu
Mwana fulani anapokea urithi wake
Mtumwa anafanyika kuwa mwana

Sura ya 6 Siku ya Watakatifu …… 61
Ufalme wa Mungu unatawala watu wote duniani
Kuufahamu wito wa Mungu
Watu wa kitume katika kitabu cha matendo
Kiriba kipywa
Kuitwa kumfuata Yesu

Sura ya 7 Kutawala na kumiliki na Kristo …… 70
Mfano wa magugu
Ufalme Wako uje
Kuja kwa Mfalme
Ni wakati wa kumfanya Yesu Mfalme
Yesu ametufanya kuwa wafalme na makuhani
Tabia za watakatifu wa siku za mwisho
Yesu yuaja kama Mfalme

Kutamatisha …….. 83

Ombi la kuingia kwa uwana ……. 85

Dibaji ya maneno

Mutume: Yesu aliinua huduma ya mtume. Huduma hii haikujulikana sana katika Agano la kale. Mtume ni mjumbe wa Kristo, aliyeamuliwa na kutumwa na yeye kumwakilisha yeye. Mtume ni 'yule aliyetumwa' kwa niamba ya mwingine akiwa na mamlaka ya aliyemtuma, na kumwakilisha kikamilifu na kufanya ajulikane aliyemtuma.

Utume: inazungumzia kanisa na kila kitu cha mkristo ambayo yanaonekana na kufanywa kupitia Agano Jipya, kulingana na neno la Mungu na sio tamaduni za watu.

Ukristo wa kitume: Ukristo wa Agano jipya, kuwa watiifu kwa neno la Mungu na kujenga kulingana na muundo uliowekwa katika neno, sio kidini.

Kikundi cha kitume: kikundi cha wanafunzi ambacho kimejipatiana na kinahudumu chini ya uongozi wa mitume/mtume ambao wana nia moja na moyo kulitumikia kusudi la Mungu.

Kanisa: mwili wa Yesu ulioundwa na waumini waliozaliwa mara ya pili ambao wametengwa kwa ajili ya Yesu Kristo, ambao wameitwa kutoka kwa dunia na mahusiano yote ya dunia, ambayo yanahusisha idara za wanadamu, na taasisi ambazo zinaonekana kama kanisa wakati huu.

Akina baba: Kwanza, mitume ambao Kristo amepatiana kuwa akina baba kanisani; pili wahuduma waliokomaa na watakatifu ambao wamefikisha kiwango cha na wamefanyika akina baba kwa walio wachanga katika Kristo.

Huduma tano: Inaongea kuhusu karama tano za huduma ambazo Kristo alilipa kanisa lake alipopaa mbinguni; "***naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu"*** **Waefeso 4:11.** Pia zinatambulika kama karama za upao.

Neema: Kibali kisichostahili, kilichotolewa bure, nguvu za kuwezesha za Mungu ambazo zinamtayarisha mtakatifu kutembea katika njia za Mungu; neema hupokelewa kwa imani.

Utoaji/kuachilia: Ni ujuzi maalumu wa kupokea upako zaidi na maisha ya Roho ambayo mara kwa mara ndio njia ambayo Mungu huachilia neema zaidi katika maisha Yetu.

Urithi: Ambacho ni chetu tunachostahili kupokea tukiwa hapa ulimwenguni wakati tunafikia kiwango cha ukomavu katika Kristo; Mungu amefanya hii ipatikane na imehifadhiwa mpaka wakati tuko tayari kupokea. Urithi unahusisha neema, nguvu, hekima, ufunuo, ushindi juu ya shetani, baraka na utukufu, na ahadi halisi ya kuja Kwake.

Ukomavu: kufikia nyakati katika Kristo; tayari kupokea urithi. Lazima mtu akomae ili aanze kutembea katika ukamilifu. Hatustahili kukaa tukiwa watoto wachanga katika Kristo.
Siri: Hekima iliyofichwa ambayo Mungu aliiazimu tangu mwanzo kwa utukufu wetu

(1 Wakorintho 2:7); kitu katika siri ambacho chastahili kutafutwa na kuelewa. Agano Jipya yasungumza kuhusu ‘siri nyingi’.

Urejesho: Mungu ameahidi kurejesha vitu vyote ambavyo vimenenwa katika neno lake. Urejesho wa mitume ni jambo la muhimu sana katika urejesho wa kanisa.

Ufunuo: Biblia ni ufunuo wa Mungu kwa mtu; tunapomtafuta kwa bidii kupitia neno Lake, Anatujulisha mapenzi Yake kwa kutupa ufahamu na kuelewa neno Lake.

Watakatifu. Wale watakatifu, wale ambao wameitwa na ni waaminifu katika kumfuata Yesu na kuwa na utiifu kwake katika ushirika wa mwili wake.

Uwana: kufikia hali ya ukomavu kupokea urithi, kutembea na Mungu kwa uhakika wa ubaba wake; Uwana huanza katika ujuzi wa mabadiliko

Ujuzi wa mabadiliko: Ujuzi mkuu wa mabadiliko ya maisha katika kutembea kwa mkristo, mabadiliko ya kwanza ni kuzaliwa mara ya pili, mabadiliko ya pili ni kujazwa na kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu; mabadiliko ya tatu ni kuwa na ujuzi wa kujua uhakika wa uwana, roho wa kufanyika mwana.

UTANGULIZI

Ufunuo wa siri

Waefeso 3:4, 6 "*Ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo…*
"*Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine;*
kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho".

Ushirika wa ndani

1Yohana 1:1, 3 "*lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia,*
tuliloliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa,
kwa habari ya Neno la uzima; …twawahubiria na ninyi;
ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi"

Nyakati za kuburudishwa

Mdo 3:21 "*zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na*
Mungu kupitia kwa kinywa cha manabii wake watakatifu"

Tunaamini tumeingia wakati muhimu katika kusudi la Mungu kimataifa.
Mungu anainua mitume katika kila taifa. Ufunuo wa kitume ni wa kanisa lote.
Ni wakati wa ukomavu – kwa watakatifu kukua na kupokea neema ya kufanyika wana.
Huu ni ujuzi wa kuyajua mabadiliko ambao Mungu anaachilia kwa kanisa lake
katika kujiadaa kwa kuja kwa Bwana "kwa kanisa tukufu".

Kuja kujua ufunuo wa siri

Katika safari ya umishonari marchi/Aprili 2004 kule Mauritius na mataifa manne ya Africa [Kenya, Uganda, Rwanda na Demokrasia ya jumuia ya ya Congo], tulipokea ufunuo wa ziada katika ufahamu wa ufunuo wa Kitume.

Nuru tunayoangaza ilipatianwa '*tulipojipatiana kwa kazi ya huduma'.* Yaliyojili katika safari hii ya umishonari ilikuwa ni makongamano ya wachungaji na viongozi. Mungu alikuwa ametutangulia, akiandaa mioyo na kulikuwa na mapokezi yaliyo wazi kwa mafundisho ya kitume na kupokea ufunuo wa siri kama ilivyoonyeshwa katika **Waefeso 3:3,5 *"ya kwamba kwa kufunuliwa nilijulishwa siri hiyo…siri hiyo hawakujulishwa vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii."***

Katika siku zetu, Mungu anajulisha tena ufunuo huu kwa Roho. Paulo anasema kwa kusoma yaliyoandikwa tutaelewa ufahamu wake wa siri; unaposomo ufunuo ambao Mungu anakupa leo, atakupa ufahamu wa kweli wa maandiko, akileta ufunuo wa siri.

Ujuzi wa mabadiliko

Tuliona Mungu akifanya kazi ya kushangaza Africa na Mauritius wakati maaskofu wengi, wachungaji na viongozi walipokea neema ya ufunuo na ufahamu; wengi wakipata ujuzi wa mabadiliko katika maisha yao, **kama kuzaliwa mara ya pili kali, ama kupokea Roho**

Mtakatifu.

Kila mahali ambapo tulienda, katika mataifa hayo matano, viongozi walitupokea, walipokea mafundisho na kumpokea Bwana alipokuja na ushawishi, akiachilia utoaji wa neema na kweli na akithibitisha ishara na maajabu. Katika kongamano moja magharibi mwa Kenya, Askofu mpendwa wa miaka therathini mwenye ujuzi wa huduma na akiyaangalia makanisa kadhaa alishuhudia kwamba hajawahi kukutana na ujuzi wa Nguvu za Roho Mtakatifu katika maisha yake mpaka tulipomuombea. Alisema, *'kwa mara ya kwanza katika maisha yangu, wakati kikundi kiliniwekea mikono,* nguvu *za Roho Mtakatifu ziliingia ndani ya mwili wangu,'* alizidiwa na nguvu za Roho Mtakatifu, kama ilivyokuwa kwa kila mtu katika kongamano – kila mtu alisongea kwa maombi.

Mungu anaandaa mioyo kwa Ufunuo wa Utume

Kama vile Yohana aliandika katika waraka wake wa kwanza, ***"lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tulilioliona kwa macho yetu, tulilolitazama, hilo tulioliona na kulisikia …twawahubiri na ninyi pia, mpate kushirikiana nasi* 1 Yohana 1:1,3".** Kuna ufunuo wa ndani unaojulikana kwa wale wanaopokea ufunuo wa kitume ambao Mungu ameachilia kwa upako wake kwa kanisa. Kote kote duniani Mungu anaandaa mioyo.

Kuna kutotoshereka kutakatifu katika mioyo ya watakatifu wengi na wahuduma. ***"Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa"* (Waefeso 5:27),** ambalo Kristo atajiletea atakapokuja, hatakuwa tayari kujiletea mivumo ambayo iko katika hali ya makanisa mengi.

Nyakati za urejesho

Tumebarikiwa kuwa tunaishi katika ***"zamani za kufanywa upya vitu yote, zilizo nenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu"* Mdo 3:21.** Maandiko yasema, "***atapokelewa mbinguni Yesu Kristo mpaka"*** wakati huo. Yesu haji mpaka vitu vyote vinavyosomwa katika maandiko ambavyo vinahusu kanisa la Agano Jipya virejeshwe.

Kanisa litarejeshwa Katika kujiandaa kwa Kuja kwa Bwana.
Anakuja kwa kanisa tukufu, kwa mwili uliokomaa wa watakatifu,
Au wana walio tayari kupokelewa kikamilifu katika utukufu,
na kutawala na kumiliki duniani na Kristo Ajapo.

Sura ya kwanza

KUFANYIKA WANA WA MUNGU

Ili kufanyika wana wa Mungu *"Bali wale wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waaminio jina lake"* **Yohana 1:12**.

Watoto wadogo, vijana, akina baba
"Nawaandikia ninyi, watoto wadogo, kwa sababu mmesamehewa dhambi zenu, kwa ajili ya jina lake.
Nawaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mmemjua yeye aliye tangu mwanzo.
Nawaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mmemshinda yule mwovu. Nimewaandikia ninyi, watoto, kwa sababu mmemjua Baba. Nimewaandikia ninyi, akina baba, kwa maana mmemjua yeye aliye tangu mwanzo.
Nimewaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mna nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule mwovu" **1 Yohana 2:12-14.**

Kuongozwa na Roho "*kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu"* **Warumi 8:14.**

Roho wa kufanyika wana "*kwa kuwa hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia Aba, yaani, Baba"* **Warumi 8:15**

Kufunuliwa kwa wana wa Mungu *"kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu"* **Warumi 8:19**

Safari ya ukomavu

Wakati tumezaliwa mara ya pili, hivyo ni wakati tunazaliwa na Mungu ***"anatupa uweza {mamlaka, haki} wa kufanyika watoto wa Mungu"*** **(Yohana 1:12-13).** Huu ndio mwanzo wa maisha yetu katika Kristo.

Kuma ujuzi aina tatu za mabadiliko:

i. Kuzaliwa mara ya pili - kufanyika mtoto wa Mungu;
ii. Kupokea nguvu za Roho Mtakatifu - kupata ujuzi wa maisha yaliyojaa Roho;
iii. Kufanyika mwana – Kuingia katika kutembea kulikokomaa na Mungu; kuna ujuzi wa tatu kwa muumini.

Kila ujuzi huu katika Kristo inatuingiza katika nafasi ya kutembea kwa undani kutoka kuwa watoto hata kufikia wana waliokomaa

Mtoto katika Kristo

Wakati tunaokolewa kwanza, tunafanyika watoto katika Kristo na maandiko yasema yakuwa lazima ***"tuyatamani maziwa ya akili yasiyoghoshiwa"*** **1Petro 2:2**. Wakati tunapokea msingi wa malezi katika Kristo tunatembea kama watoto. Yohana anasema katika **1 Yohana 2:12-14** ya kwamba watoto wadogo ***"wanajua dhambi zao zimesamehewa"*** na ***"wamemjua Baba".***

Mambo mawili ya dhamani ambayo wakristo wapya wanajua ni: ya kwamba Yesu ametusamehea dhambi zetu zote na hivyo sasa sisi ni wa jamii ya milele ya Mungu. Wengi wetu wanaweza kumbuka habari njema ya ajabu iliyotufikia wakati tulizaliwa mara ya pili.

Fanya wanafunzi

Kutembea kwetu kama watoto ni kutembea kwa uwanafunzi. Mwanafunzi ni yule amekwisha fundishwa na, katika mazingira ya Kristo, akifundishwa neno la Mungu. Yesu aliwaagiza wanafunzi wake, haswa mitume, ***"kufanya mataifa yote kuwa wanafunzi…..na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi"*** **Mathayo 28:19-20.**

Wanafunzi wanahitaji mwalimu na ni katika kipindi hiki cha 'utoto' ambapo tunahitaji kuendelea katika uwanafunzi – tukifundishwa neno la Mungu. Hivyo, huduma kuu ya mwalimu ni kufanya wanafunzi [hii ni karama ya huduma tano ya **Waefeso 4: 11].** Katika asiri tunawatuma watoto wetu shule kwa kipindi cha miaka kumi na miwili "ili wafundishwe" katika elimu ya dunia hii. Zaidi namna gani twapaswa kuwa tukifanya wakristo wanafunzi, ikihusisha watoto wa wakristo, katika maarifa ya neno la Mungu?

Wanafunzi wanatakiwa kuwa waalimu

Watoto wanahitaji mkate kila siku wa neno la Mungu. Mwanafunzi anatakiwa kufundishwa neno la Mungu hadi mwanafunzi aweze kulifundisha neno la Mungu.

Mtume akiandikia Waebrania **(5:12)** anawaonya waumini akisema ***"kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu''.*** Kutoka kifungo hiki cha maandiko katika ***Waebrania*** **5** na **6**, tunaelewa kwamba mafundisho ya msingi ambayo kila mwanafunzi anahitaji kuwekwa msingi ndani yake ndizo kanuni za kwanza za Kristo kama ilivyoorodheshwa katika **waebrania 6:1-2**. Kumekuwa na upungufu katika makanisa mengi katika eneo hili la msingi la uwanafunzi. Kama matokeo waumini wengi hawajawekwa msingi katika kanuni za kwanza za kristo na wamebaki bila kukomaa.

Tunatakiwa kukua kutoka watoto kuwa vijana,
na kisha kukua mpaka ukomavu,
utimilifu ukiwa ndilo lengo.

Lengo ni ukomavu

Lengo la Mungu ni kila muumini akue kutoka mtoto kuwa mtu mzima. Hatua tatu za ukomavu:

- Watoto wadogo – wanafunzi ambao watakiwa kufundishwa,
- Vijana – tayari kuandaliwa katika huduma,
- Akina baba – waliokomaa, wakiwa tayari kuwa na wana wa kiroho.

Katika **Waefeso 4:11-16** mtume anatufundisha kwamba karama ya huduma tano iliyopeanwa na Kristo ni ya kufanya kazi mpaka kanisa lifikie ukomavu kamili: **"*ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu"* Aya 14**. Waumini waliokomaa hawatandanganywa wala kupotoshwa na waalimu wa uongo kwa kuwa wamefundishwa vyema, hivyo ni kufundishwa neno la Mungu.

***"ufunge huo ushuhuda, ukaitie muhuri sheria kati ya wanafunzi wangu. Ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi"* (Isaiah 8:16** na **20)**

Kutoka kwa watoto hata kwa vijana

Tunaanza safari yetu ya ukristo kama watoto ambao wamelelewa na maziwa ya neno, na kisha kama watoto tunakua tunapopokea mkate wa kila siku.

Hatua ya pili ya maisha yetu ya ukristo ni kufanya kazi na kutumika kama *'vijana'* ambao ***"wana nguvu na wamemshinda yule mwovu kwa sababu neno la Mungu linakaa ndani yao"* 1Yohana 2:13-14**. Chanzo cha nguvu ya vijana ni neno la Mungu linalodumu ndani. Yesu alisema ***"ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli. Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru"* Yohana 8:31-32**. Kama matokeo ya neno la Mungu likikaa ndani yao, 'vijana' wanajua ushindi dhidi ya yule muovu – wao ni washindi na hivyo wanaweza kuhudumia wengine.

Kukamilisha na kujenga wahuduma

Hawa wako tayari kwa kukamilishwa kwa awamu kama Timotheo – kujiunga na mtume, ama kikundi cha kitume, na kufundishwa kwa huduma ya uongozi. Katika asiri, wakati watoto wamemaliza masomo ya msingi na ya upili, kisha huenda katika chuo kikuu, wanajifundisha ama wanaenda moja kwa moja katika eneo la kazi. Wamekuwa vijana wa kike na wa kiume, tayari kwa kukamilishwa, tayari kwa huduma, tayari kwa kazi. Kwa hivyo katika kiroho ni vile vile.

Mara tu mwanafunzi ameandaliwa kiwango ya kwamba
sasa anaweza kufundisha neno, wamefikia kiwango cha 'vijana';
na kama vijana katika Kristo wameandalika kwa
kukamilishwa na kujengwa kwa huduma.

Kutoka kwa mwanafunzi hadi kwa muhuduma – katika maandalizi

Timotheo alikuwa mwanafunzi Listra. ***"Mtu huyo alishuhudiwa vema na ndugu waliokaa Listra na Ikonio"* Mdo 16:1-2**. Paulo alimchukuwa katika safari yake wakaadamana, lakini haikuwa mpaka wakati alimtahiri – gharama ya kiwango cha juu kwa mwanafunzi huyu! Timotheo alikuwa amefanyika 'kijana' katika Kristo. Wazee wa mahali pamoja katika Listra na Ikonio walikuwa wamefaulu katika kufanya wanafunzi wa Timotheo.

Kusudi la uwanafunzi ni uwajibikaji wa wazee, hivyo ni, wachungaji na waalimu ambao wamewekwa wakfu katika kanisa la mahali pamoja ***"lichungeni kudi la Mungu"* (1Petro 5:2** na **Mdo 20:28)**

Wakati muumini amemefanya mwanafunzi vyema muumini ako tayari sasa kwa mafunzo na kuandaliwa kwa huduma, na huo ndio wajibu wa mitume na manabii.

Timotheo aliingia katika wakati wa mafunzo kwa kuenenda na kikundi na Paulo na alikuwa mmoja wa *'shule ya Tirano*" ya Paulo **(Mdo 19:9-10**) katika Efeso. Baadaye Paulo anarejelea kwa wakati huu wa mafundisho katika **2 Timotheo 2:2** wakati anasema, **"*na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu,***

watakaofaa kuwafundisha na wengine". Kwa wakati huo Timotheo alikuwa ni mhuduma aliye kazini kikamilifu kama mtume na alikuwa ameagizwa na Paulo kuachilia mafundisho kwa wale anawafundisha kwa huduma. Wale ambao wameandaliwa wana uwezo wa kuachilia mafundisho ya kitume kwa wengine.

Akina Baba wa kiroho

Uhakika wa kuwa na baba wa kiroho

Uhakika huu ni kama siri kwa kanisa la wakati huu kwa sababu uhakika wa kuwa na akina baba wa kiroho umekuwa umekosa. Hata hivyo, wahuduma na watakatifu kila mahali wanakumbatia mahusiano kama hayo na kufurahia kuwa na baba wa kiroho na akina mama. Tunashuhudia kwamba huu umekuwa ujuzi kwetu kwa miaka ya hivi karibuni na mahusiano haya yamekuwa yakileta ujuzi wa mabadiliko na kutembea katika neema ambayo hatukujua kuwa iko.

Akina baba wanarejeshwa kulingana na neno la kiunabii: **"*Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na kuogofya. Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana".*** Watoto (wana) wanarejeshwa*: "Naye atageuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao".* Hili ni jambo ambalo Mungu analifanya **(Malaki 4:5-6).**

Uhusiano na baba wa kiroho

Ujuzi huu wa uwana unaachiliwa wakati mtu anakuwa na uhusiano na baba wa kitume, ama anahudumiwa na baba wa kitume. Kwa bahati baya, viongozi wengi wa huduma katika kanisa sio akina baba. Ni viongozi ambao hawana moyo wa baba, makini kufundisha, kuhubiri na kuhudumu na kutumika na kulinda huduma zao, mwito wao, kipato chao cha fungu la kumi vitu vyao…vyovyote. Haya ni matokeo kwa upana ya kutokuwa na akina baba kwa wahuduma wakati walipokuwa wakikua.

Urejesho wa akina baba wa kitume

Kumekuwa na njaa ya viongozi wa kitume katika kanisa. Paulo anasema **"*kwa kuwa ijapokuwa mna waalimu kumi elfu katika Kristo, walakini hamna baba wengi"* 1Wakorintho 4:15.** Kwa bahati baya wengi wetu wamekuwa chini ya viongozi ambao hawakuwa akina baba kwa hivyo kukua kwetu na kuandaliwa kumeharibiwa, kukagandamizwa, ukosefu wa vyakula na uyatima.

Mungu asifiwe! Leo anarejesha akina baba wa kiroho na huduma ya mitume kwa kanisa. Wahuduma wa miaka mingi ya kuhudumu ambao wamekuza makanisa mengi na wengine katika huduma sasa wanapata baba wa kiroho, sasa wanapokea neema ya kufanyika wana na kuingia katika mahali pa usalama kama wana. Kiongozi mmoja mkuu alishiriki nasi kwamba alikuwa amewainua wana wengi katika huduma lakini wote walikuwa wamemuacha. Wakati alisikia ujumbe wa uwana akatambua kwamba ni kwa sababu yeye hakuwa na baba.

Kiwango cha tatu cha kukua kiroho ni kuingia katika uwana,
kupokea neema ya kutembea katika ukomavu; kama mwana aliyekomaa,
sasa tayari kuleta mazao, hivyo ni kupata wana wa kiroho, kufanyika baba.

Mwanafunzi, mtumishi, mwana

Mwanafunzi anajifundisha kutoka kwa mwalimu, anatumikia bwana, akifanyika mwana kwa baba. Kuingia kwa uwana haifanyiki kwa urahisi. Elisha, 'mwana' maarufu katika

maandiko, alikuwa mwanafunzi na kisha mtumishi kwa miaka kadhaa. ***"Aliyekuwa akimimina maji juu ya mikono yake Eliya''*** **2 wafalme 3:11**. Eliya alikuwa bwana wake mpaka wakati alipochukuliwa juu; manabii wa betheli na kule Yeriko wote walitambua ya kwamba Eliya alikuwa bwana 'juu' ya Elisha **(2 wafalme 2:3,5).** Hata hivyo siku hiyo Elisha *'aliona'* na akalia, ***"baba yangu, baba yangu"*** **2 wafalme 2:12**). Aliingia katika uwana, akipokea urithi wake kama mzaliwa wa kwanza ambayo ilikuwa ni sehemu mara dufu ya kile chote ambacho baba yake alikuwa nacho.

Mwanafunzi anafanyika mwana

Baadaye katika maandiko Paulo anamtuma Timotheo katika Korintho akisema ***"kwa sababu hii nimemtuma Timotheo kwenu aliye mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana, atakaye wakumbusha njia zangu zilizo katika Kristo, kama vile nifundishavyo kila mahali katika kila kanisa''*** **1 Wakorintho 4:17**. Timotheo alikuwa mwanafunzi wa kanisa la mahali pamoja katika Listra na Ikonio na akachukuliwa na paulo kwa mafundisho katika huduma. Katika aya iliyo juu, Timotheo kwa wakati huu alikuwa amefanyika mwana katika imani na ako tayari kutumwa na baba yake wa kiroho kumwakilisha mtume katika huduma ya neno.

Kwa wakati unaofaa mwanafunzi anahitimu kwa kuandaliwa na mwanafunzi anakuwa kwa ukomavu, akifanyika mwana. Kuingia katika uwana inafanyika tu wakati muumini amefika kiwango cha ukomavu cha kiroho. Yohana anarejelea kwa hawa kama akina *'baba'*. Akina baba katika maelezo wako na watoto na bila shaka tunazungumza habari ya watoto wa kiroho. Kiwango hiki cha ukomavu sio kitu ambacho tunaweza kufikia lakini inaamuriwa na baba, **"*lakini nasema ya kuwa mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote; bali yu chini ya mawakili na watunzaji, hata wakati uliokwisha kuamuriwa na baba"*** **Wagalatia 4:1-2**. Na sasa ni wakati ambapo Mungu Baba anaiita kanisa lake katika ukomavu.

Ujuzi wa mabadiliko

Kuzaliwa mara ya pili ni utenda kazi wa siri ya neema ya Mungu iliyopokelewa kwa imani. Kupokea Roho Mtakatifu kwa nguvu, hivyo ni, kubatizwa na Roho Mtakatifu **(Mathayo 3:11),** ni siri ya neema ya Mungu ikipokelewa kwa imani. Hata hivyo kupokea neema ya uwana, kuwa na ujuzi wa mabadiliko, ni utenda kazi wa siri ya neema ya Mungu ikipokelewa kwa imani. Matokeo ni kutembea na Bwana kulikogeuzwa, ambayo inafanyiwa kazi katika uhusiano wa ndani ikiachilia ujasiri, usalama, nidhamu ya kiungu, kitambulisho na ufanisi.

Utoaji wa nguvu za roho

Ni vigumu kueleza lakini kuna kuachiliwa kwa upendo wa Mungu ambao ni upendo wa Baba. Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu kwa kuachiliwa ambayo inatuwacha bila shaka ya kwamba sisi ni wana wa Mungu; na tuna baba wa kiroho katika hiyo, ambaye Mungu alimtuma kwetu, kuachilia neema Yake. Katika njia iliyo bora kila mmoja aliye katika uongozi amepata Roho ya Baba. Mwinjilisti anayewaleta watu kwa Kristo anaweza kuwa na moyo wa baba. Mchungaji/mwalimu ambaye anakulea anaweza kuwa na moyo wa baba kwako. Sisi ni watoto tunaokuwa kwa jamii na tunahitaji baba.

Tunashuhudia ya kwamba Mungu amekuwa akiachilia neema ambayo inatuwezesha kuingia katika uwana; tunasema huu ni ujuzi wa tatu. Ujuzi huu unaingiwa na watakatifu ambao mioyo yao imeandalika. Mungu anapatiana kuachiliwa huku kiungu katika mikutano ambapo mtume anahudumu ata wakati neno linatangazwa, na katika mialiko kupitia kuwekea mikono.

Ujuzi huu unakuja kama ufunuo na kama kuwachiliwa kwa nguvu za Roho. Maandiko yanasema "***kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu hao ndio wana wa Mungu"*** **Warumi 8:14**. Matokeo ya mabadiliko katika watakatifu, wakati kuachiliwa kumetendeka inaanza kudhihirisha utukufu wa Mungu.

Matokeo ya kuingia katika uwana ni mabadiliko ya ndani ya kiroho ikidhihirika katika ujasiri mkuu, usalama wa ndani, uweza mkuu wa kupokea urudi na kuonyesha maisha ya nidhamu, ikifunua hatima ya mtu katika kristo, ikitimiza wito na hivyo kufaulu.

Roho wa Uwana

"Kwa kuwa hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hio twalia Abba, yani, baba" Warumi 8:15. Neno kufanyika wana imetumika mara tano katika KJV katika maandiko ya paulo. Neno kufanyika wana ni utafsiri hafifu wa neno la kiyunani ***huoithesia*** ambayo inamaanisha 'kumweka mwana mahali pake'. Haizungumzii kuzaliwa mara ya pili katika jamii ya Mungu **(Yohana 3:3-6).**

Wakati tunazaliwa mara ya pili, tunazaliwa kihalali na Roho **(Yohana 1:12-13).** Kutoka wakati ambapo tumezaliwa mara ya pili tuna ***"uweza [nguvu] wa kufanyika wana [watoto] wa Mungu"*** **Yohna 1:12.** Wakati tunazaliwa mara ya pili, kwanza sisi ni watoto lakini kiasili ndani yetu tuna nguvu za kukua mpaka tufikie umri wa ukomavu. Katika matamshi ya biblia na utamaduni wa biblia, huu ulikuwa ni wakati wa kufanywa wana ambapo mwana katika umri wa miaka thelathini alirithi.

"Kama vile alivyotuchagua katika yeye … kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na Uradhi kwa mapenzi yake. Na usifiwe utukufu wa neema yake" **Waefeso 1:4-6.** Sio kwamba tu tuliwekewa hatima kuzaliwa mara ya pili lakini kwa uhakika wa kuzaliwa mara ya pili tulifanyika kwa imani wana wa Mungu na kwa wakati ufaao tutarithi **(Wagalatia3:26).** Hata hivyo, 'wana' inazungumzia wale ambao wamefikia ukomavu na wamerithi, hivyo wakimwakilisha baba kikamilivu, **"*mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu"* (Waefeso 3:19b).**

Katika **Wagalatia 4:4-7** maandiko inasema ya kwamba kuzaliwa na Roho wa Mungu ni sawa na kuwekwa kama 'wana'. Hii ni kweli lakini bado kungali kuna wakati wa kukua kwa sababu mtoto hapokei urithi. **Warumi 8:17** inatuambia kwamba kama watoto sisi ni warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye. Ni katika kipindi cha kukua katika Kristo ambapo tunapitia nyakati za kuteseka. ***"Mkianguka katika majaribu mbali*** **mbali''** ili ***"saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno''.*** (**Yakobo 1:2-4**). **Wagalatia 4:1-2** iko wazi: watoto, ikawa ni warithi hawawezi kurithi mpaka ***"wakati uliowekwa".***

Urithi ni wa wana

Ni wana ambao hupokea urithi kutoka kwa akina baba, sio watoto wala vijana lakini ni wale ambao wamefika umri wa ukomavu. Kuingia katika uwana ni mwanzo wa kutembea katika urithi ambao umewekwa kwa kila mmoja na baba. Urithi ni kutoka kwa Baba. Mungu anaachilia urithi kwetu kwa njia ya kuachilia neema mioyo yetu inapoandalika na tunaweza kuingia katika uwana. Hatuhitimu kulingana na kazi lakini hata kama vile tunaokolewa kwa neema kupitia imani, hivyo ndivyo ilivyo kazi ya neema ikipokelewa kwa imani inayo tuwezesha kuingia katika uwana **(Waefeso 2:8).** Hii ni ya muhimu sana! Kila kitu kinatoka kwa Mungu kupitia

Bwana Yesu Kristo kwa Roho mtakatifu. Ni karama ya bure. Amepatiana Roho wake mtakatifu! Amepatiana neema yake!

Kuwachiliwa katika uwana ni kazi ya neema
sawa na kuzaliwa mara ya pili
sawa na kupokea Roho mtakatifu.

Ujuzi wa uwana.

Huu ni ujuzi maalumu ambayo kama ujuzi zingine wa kuzaliwa mara ya pili, na kujazwa na roho mtakatifu, iko tofauti kwa kila mtu, Lakini inakuwa wazi kwa maisha ya kila mtu wakati wameupata. Kama mtu hana uhakika kama amezaliwa mara ya pili yawezekana hajaokoka. Vivyo hivyo kama mtu hana uhakika kama amepokea Roho mtakatifu inawezekana hajapokea. Hata kama kuna kitu cha kujua wakati mtu anaingia katika uwana. Mtu anaweza kushuhudia mabadiliko na uhakika wa neema ikifanya kazi katika maisha ya mtu.

Wana wanafunuliwa

Unafikia wakati na mahali pa kuandalika kupokea neema ya uwana
kupokea urithi na kuanza kutembea katika ukomavu
ukitembea katika utimilifu.

Urithi uko ndani ya Kristo; umehakikishiwa kuja kwetu. Mungu ametupa Roho wa kufanyika wana **(Waefeso 1:5).** Roho mtakatifu yuko na kila mmoja wetu na anatufundisha na kutuelekeza katika ukweli wote. Ukweli wa uwana umekuwa katika maandiko.

- ***"Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu hao ndio wana wa Mungu''*** **Warumi 8:14.**
- ***"Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku mingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu"*** **Warumi 8:19.**
- ***"Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu"*** **Wagalatia 4:6-7.**

Ni wana waliofunuliwa watakaoinua laana ya ubatili ya viumbe, wanapotembea ndani ya Roho **(Wagalatia 5:25),** wakitii Baba kwa kikamilifu **(2 Wakorintho 10:6),** hata kama vile Yesu alionyesha

Mtoto alizaliwa; mwana alipatianwa

Yesu mtoto

Yesu alizaliwa kama mwana wa mwanadamu lakini Mungu alimpatiana kama Mwana. ***''Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanaume''*** **Isaia 9:6.** ***"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe…."*** **Yohana 3:16.** Bila shaka Yesu alikuwa ni mwana aliyetanguliwa kufanywa mwana wa Mungu {'alidumu milele'}; alikuwa mmoja na sawa na Mungu **(Yohana 1:1).** Hata hivyo, kama mtu wa kawaida Yesu alikuwa mtoto halisi akiwa na mahitaji ya mtoto. Ninaamini ya kwamba alikuwa mtoto wakupendeza lakini ni kweli alipotea akiwa na umri wa miaka kumi na miwili na akasababisha wazazi wake kuwa na umakini sana. Biblia inasema baada ya tukio hili, **"*akashuka pamoja nao mpaka Nazareti, naye alikuwa akiwatii''*** **Luka 2:51.**

Yesu kijana

Kama kijana tunafikiria Yesu alitayarishwa na akafanya kazi kama seremala. Pia tunajua alikuwa akihudhuria na kuhusika katika ibaada ya kusoma maandiko katika sunagogi **(Luka 4:16).** Ilikuwa ni katika umri wa miaka thelathini ambapo Yesu alibatizwa na baadae akaanza huduma yake **(Luka 3:23).**

Yesu Mwana

Yesu aliingia katika uwana alipobatizwa- Roho wa Mungu, Baba Yake, wakaja juu yake na kutoa uwana; sauti ya Baba ikanena ikitoa uwana ***"Huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye"*** **Mathayo 3:17.**

Kwa wakati huu yesu alikuwa hajafanya kitu bado lakini katika wakati huu aliingia katika utimilifu wa uwana na akaanza kupokea urithi wake **(zaburi 2:7-8).** Yesu sasa akaanza huduma yake. Kupokea Roho Mtakatifu bila kipimo ilikuwa ndiyo funguo za Yesu kutembea katika urithi wake. Yesu alipatikana kwa Roho Mtakatifu; hiyo inamaanisha hakuhitaji kuzaliwa mara ya pili; kila wakati alimjua Baba Yake. Kwa hivyo, Aliambia mama yake ***"hamkujua yakuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba Yangu*****?"** **Luka 2:49**. Hata hivyo mpaka alipopokea Roho wa Baba kikamilifu, hangefanya kazi kuu. Maswali aliyouliza akiwa kijana wa miaka 12 hekaluni, sasa alikuwa akiyajibu kwa Roho wa Mungu.

Wana wa Mungu ni akina nani.

"Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu'' **Warumi 8:14**. Yesu aliongozwa na Roho jangwani kwenda kujaribiwa na shetani na akatoka nyikani **"*na nguvu za Roho Mtakatifu''*** **Luka 4:14**. Kwanzia wakati huo alitenda tu kile Baba alimuonesha kupitia Roho. Kama vile Yesu aliongozwa na Roho mtakatifu na akatembea katika urithi wake ndivyo ilivyo kwa waumini ambao wamekua katika Kristo kutoka utoto kupitia ujuzi wa huduma kama "*kijana'* na sasa kuongozwa na Roho Mtakatifu kama mwana, akifanya kazi za Baba.

Yesu ndiye ***"mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi"*** **Warumi 8:29**; tumewekewa hatima tufananishwe na yeye. Tunastahili kubadilishwa katika uwana wake. Wakati Yesu aliingia katika uwana na akakamilishwa, kisha aliwaongoza wana wengi katika utukufu (**Waebrania 2:10**). Hili ndilo lengo la Mungu kwa waumini wote: wawe wana waliodhihirishwa. Wana ni wale wanaoongozwa na Roho Mtakatifu; wale ambao wamepokea Roho bila kipimo.

Utukufu unafunuliwa kupitia wana wa Mungu

Roho wa kufanyika wana anakuja kwetu wakati tunapokea kikamilifu Roha wa Baba "***kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku mingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu''*** **Warumi 8:19,** na ***"kwa kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu hata viingie kwenye uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu*****"*** **aya 21**. Kanisa linastahili kutembea katika utukufu. Dunia yote itajazwa na utukufu wa Mungu **(Hesabu 4:21)** kupitia kufunuliwa kwa wana. ***"Maarifa ya utukufu wa BWANA"*** utajaza dunia ***"kama maji yafunikavyo bahari"*** **Habakuki 2:14**.

Umeshangaa: haya yaweza kutendeka aje? Utukufu wa Mungu utafunika aje dunia? Aya katika Warumi 8 inatupa mwangaza. Ni wakati tunapoongozwa na Roho wa Mungu. Roho Mtakatifu atatuongoza katika ukweli wote; Roho Mtakatifu atatutia nguvu na kuwachilia karama zake kupitia sisi. Maandiko yanaweka wazi kwamba wana wanakamilishwa kupitia mateso na hio ndio funguo ya utukufu kuachiliwa.

Roho na nguvu ya Eliya.

Kuja katika uwana ni kupokea roho na nguvu ya Eliya. Kufaulu kwa huduma ya Eliya ilikuwa ni kugeuza mioyo ya watu imrejee Mungu katika **1 Wafalme 18**. Eliya alitembea katika uwana. Mitume ndio ambao Mungu amepatia roho wa Eliya. Roho wa Eliya anawapatia mitume Roho wa baba kwa watu wa Mungu, ikiwezesha kanisa kukua katika ukomavu. Roho huo wa Eliya anapeanwa kwa watoto wa Mungu wapokee akina baba, hivyo kuingia katika uwana. Wakati tunakuja katika uwana, sasa tunatembea katika ukomavu, hivyo ni, kama akina baba na matokeo itakuwa kwamba tumebarikiwa na wana wengi wa kiroho.

Roho wa ukomavu

Waumini wote waliozaliwa mara ya pili ni warithi, lakini watoto kijumla hawarithi – lazima wangojee mpaka wafikishe umri. Katika tabia za wayahudi wakati wa ukomavu ama[uwana] ambapo mtoto alipokea ambacho alikuwa amewekewa ilikuwa miaka 30. Kwa hivyo Yesu alikuwa na umri wa miaka 30 wakati alimuendea Yohana mbatizaji. Yohana alikuwa ameanza huduma tu na kama umri wa miaka 30. Mfalme Daudi alifanyika mfalme Hebroni akiwa na umri wa miaka 30 **(2 Samueli 5:4).** Yusufu alikuwa na umri wa miaka 30 wakati aliachiliwa kutoka korokoro ili awe waziri mkuu kule Misri. Mgombea wa nafasi ya kuhani mkuu alikuwa awe na miaka 30.

Neema imeachiliwa

Neema ambayo Mungu ameachilia kuleta watu wake katika uwana, ni ajabu. Neema hii ni hakika, inaweza kujulikana na ni ya kubadilisha maisha. Ni kuwachiliwa katika uwana ambapo tunapokea na kuanza kutembea katika urithi wetu. Tunaanza kutembea katika ukomavu wakati tunafikisha umri. Hata kama vile Yesu alitembea katika urithi ambao Baba alikua amemuekea, sasa Mungu anatuita katika kutembea kulikokomaa na yeye.

Sisi sio watoto tena! Hatustahili kuchanganywa na miundo isiyo ya kiungu ya makanisa! Hatustahili kutawaliwa na kuwekewa mipaka na tamaduni za watu, ama kwa mamlaka ya mtu! Tunastahili kutembea katika mamlaka ya Bwana Yesu Kristo ambayo haina kipimo, ambayo inatuweka huru, ambayo ina mazao na inafanya kazi.

Bwana asifiwe! Ameahidi kutuma Roho wa Eliya na hivyo ndivyo anafanya akiinua akina baba, Viongozi wa kweli wa kitume wakiwa na kushughulika kwa mzazi, kwa kizazi kingine cha viongozi ambao wanafundishwa wale wako tayari katika uongozi na watakatifu wote.

Bwana asifiwe! Roho wa Eliya ameachiliwa na wana wengi wamepatianwa. Watoto wa Mungu wamekuja katika umri wa ukomavu wakipokea Roho, neema ikiachiliwa kutembea katika ukomavu.

Tunafanyika wana kwa neema kupitia imani, ni karama ya Mungu, sio kwa kazi ili mtu awae yote ajivune.

Sura ya Pili

KUITWA KUWA KIKUNDI CHA KITUME

Kwa moyo moja

Mdo 1:13a-14 *"Hata walipoingia, wakapanda orofani, walipokuwa wakikaa; Hata wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali, pamoja nao wanawake, na Mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake".*

Wakawa wakidumu

Mdo 2:41-47 "*Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*
Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.
Kila mtu akaingiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume. Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika, wakiuza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja.
Na sikuzote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya Hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."

Kumwagwa kwa Roho

Yohana 7:37-39 "*Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama, akapasa sauti yake akisema, Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo aliliesema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa".*

Kikundi cha kwanza cha kitume

Kama tukisoma sura za kwanza za kitabu cha Mdo, tunaona kuundwa kwa kikundi cha kwanza cha kitume. Kikundi hiki kilihusisha mitume ambao walikuwa na Yesu, **"*pamoja nao wanawake, na Mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake*" Mdo 1:14**, hivyo hivyo na ndugu wengine, ***"jumla ya majina ilipata mia na ishirini"* Mdo 15b**. Walikuwa waume na wake ambao walikuwa katika umoja na moyo mmoja **(mdo 1:14 na 2:1);** walikuwa na ***"moyo mmoja na roho moja"* Mdo 4:32**. Kikundi hiki cha kitume kilijitolea kwa maombi. Ilikuwa ni kupitia maombi ambapo Petro aliongozwa na Roho Mtakatifu kumchagua Mathiya kuchukua nafasi ya Yuda kama mtume wa kumi na wawili.

Kuweka katika mpangilio, tayari kupokea maelfu ya waumini wapya

Kikundi cha kitume ni lazima kingewekwa katika mpangilio. Yesu alikuwa amewafundisha mitume kumi na wawili na wanafunzi wengine wengi. Kikudi kilicho ngonjea katika chumba cha juu kilihusisha mitume kumi na mmoja na wanafunzi wengine wengi ambao walikuwa katika ngazi tofauti za maandalizi na ujuzi. Hakika mama ya Yesu na ndugu zake walikuwa waumini wapya **(1Wakorintho 15:7).** Kuwekwa katika mpangilio kwa mtume wa kumi na wawili, Mathiya, ilikuwa ni kitendo cha mwisho katika kuandaa kuja kwa Roho Mtakatifu. Ilikuwa ni kwa kikundi hiki cha kitume ambapo *'kuliwekwa katika mpangilio'* na *'katika kusudi moja'* ambapo Roho Mtakatifu alikuja.

Petro aliweza kusimama kwa niaba ya wale kumi na mmoja na kuhubiri injili ya nguvu akiwaita watu ***"tubuni mkabatizwe, kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu".*** **Mdo 2:38**. Kikundi hiki cha kitume kiliandaliwa na kilikuwa tayari kuwapokea waumini wapya elfu tatu kwa siku moja! Na pamoja ***"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali."*** **Mdo2:42**.

Tumeitwa tuwe sehemu ya kikundi kama hicho cha kitume:
tukiunganishwa kwa 'kusudi moja',
na moyo mmoja na nia moja kama mwili huu wa waumini.

Katika siku hizi Bwana anainua vikundi vya kiutume, vikiongozwa na mitume, pakiwepo karama tano za huduma, kufanya kazi kama mwili. Kila sehemu ya mwili ***"ikiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadili ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo"*** **Waefeso 4:16.**
Mungu anaangalia vikundi vya kiutume ambavyo anaweza kuongezea nafsi elfu tatu kwa siku moja!

Kuitwa kuwa mtu wa kitume

Wito wa Mungu ni wito wa kuwa mtu wa kitume: kuitwa kutoka dunia kumfuata Yesu, kuachana na vyote na kutafuta kwanza ufalme wa Mungu, kuuchukua msalaba wa kujikana na kukumbatia mateso kwa ajili yake, na kuenda kushuhudia na kuhudumu popote ambapo Mungu atakutuma. Utiifu wa wito huu unahitaji kufundishwa tena ya maisha ya mtu kuweka kipa umbele kwa malengo yote ya maisha na mambo yote tunayojihusisha nayo ili tuingie kwenye wito wa Mungu.

Mwito wa Mungu sio kuwa mkristo mwema pekee; sio kufaulu katika maisha ya kijamii kama hio ndio hatima; sio kufaulu katika biashara, ila iwe ni mapenzi ya Mungu. Wito wa Mungu ni kutimiza kusudi la Mungu: ***"tumeitwa kulingana na kusudi lake"***. Kusudi la Mungu linajulikana kwetu kupitia ufahamu wa siri kulingana na **Waefeso 3:1-11.**

Kuitwa kuwa kanisa la kitume.

Kanisa la kitume katika Agano jipya halikuwa la kiudini na hivyo kanisa la kitume la siku za mwisho. Kila mahali miongoni mwetu waumini na viongozi wa kikristo wamejipatiana katika makubaliano, na kwa hakika sio kujipatiana kwa mwito wa Mungu kama ilivyo wekwa na Yesu na mitume katika Biblia ama kupuuza kila ambacho Biblia inasema. Wakristo kama hao wanapendekeza njia za utamaduni ya watu kuliko kulitii neno la Mungu, wakifanya makosa kujipatiana kwa dini ama tamaduni kuliko uaminifu kwa neno la Mungu.

Yesu anatakiwa kuwa na ukuu

Mara kwa mara mtu akishuhudia kwa imani yake katika Yesu, swali linalotokea ni, 'hua unaenda kanisa gani?' Wazo la mwanadamu la utendaji la kanisa kihistoria limeinuliwa kuliko Yesu na ilahali Yesu anatakiwa kila mara kuinuliwa juu ya mambo yote **(Wakolosai1:18)**. Wakristo kwa jumla wanaongea zaidi kuhusu makanisa yao na kile kinatedeka (ratiba) kuliko Yesu na kile kinatendeka katika kutembea kwao na Mungu. Hii ni kwa sababu tumelifanya kanisa kuwa 'letu' kuliko liwe kanisa la Yesu Kristo kulingana na Agano jipya.

Kuyafikia Mataifa kupitia neema na utume.

Katika **Warumi 1:5,** Paulo anasema kwamba yeye na kanisa la siku zake, mwili wa Kristo, "***tulipokea neema na utume, ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani, kwa ajili ya jina lake".*** Sio kanisa la kikatoleki la Rumi, wala kanisa la kale la mtakatifu Tomaso katika kusini ya India, wala makanisa ya karismatiki iliyofaulu kuyafikia maelfu na pia makumi ya maelfu, wala pia mitandao ya kisasa ya makanisa yanayo jitawala au vikundi vya maombi vya wachungaji ambazo zitayafikia mataifa kwa injili na itafanyika chumvi na nuru katika jamii.

Biblia inasema ni kupitia neema na utume
iliyopokelewa kutoka kwa Baba kupitia Kristo
ambayo inaelekeza kwa utiifu wa imani katika mataifa.

Kwa kuwa wakristo wameacha njia ya Mungu ya maisha ya Kanisa na utendaji wa huduma wa biblia, kanisa la kikristo kwa jumla limepoteza nafasi yake ya kweli katika ulimwengu ya kuwa chumvi na nuru. Kihistoria katika Australia, azimio la Bunge la ndoa lilishikilia kwamba ndoa ni kati ya mwanamume na mwanamke. Lakini mwaka wa 2017 walibadirisha na sasa Australia wanakubalisha watu wa jinsia moja kuoana. Jambo baya kwa hii ni kwamba dini moja kubwa, walitangulia serekali na kubariki ndoa ya watu wa jinsia moja, na wakasema kitendo hicho kiko kiko sawa. Sela za makanisa hayo ni mfano wa kusikitika wa kanisa la umma. Kunatakiwa kuwa na marekebisho kamili wa kile tunaita kanisa ili liwe kanisa la Yesu Kristo ambalo anajenga.

Marekebisho ya kitume ya kanisa

Historia ya marekebisho

Katika siku hizi, Mungu ameinua mitume na baadhi ya mitume wanaliita kanisa kwa marekebisho. Marekebisho kama hayo yanaita mabadiriko makuu kuliko yale yaliyo ongozwa na Luther katika Karne ya kumi na sita. Katika nyakati hizo mabadiriko ya kihistoria ilitengenezewa kanisani lakini miundo ya taasisi mingi na utendaji haukubadilika. Waluteri baabaye walifanyika kuwa mashirika yaliyofadhiliwa na Serekali katika Ujerumani, kama walivyotenda Wa Calvinisti katika Swizerland na walimbadilika wa Dutch katika Holland. Waanglikana kwa kweli katika Uingereza wamekuweko kwa msaada wa mamlaka. Kutoka karne ya nne, Kanisa Katoleki la kirumi lilikuwa kikamilifu limeungana na uongozi unaotawala ya utawala wa uongozi baadaye kule Uropa. Kanisa la Kiprotestanti kwa hakika ni kanisa mwenza ya Kirumi na kulipokuwa na mabadiliko mengi makali katika fundisho na mahubiri na kweli kwa sehemu zilirejeshwa, hakujakuwa na jitihada za tamasha kurejelea ukristo wa kitume kama ilivyo fundishwa na ikafanywa katika Agano Jipya.

Ukristo wa kitume utateswa

Wakati huo huo kote kote katika historia ya ukristo kumekuwa na mifuko ya ukristo wa kitume. *Popote ambapo mafundisho ya kitume na utendaji ziliimarishwa katika historia ya kanisa mateso mazito yaliinuka dhidi ya wahubiri hao na makanisa. Mateso haya yalisukumwa kwao na makanisa ambayo yalikuwa yanapokea msaada, kutoka kwa serekali. Wakati wa Luther, waumini walikuwa wanaitwa Anabaptists; hii ilikuwa ni kwa sababu walikuwa wakibatiza waumini tena ambao walikuwa wamebatizwa wakiwa watoto. Waluteri walipinga sana kama vile wakatoliki walikuwa wameipinga. Yesu kwa hakika alikuwa amewaonya wale mitume 12 wakati aliwaagiza ya kwamba watakutana na mateso mengi **(Mathayo 10:16-36).**

['The pilgrim church," by E.H. Broadbent, a pickering classic, 1931- historia bora ya kanisa la kweli, kanisa ambalo msingi wake ni katika maandiko katika kipindi cha kanisa. Kitabu hiki kimechapishwa tena hivi punde.]

Kanisa la kitaasisi na kanisa la kitume

Leo watu wengi wa Mungu wamehusika na kanisa la kitaasisi. Wengine ni wahubiri, waalimu na wahuduma ambao wameshawishika watafanya vyema wakibaki katika taasisi, na ndivyo. Hata hivyo tunahitaji kujifundisha kutoka kwa historia na haswa tunastahili kuwa watiifu wa maneno ya Bwana Yesu Kristo. Hakufa msalabani aimarishe makanisa ya kidini. Dini ni mpango wa mwanadamu kuanzia mwanzo hadi mwisho. Aliwachagua mitume 12 wawe jiwe la msingi na wajenzi wa kanisa.

Yesu aliwafundisha na akawachagua mitume12: hao akawaaminia kuzaliwa na kuundwa kwa kanisa; kwa hao alitoa funguo za ufalme wa mbinguni. Analijenga kanisa lake kupitia mitume na hili ndilo kanisa ambalo litalishinda milango ya kuzimu.

Kuundwa kwa vikundi vya kitume

Leo tunaona kuundwa kwa vikundi vya kitume katika matayarisho ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu ambaye ataachilia ufifio wa siku za mwisho kabla ya kuja kwa Bwana.

Roho Mtakatifu alikuja kutimiza pentekosti.

Katika **Mdo 1&2** tunaona maandalizi na kuweka mipangilio ya mwisho ya kikundi cha kwanza cha kitume na kwa kuja kwa Roho Mtakatifu kwa kikundi hicho katika kutimiza kile Yesu alikuwa amewaambia katika kutimizwa kwa sikukuu ya Pentekosti. [sikukuu za majuma katika Agano la kale- ona **Mambo ya Walawi 23:15-22].** Wale wanafunzi mia na ishirini walikuwa wamekusanyika katika kutii maagizo ya Yesu, ***"lakini kaeni humo mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu"*** **Luka 24:49**. Walipokuwa wakingojea katika maombi na dua katika moyo mmoja, Bwana akamuonyesha Petro ya kwamba mtume wa kumi na mbili ni lazima awekwe. Wakati haya yalitendeka kwa mwelekeo wa kiungu, kisha siku ya pentekoste ***"ingekuja kikamilifu"*** **Mdo 2:1.** Roho Mtakatifu alikuja katika kutimiza sikukuu, ambayo ilikuwa imeanzilishwa na Mungu wakati Mungu alimpa Musa sheria katika mlima Sinai miaka 1500 kabla.

Sikukuu ya Vibanda lazima itimizwe

Yesu ametabiri wazi kuja kwa nguvu kwa Roho Mtakatifu kutimiza sikukuu ya vibanda [mvua ya mwisho ya **Yoeli 2:23**] katika **Yohana 7:37-39**. **Yohana 7** ni mazingira ya sikukuu ya vibanda. Yesu alienda kisirisiri kisha akaonekana miongoni mwa kusanyiko kubwa ya siku ya 8, **"*siku ile kubwa ya sikukuu''* aya 37**. Mambo ya **Walawi 23** inatwambia kwamba kwa siku saba

watu wa Mungu walikaa katika vibanda vilivyojengwa na matawi ya mielezi na matawi ya miti, lakini siku ya nane ilikuwa ni siku ya kusanyiko ya sadaka, siku takatifu, sabato **(aya 33-43).**

Sikukuu ni kalenda ya kiunabii

Sikukuu za Israeli zilipatianwa na Mungu kwa Musa na ni kalenda ya kiunabii ambayo kupitia hiyo tunaona utenda kazi wa kusudi la Mungu likitimizwa

- Pasaka na pentekosti zimetimizwa katika Kristo, kupitia kufa na kufufuka kwake na kuja kwa Roho Mtakatifu na zimetimizwa katika ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili na kujazwa kwa Roho Mtakatifu kwa mkristo.
- Kupulizwa kwa baragumu na siku ya upatanisho na sikukuu ya vibanda zimetimizwa katika Kristo na sasa zinatimizwa katika kanisa siku za mwisho.

Mwanzo Mungu aliambia Musa ya kwamba sikukuu ya vibanda katika mwezi wa saba ilikuwa isisherehekewe mpaka watu wa Mungu wafike kwa nchi. Nchi yetu ni ahadi za Mungu katika mwisho wa nyakati, kanisa linatakiwa kuja katika ukomavu (nchi) kulingana na ahadi za Mungu.

Kuelewa neno kiunabii

Kupulizwa kwa baragumu inaweza kutafsiriwa kama neno la Mungu la kiunabii likija kuandaa kanisa kwa kuja kwa Bwana. Tangu vita vya pili vya ulimwengu kumekuwa na uamsho wa kushangaza wa neno la Mungu duniani. Katika mwaka wa 1948 kulikuwa na kuachiliwa kwa ajabu kwa ufunuo kupitia kile kilichoitwa ufifio wa mvua ya siku ya mwisho. Mwisho wa mwaka wa 1940 na 1950 waliona kuinuliwa kwa uponyaji mkuu kwa kuinuliwa kwa wainjilisti walioponya na tangu wakati huo, kumekuwa na kuendelea kwa kurejeshwa kwa ukweli, huduma na miondoko ya ufifio, ikiandaa kanisa kwa mwisho wa nyakati.

Maisha yasiyo na dhambi

Siku ya upatanisho ilikuwa imetimizwa katika Kristo wakati aliingia patakatifu pa patakatifu kwa damu yake **(Waebrania 9:11-12**) akitutengenezea njia. Hata hivyo siku ya Upatanisho ni kuwa na utendakazi katika maisha ya kanisa na maisha ya muumini ambapo tunatembea huru kutokana na dhambi zote, tukijua ya kwamba Yesu ametuondolea dhambi zote kikamilifu. Huku ni kuachiliwa kwa kutembea katika ukomavu kuingia katika utimilifu. Hili ndilo lengo lililonenwa katika **1 Wathesalonike 5:23, *"Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo''***

Kinywaji kwa waliopotea kupitia waumini

Sikukuu ya Vibanda ilihusisha siku saba za kuishi kwenye vibanda vya muda, ikifuatwa na siku ya nane ambapo kusanyiko lote lilikuwa likutanike pamoja kutoa sadaka kwa moto. Yesu alizungumza habari ya siku ya nane. Alisimama kati na akalia kwa sababu ya vikundi viwili vya watu **(Yohanna7:37-38):**

- Kwanza alilia kwa walio na 'kiu' hawa ni wale hawajaokoka, walio na kiu ya ukweli, kwa wokovu;
- Pili alilia kwa sababu ya waumini, ***'yeyote aniaminiye mimi',*** kutoka ndani mwake, mito ya maji ya uzima itatiririka ikileta kinywaji kwa watu walio na kiu siku hiyo.

Siku hiyo inaongea habari ya siku za mwisho, kabla ya kuja kwa Bwana katika utukufu wakati Yesu ataonekana katika kanisa lake tukufu, lililokomaa. Atapatia Roho Mtakatifu, **"*mvua ya mwisho",*** kumwagwa kwa Roho Mtakatifu wake katika kutimizwa kwa Yoeli na katika kutimizwa kwa ahadi yake ya ajabu ya kiunabii katika **Yohana 7. Aya 39** yasema alikuwa anazungumza kuhusu Roho Mtakatifu.

Kikundi cha kitume ni nini?

Kikundi cha kitume ni mwili wa watakatifu ambao wameitwa pamoja katika kujipatiana kuona ufalme wa Mungu umeimarishwa duniani miongoni mwa mataifa. Watakatifu hawa wameitwa kutoka mashirika na taasisi ambapo utiifu wazi wa Kristo umetawaliwa kwa sheria na utendaji wa taasisi na mashirika. Katika vikundi kama hivi, huduma zote na karama ambazo Mungu amepatiana katika Agano Jipya zinapata nafasi yake na kufanya kazi kikamilifu.

Vikundi hivi vimetanda kwa mataifa; vikiongozwa na mtume;
yana tabia za washirika wote wa kikundi kuwa na ufahamu
wa wito wa Mungu na ufunuo wa nguvu wa uwana

Mfano wa Agano la kale wa kikundi cha kitume

Warekabi

Katika **Yeremia 35** tunasoma habari ya ukoo wa watu waliitwa 'Warekabi'. Wao ni kielelezo cha kikundi cha kitume na ushawishi wa nguvu ambao baba wa Kiroho anaweza kuwa nao. Ukoo huu uliishi chini ya kifuniko cha baba wao wa kitume kwa vizazi akiisha kuishi.

Warekabi wanawekewa mtihani

Eneo limewekwa katika **Yeremiah 35:1-2,** "***Neno hili ndilo lililomjia Yeremiah, kutoka kwa BWANA, katika siku za Yehoyakimu, mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, kusema, Enenda nyumbani kwa Warekabi, ukanene nao, ukawalete nyumbani kwa BWANA, katika chumba kimoja, ukawape divai wanywe".*** Yeremia alikuwa ni nabii wa Bwana aliyeaminiwa na Mungu akamwambia kufanya jambo fulani. Alikuwa awaendee Warekabi, awalete katika nyumba ya Bwana na awape divai wanywe. Yeremia alitii neno la Bwana: ***"nikawaleta ndani ya nyumba ya BWANA, ndani ya chumba cha wana wa Hanani, mwana wa igdalia, mtu wa Mungu…"*** **aya 4.** ***"Nikaweka mabakuli yaliyojaa divai, na vikombe, mbele ya wana wa nyumba ya Warekabi, nikawaambia, Nyweni divai"*** **(aya 5).**

Warekabi walipita mtihani

Hata hivyo hawa wana wa Rekabu hawakufaya kama walipoagizwa na Yeremia, "***Lakini wakasema, hatutakunywa divai; kwa maana Yonadabu, mwana wa Rekabu, baba yetu, alituamuru, akisema, Msinywe divai, ninyi wala wana wenu, hata milele" aya 6.*** Walijua jinsi ya kuitikia katika msingi wa '***fundisho la kweli'*** ambalo walikuwa wamefundishwa. Kuitikia kwao kulikuwa na msingi katika mafundisho ambayo walikuwa wamefikishiwa kutoka kizazi hadi kizazi. Paulo mtume alimchagua Timotheo kuwakabidhi **"*Watu waaminifu"*** mambo ambayo alikuwa amejifundisha na kupokea kutoka kwa Paulo ili wawafundishe wengine. Fundisho la kweli, lenye msingi wa neno la akina baba, haswa Yesu na Paulo, linastahili lipitishwe kutoka kizazi hadi kizazi na linastahili kupokelewa, hata katika karne ya ishirini na moja.

Maagizo ya Yonadabu yallifunika maisha yote

Mtu huyu Yonadabu alikuwa ameishi miaka 200 kabla ya tukio hili. Hapana yeyote katika kizazi hiki ambaye aliyemfahamu mtu huyu, lakini uzao wake wakali wametii maagizo yaliotolewa na baba yao [mtume wao]. "***Nasi tumetii sauti ya Yonadabu, mwana wa Rekabu, baba yetu, katika yote aliyotuamuru, kwamba tusinywe divai siku zetu zote, sisi, na wake zetu na wana wetu, na binti zetu"*** **Yeremia 35:8**. 'Baba' yao pia alikuwa amewaambia "***wala msijenge nyumba, wala msipande mbegu, wala msipande mizabibu, wala msiwe nayo; bali siku zenu zote mtakaa katika hema, mpate kuishi siku nyingi katika nchi ambayo mtakaa ndani yake hali ya wageni"*** **aya 7** na walikuwa wametii neno hili **(aya 9 na 10).**

Hawa watu hawakuwa wana wa Israeli, lakini walidumu katika nchi ya Waisraeli. Kwa zaidi ya miaka 200 walibaki waaminifu kwa sauti ya baba wao wa kitume ambaye alisema, 'mkiitii sauti yangu mtapata ufanisi na kubarikiwa'. **[2 Wafalme 10:15 na 16** inatanguliza Yonadabu: yeye ndiye yule moyo wake ulikuwa mmoja na mfalme Yehu katika kulitimiza kusudi la Mungu siku hiyo].

Mungu anataka tujifundishe kutoka kwa kikundi hiki cha kitume

Bwana alimpa Yeremia maagizo zaidi, ***"Enenda ukawaambie wana wa Yuda, na wenyeji wa Yerusalemu, Je! hamtaki kupokea mafundisho, myasikilize maneno yangu? Asema BWANA. Maneno ya Yonadabu, mwana wa Rekabu, aliyowaamuru wanawe, kwamba wasinywe divai, yametimizwa, na hata leo hawanywi; maana waitii hiyo amri ya baba yao, lakini mimi nimesema nanyi, nikiamka mapema na kunena, bali ninyi hamkunisikiliza mimi"*** **aya 13-14.** Huu ni mfano wa kikundi cha kitume ambao, baada ya mamia ya miaka, walikuwa wanatii sauti ya baba wao wa kitume na kwa sababu walikuwa wametii, walibarikiwa.

Watu wa kitume wanajulikana

Mungu aliweka ukoo huu kama kikundi cha watu walio kitamburisho hata kama walikuwa wageni na wapitaji katika nchi ya ugeni kwa mamia ya miaka. Walikuwa na ushuhuda kati ya watu ambapo waliishi kama watu walio tofauti. Kila mtu alijua walikuwa akina nani. Wakati Bwana alimuambia Yeremia aende kwa Warekabu, haikumbidi kuuliza, 'wao ni akina nani?'

Weka maagizo ya baba

Bwana alitaka kutumia kuitikia kwa wana wa Rekabu kuzungumza na watu wake, "***pia niliwapeleka watumishi wangu wote, manabii, kwenu ninyi, nikiamka mapema na kuwapeleka, nikisema, Rudini sasa, kila mtu na aiache njia yake baya, mkatengeneze matendo yenu, wala msiwafuate miungu mingine, ili kuwatumikia, nanyi mtakaa katika nchi hii, niliyowapa ninyi na baba zenu, lakini hamkutega masikio yenu, wala hamkunisikiliza. Basi, kwa kuwa wana wa Yonadabu, mwana wa Rekabu, wameitimiza amri ya baba yao aliyowaamuru, lakini watu hawa hawakunisikiliza mimi"*** **Yeremia 35:15-16.**

Mungu hudhawabu waaminifu

Kipitia kitendo cha kinabii, Mungu alitumia jamii hii ya kitume kama mfano kwa watu wake kuwaonyesha aliyotarajia kutoka kwao. Mungu alitangaza hukumu kwa watu wake kwa sababu hawajatii neno alilonena nao **(aya 17)** kupitia Musa na manabii. Jamii hii tiifu ya kitume itakuwa na msimamo mbele ya Mungu: "***Basi, kwa sababu hiyo, BWANA wa majeshi, Mungu***

wa Israeli, asema hivi, Yonadabu, mwana wa Rekabu, hatakosa kuwa na mtu wa kusimama mbele zangu hata milele" **aya19.**

Vikundi vya kitume katika Agano Jipya

Katika Agano Jipya, kuna akina baba wa kitume wazi na mfano wa vikundi lakini kama katika Agano la Kale, watu wengi wa Mungu hawajalisikia neno la akina baba [mitume]. Warekabu wanaonyesha asili ya kikundi cha kitume. Kihistoria na wakati huu makanisa ya kikristo yamegawanyika katika dini, kila mmoja na mafundisho yao na mafundisho ya sharti, pasina makubaliano kwa kuwa hawana baba ambaye neno lake wanalitii.

Akina baba wa kitume.

Akina baba wa kitume waliandika maandiko chini ya maelekezi ya Roho Mtakatifu. Yesu ndiye mtume wetu **(Waebrania 3:1)** na sisi tu wana wake **(Waebrania 2:13),** na haswa Paulo ni mtume kwa watu wa mataifa **(Wagalatia2:8).** Kwa hivyo, kanisa katika wakati wote lilitakiwa kuwa tiifu kwa neno la Yesu katika injili na maneno ya akina baba wa kiroho katika nyaraka. Kama kanisa lingekuwa tiifu hatungekuwa na kanisa nyonge la kikristo lililogawanyika ambalo halitambuliki kimaandiko. Hata hivyo sasa Mungu anarejesha mitume (akina baba) na kuinua vikundi vya kitume ambavyo vinaundwa juu ya muundo wa kitume katika maandiko.

Tukijinyenyekesha na kurudia Bwana, kuliweka neno lake na kuyatenda yote alioagiza kupitia Yesu na kupitia maandiko ya mitume wa Yesu katika Agano Jipya, tutabarikiwa, tutafaulu na kufanikiwa.

Ni wakati wa kutambua tena maisha ya kitume

Neno ambalo Bwana amefunua katika **Yeremia 35** linafaa sana. Ni mfano katika maandiko wa kikundi cha kitume - jamii ya watu wanaohusiana kupitia baba mmoja, wakiwa wanatii maagizo yake kwa zaidi ya miaka 200 na baadaye kubarikiwa kwa sababu ya kutii kwao. Hata hivyo kanisa leo limekuwa kama wana wa Israeli na hatujatii maagizo ya baba zetu wa kiroho, kwa hivyo kuingia kwenye hukumu ya Mungu badala ya Baraka zake.

Ni wakati wa kanisa kuwa watiifu kwa maneno ya akina baba wa kitume, ili kila mtu awe amewekwa vyema "***mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, Naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni"*** **Waefeso 2: 20.** Kisha "***ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu"*** **aya 19.** Kama Warekabu watiifu tutakuwa na ushuhuda na tutapata kibali katika jamii kama kikundi cha kwanza cha kitume katika **Mdo 2:42-47**.

Mpango wa Mungu unafanya kazi katika mwisho wa nyakati

- *Katika mwisho wa nyakati Mungu anakusanya vikundi vya waumini vilivyo jipatiana katika vikundi vya kitume kutayarishwa na kuandaliwa na kuwekwa vyema ili wafanye kazi.*

- *Vikundi hivi vitakuwa pamoja kwa kusudi moja, moyo mmoja na nia moja kulitumikia kusudi la Mungu, kuyafikia mataifa na kuwa jamii ya nuru na ukweli na upendo.*

- *Ni kwa vikundi hivi vya waumini vilivyoungana na kujipatiana na uongozi wa kitume ambapoMungu atamwaga Roho wake kwa njia ambayo maelfu wanaweza kuokolewa katika kila mahali.*

- *Ni kutoka kwa maeneo ya ndani ya moyo wa waumini vikiungwa kama vikundi na mkono wa Mungu ambapo mito ya maji yaliyo hai yatatiririka kuleta kinywaji kwa wenye kiu.*

- *Hili litakuwa jambo la ulimwengu na kwa mwisho huu watakatifu katika kila taifa wanaitikia ujumbe wa kitume na kupokea neema kutembea katika utimilifu wa wito wa Mungu. Kila nafsi itasikia na kila moyo wenye kiu utapokea wokovu.*

Sura ya tatu (a)

SIRI YA KANISA - Sehemu ya kwanza

Kujua siri – Waefeso 3:3-6

"Ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache. Kwa hayo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo. Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho; ya kwamba mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi, wa ahadi yake iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili ... **aya 8-11** *ya kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika; na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote; ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu".*

Naye alitoa wengine - Waefeso 4:8-11

"'Alipopaa juu aliteka mateka, akawapa wanadamu vipawa'.
... Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu".

Kanisa tukufu – Waefeso 5:26-27

"Ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. **Aya 32** *Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na kanisa".*

Kanisa katika Yerusalemu.

Kanisa la kitume

Kanisa la kwanza lilikua katika Yerusalemu kukiwa na umati uliojiunga kwa hesabu yao. Wakati kanisa la Yerusalemu lilianza kuwa kanisa la *'***kutuma'** hivyo ni kanisa la kitume. Hakika, ilichukuwa mateso kuwatoa wanafunzi Yerusalemu kutimiza maagizo ya Yesu kuenenda Samaria na misho yote ya dunia **(Mdo 1:8** na **8:1, 4).**

Kitengo cha wayahudi

Mara tu injili ilitanda makanisa yakapandwa katika maeneo kwingine, kanisa la Yerusalemu lilifanyika kanisa 'mama'. Kanisa hili lilikuwa tu na waumini wa kiyahudi na kwa miaka mingi waumini walijulikana kama kitengo cha wayahudi ambacho pia kiliitwa 'watu wa njia', wakitambua ya kwamba walikuwa wanamwamini Yesu, na walikuwa watu tofauti. Wakati Petro aliripoti kuenda katika nyumba ya mtu wa mataifa ya Korinelio kuhubiri Yesu, hakupokelewa kwa urahisi na wandugu wayahudi. Mpaka wakati waumini wayahudi hawakuwa

na mawazo ya watu wasio wayahudi wakifanyika sehemu ya kanisa ila tu kwa njia ya kufanywa wayahudi na kujiunga na dini ya kiyahudi.

Wayahudi na watu wa mataifa kanisani.

Baadae katika **Mdo 15**, baraza spesheli la kanisa lilikutanika Yerusalemu kutafakari zaidi kuhusu watu wa mataifa kujiunga kanisani. Kwa wakati huu kulikuwa na waumini wengi wa kimataifa, pakiwepo watu wa mataifa na waumini wayahudi kanisani pamoja katika miji. Hata hivyo palitokea shinda baya kwa sababu ya waumini wayahudi waliokuwa Yerusalemu walikuwa wakiendelesha sheria za Musa na zilikuwa ni sehemu za ibada hekaluni. Imani yao ilikuwa ya kwamba watu wa mataifa waliookolewa walipaswa kuzitekeleza sheria na pia kupata tohara. Barua ya Paulo kwa Wagalatia, inashughulikia maswala haya ambayo yaliwakumba waumini wa mataifa anaposhutumu mafundisho ya kiyahudi.

Upungufu wa kanisa Yerusalemu

Kanisa mama la Yerusalemu halikutoka katika tabia za Uyahudi na baada ya kuharibika kwa Yerusalemu na hekalu katika AD 70, kanisa la Uyahudi lilipotea katika historia. Kanisa la kwanza Yerusalemu halikutimiza mabadiliko kutoka kwa Uyahudi kuingia kwa ukristo hata kama kazi kubwa zilitendeka Yerusalemu kupitia nguvu za Roho Mtakatifu na kwa jina la Yesu Kristo.

Watu wa mataifa wanapokea Roho Mtakatifu

Katika **Mdo 10,** watu wa mataifa walisikia neno kupitia mtume Petro. Tunajua kutoka kwa maandiko ya kwamba huu ulikuwa mkutano uliopangwa kiungu. Maandiko yanasema ***"Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliosikia lile neno"*** **aya 44.** Hii ilidhihirisha upenyo mkubwa katika himaya ya mbinguni kwa injili. Kama matokeo Roho wa Mungu aliweza kupokelewa na mataifa. Upenyo mwingine ulipatikana Antiokia ambapo wale ambao walikuwa wametawanyika ***"wakasema na Wayahudi wa Kiyunani, wakihubiri habari njema za Bwana Yesu. Mkono wa Bwana ukawa pamoja nao; watu wengi wakaamini, wakamwelekea Bwana"*** **Mdo 11:19-21.** Kwa sababu ya upenyo kwa nyumba ya Kornelio watu wa mataifa waliokolewa sasa kanisani, pamoja na Wayahudi.

Kanisa la Antiokia

Waliitwa kwanza wakristo

Kama matokeo, kanisa la Antiokia lilikuwa na Wayahudi na Wayunani. Haya yalikuwa ni mabadiliko makubwa kutoka kwa kanisa mama katika Yerusalemu ambapo wakristo walijulikana kama kitengo cha Wayahudi. Sasa katika Antiokia sasa kanisa limewakilisha mwili wa Kristo [likiwa na wayahudi na watu wa mataifa **Waefeso 3:6**] na kwa mara ya kwanza wakaitwa wakristo (**Mdo 11:26**). Sasa kanisa lilielezwa vizuri kama kikundi kilicho tofauti na Wayahudi.

Neema kubwa kanisani

Biblia inasema ya kwamba neema ya Mungu iliweza kuonekana ikifanya kazi kwa waumini katika Antiokia **(Mdo 11:23).** Kitu spesheli kilikuwa kikifanyika Antiokia! Kitu kipya na tofauti sana kilikuwa kikifanyika tofauti na kile kilikuwa kimefanyika Yerusalemu. Tofauti kubwa ilikuwa ni kuunganika kwa Wayahudi waumini na waumini wa mataifa katika kanisa moja na mwanzo palikuwa hapana shinda kwa sababu neema ya Mungu ilikuwa ikionekana. **Waefeso 2:14-16** inatuambia Yesu aliumba **"*mtu mmoja mpya kutoka kwa wawili";*** kwa

sababu ya msalaba hakuna tena migawanyiko kati ya wayahudi na watu wa mataifa katika kanisa la Kristo.

Kanisa la kitume

Kwa haraka kanisa la Antiokia lilifanyika kuwa kanisa mama, hivyo ni kanisa la kutuma, hivyo ni kanisa la kitume. Katika rekodi ya kitabu cha Matendo ya kwamba kanisa hili lilichukuwa nafasi ya kanisa la Yerusalemu kwa wakati kama kanisa la kitume ambapo mitume walitumwa na makanisa mapya yakapandwa na yakainuliwa.

Matatizo katika kanisa la Antiokia

Hata hivyo, hata katika Antiokia matatizo ya sheria na tohara yaliinuka. Kulikuwa na uaminifu uliochanganyika, kwa nguvu sana, ya kwamba hata Barnaba ***"alikuwa na unafiki",*** akigeuka kutoka kwa uhuru ambao alikuwa ameupata katika Kristo akikataa kukula na watu wa mataifa **(Wagalatia 2:13)**. Paul alikabiliana na shinda hii kwa kiwango cha juu, wa wazi akimkosoa mtume Petro. Kwa bahati baya, baada ya shinda hii kuongezeka inaonekana Paulo hakuona kanisa hili la Antiokia likiwa nzuri kama kanisa mama na ila tu kwa kutembea katika safari yake kule Yerusalemu Paulo hakurudi hapo tena.

Kanisa la Efeso

Wakati Paul alipokuja Efeso katika **Matendo 19**, alikuwa na ujuzi wa kuhubiri injili na kupanda makanisa. Ushuhuda wa paul katika Efeso unaonekana sana, tunaona kwamba kanisa katika Efeso ndilo linanenwa sana katika biblia. **Matendo 19** yote imetolewa kwa kupanda kanisa na kuliinua kanisa la Efeso. **Mdo 20:17-38** inanakili mashauri ya Paulo kwa wazee kutoka Efeso. Kitabu cha **Waefeso [sura 6]** inabeba ufunuo mkubwa kuhusu kanisa katika biblia yote. Kanisa la Efeso lilikuwa moja yapo ya makanisa ambalo Yesu aliandika katika **Ufunuo 2.** Pengine Timotheo alikuwa Efeso kama mtume wakati Paulo alimuandikia barua.

Historia inatuambia kwamba kanisa la Efeso lilifanyika kanisa mama na kituo cha mitume cha huduma zilizoongoza kwa miongo mingi baada ya Agano Jipya kuandikwa. Inaaminika kwamba mtume Yohana alikuwa pale; kwamba Mariamu mama yake Yesu aliishi siku zake za mwisho pale. Mengi ya ufunuo wa kanisa ni nani na ni nini inatoka katika kitabu cha Efeso. Kuna ufunuo unaofunguka wa kanisa katika kitabu hiki na baraka zilizo zetu kupitia Kristo kama kanisa. Katika Waefeso Paulo anaweka kutembea kwa kanisa katika ukomavu.

Kubarikiwa na baraka zote za rohoni.

Waefeso sura ya kwanza inatuambia kuhusu baraka za rohoni ambazo tumepokea ndani ya Kristo. Ziko baraka saba ambazo zimeorodheshwa:

- **Aya ya 4** kuchaguliwa ndani ya Kristo kabla ya msingi wa ulimwengu tuwe watakatifu bila lawama;
- **Aya ya 5** tumewekewa hatima ya kufanyika wana;
- **Aya ya 6** kukubalika ndani ya Mpendwa;
- **Aya ya 7** ukombozi kupitia damu yake, msamaha wa dhambi;
- **Aya ya 8-9** kudumu katika maarifa na ufahamu kujua siri ya mapenzi yake, ***"Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia, Naam katika Yeye Huyo" aya 10.***
- **Aya ya 11** tumeupokea urithi;
- **Aya ya 13** tumewekwa muhuri na Roho wake wa ahadi, ambaye ndiye arabuni ya urithi wetu.

Tunahitaji roho wa hekima na ufunuo

Kutoka **aya 15-19** Paul anatuombea tupate ***"roho ya hekima na ufunuo katika kumjua yeye [Yesu Kristo]; macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uwezo wake".*** Hebu niwaambie: ukiomba ombi hili mara kwa mara na bidii Mungu atakufunulia maarifa ya siri. Paul anaanza kuifungua siri kwa kutuombea ombi hili katika sura ya kwanza.

Miaka mingi katika sehemu ya maombi na kufunga, kutafuta maarifa ya mapenzi ya Mungu na ujumbe wa kanisa leo, mimi binafsi niliomba ombi hili juu ya maisha yangu zaidi ya mara moja. Matokeo yamekuwa ya kushangaza! Nimepata Mungu akijibu ombi hili kwa njia mingi za ajabu katika hali ya ufunuo wa neno lake. Roho wa maarifa na ufunuo anapatikana kwa kila mtakatifu.

Mahali kristo na kanisa lake wamewekwa

Sehemu ya mwisho ya sura ya kwanza inafunua mahali ***"Kristo ameinuliwa juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, … akavitia vitu vyote chini ya miguu yake,"*** na inaonyesha kuwa kanisa ni mwili wake; ya kuwa kanisa ni ***"ukamilifu wake yeye anayekamilika kwa vyote katika vyote".*** Paul anaiweka wazi ya kwamba ***"tumeinuliwa pamoja naye, na kuketishwa pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu"*** **Waefeso 1:20-23** na **2:6.** Ufunuo wa siri umeanza!

Mtu mpya ameumbika

2Wakorintho 5:17 inasema ya kwamba sisi ni viumbe vipya katika Kristo; katika **Waefeso 2:10** Paulo anasema ***"maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu tutende matendo mema". "Tumekuwa karibu kwa damu yake Kristo"*** **aya 13**; na Mungu amefanya ***"hao wawili kuwa mtu mmoja mpya"*** **aya 15** kupitia Yesu Kristo, hakuna uadui tena kati ya wayahudi na watu wa mataifa katika kanisa la kweli la Yesu Kristo. Kuna ufunuo wa kanisa katika aya hizi: sisi ni viumbe vipya, kazi yake, tumeletwa karibu kwa damu ya yesu kama mtu mmoja aliyeunganika.

"Nitalijenga kanisa langu"- Mathayo 16:18

Misingi ya biblia

Kanisa ni nyumba ya Mungu na imejengwa katika msingi wa mitume na manabii **(Waefeso 2:20)** Hakuna msingi mwingine ambao kanisa litajengwa juu yake ila huduma ya mitume na manabii ambao Mungu amepatiana kupitia Kristo kanisani kwa kujenga kanisa. Kwa miaka 1800 kanisa kwa jumla halijakuwa na msingi wa biblia. Mapema baada ya kufungwa kwa nyakati za kuandikwa kwa agano jipya, kanisa lilianza kubadilisha mitume na ofisi iliyowekwa na mtu ya askofu. Askofu aliinuliwa kulitawala kanisa la mji kinyume na mafundisho wazi ya kibiblia ambayo inasema kwamba kanisa la mji linachungwa na kuangaliwa na wazee. Wazee hawa waliwekwa wakfu na mitume. Huu ndio muundo wa biblia **(Mdo 14:23, Mdo 20:28** na **Tito 1:5).**

Kurejeshwa kwa misingi iliyo sawa

Katika maandiko, wazee na maaskofu ni ofisi moja ama huduma. Hakuna hali katika maandiko ambapo mzee moja alipewa utawala juu ya kanisa ya mji, ila wazee walitajwa kwa wingi. Sasa katika siku za mwisho, Mungu anarejesha mitume na manabii ili kanisa la siku za

mwisho lijengwe katika msingi ulio bora. Yesu anakuja kwa kanisa lake, ambalo limejengwa kwa njia yake, sio kongamano ambalo mwanadamu amelichanganya na sasa anajaribu kulileta pamoja bila kufikiri muundo wa kimaandiko uliofunuliwa.

Jiwe la pembeni

Maandiko yanasema Yesu Kristo ndiye jiwe la pembeni. Jiwe la pembeni katika mjengo linawekwa baada ya msingi kuwekwa. Mara tu jiwe la pembeni limewekwa hapo kuta za mjengo zinaweza kuwekwa. Katika maandiko kuna kanisa moja tu na kanisa hili linajengwa juu ya mitume na manabii ambao sio wa kidini ambao wamechaguliwa kanisani na Mungu mwenyewe **(1Wakorintho 12:28).** Kanisa ambalo limeinuka kihistoria halijajengwa katika msingi wa mitume na manabii na kwa hivyo tumekuwa na migawanyiko ya kidini katika kanisa kwa maana watu wamefuata viongozi na utamaduni wa watu. Kanisa la Yesu Kristo sio kuja pamoja kwa migawanyiko ya kidini lakini ni kanisa lililorekebishwa kulingana na maandiko.

Mara misingi ya kibiblia inaporejeshwa na Yesu kutambuliwa na kupokelewa tena kama jiwe la pembeni, **"*jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho*" Waefeso 2:21-22.**

Ufunuo wa siri

Vitu vyote kukusanywa pamoja ndani ya Kristo

Mungu atatupa **"*hekima na ufunuo katika kumjua yeye"* Waefeso 1:17**. Siri hii inafanya kazi katika kuvikusanya vitu vyote ndani ya Kristo, vitu vilivyo mbinguni na duniani **(Waefeso 1:10).** Hii inazungumzia kuja kwa Kristo katika **1 Wathesalonike 4:13-18,** wakati Mungu ataleta pamoja na Yesu wale waliolala, hivyo ni, waliokufa katika Kristo **(aya 14).** Wakati Bwana atashuka kutoka mbinguni "***wafu katika Kristo watafufuka kwanza***" **aya 16**. ***"kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani,"* aya 17.** Huku ndiko kukusanya pamoja kwa vitu vyote katika Kristo itakayoelekeza majira mapya katika Kristo kutawala na kutamalaki kupitia watakatifu wake.

Kufunuliwa na Roho

Ufunuo wa siri ni ***"kufunuliwa na Roho kwa mitume wake watakatifu na manabii"* Waefeso 3:5,** ili sasa **"*Utajiri wake Kristo usiopimika"*** unaweza kuhubiriwa" **(Waefeso 3:8**), ikielekeza ***"ufunuo wa hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho"* Waefeso 3:10**. Lengo la Mungu ni kubadilisha mamlaka na nguvu katika ulimwengu wa roho na kuweka kanisa lake. Kanisa linafahamu siri kwa sababu utajiri wa Kristo usiopimika zinahubiriwa na mitume na manabii ambao Mungu ameweka, zikiwezesha watakatifu kutembea katika maarifa ya siri.

Ufunuo wa kanisa la kweli

Ni wakati kanisa linapofikia kujua ufunuo wa maarifa ya siri ya mapenzi ya Mungu ikifanya kazi kupitia kanisa ulimwenguni ambapo utukufu wa Mungu utafunuliwa. Ufunuo huu ni ufunuo wa kanisa la kweli kama ulivyofunuliwa na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu hutoa ufunuo kwanza kwa mitume na manabii ambao kisha kupitia "***habari za uwakili wa neema"* Waefeso 3:2,** huhubiri utajiri wa Kristo usiopimika, ikiwezesha watakatifu "***kuwaangazia watu wote wajue habari ya madaraka ya siri hiyo"* aya 9.** Kuna mengi ambayo watakatifu wanapaswa kuingia ndani yake; Mungu anataka kujulisha "***utajiri wa utukufu wa siri katika***

watakatifu" **Waefeso 1:18.** Hata sasa watakatifu wengi hawajasikia kuhubiriwa kwa Kristo kwa njia ambayo inafunua siri.

Ufahamu wa siri ulifichwa

Siri hiyo "***ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu"*** **Waefeso 3:9**. Wakati Mungu aliviumba vitu vyote kupitia Yesu Kristo, siri hii, ambayo inaitwa ***"hekima iliyofichwa"*** **1Wakorintho 2:7**, ilikuwapo wakati wa kuuba lakini haikujulikana wala kueleweka. Paulo anasema katika **1 Wakorintho 2:6** kwamba siri hii haijulikani na watawala wa mapepo ya wakati huu lakini inastahili kueleweka na watakatifu ambao wamefikia kiwango cha ukomavu katika ufahamu wao wa ukristo, wakijua nia ya Kristo **(1 Wakorintho 2:16).** Kote katika historia, mwanadamu katika ustaarabu wake na jamii za makabira wametafuta maarifa haya nje ya Kristo. Hekima hii ya ndani inaweza kujulikana tu kupitia injili, ikifunuliwa na Roho Mtakatifu.

Kuhamisha nguvu za mapepo

Kanisa linapofikia katika ufunuo wa ufahamu wa Kristo ni nani na ya kwamba kanisa ni "***mwili wake yeye anayevijaza vyote katika yote",*** kisha ufunuo huu utajulikana na utawala wa mapepo kupitia kanisa **(Waefeso 3:10).** Mabadiliko makubwa yametendeka kanisani kwa sababu Yesu alikufa msalabani. Tunda la kifo chake na kufufuka kwake ni kuubwa kwa mwili wake, kanisa. Kanisa lake linapounganishwa na Kristo aliye kichwa kisha hekima ya Mungu ya namna nyingi, ikieleweka kwa kanisa kupitia kuhubiriwa neno la Mungu kiunabii inajaza himaya ya mbinguni ikiondoa uongozi na utawala wa nguvu za mapepo. Nguvu hizi kwa wakati huu zinatawala kupitia udanganyifu na dini za uongo. Wakati kanisa linakuja kujua ufunuo wa siri, falme za mapepo zinajitiisha katika ufalme wa Kristo.

Ufunuo wa siri unaachilia utukufu

Hekima hii si ya watoto wachanga- watoto wachanga wanahitaji ***'maziwa ya neno';*** hekima hii si ya watoto- watoto wanahitaji '***nyama ya neno';*** hekima hii ni ***'manna iliyofichwa'*** kwa wale ambao wanakua katika ukomavu. Paul anasema ***"Mungu aliazimu hekima hii kabla ya wakati kwa utukufu wetu***" na sasa Roho anafunua hekima hii kwetu **(1 Wakorintho 2:10).** Hekima hii haijulikani na akili za mwanadamu; ni kwa njia ya ufunuo kwa mtu wa rohoni. Kuhakikisha ya kuwa watakatifu wake wanaelewa ufunuo huu wa mapenzi yake, Mungu kwa hakika ametupatia ***"nia ya kristo"*** **1 Wakorintho 2:16**. Hii inamaanisha watakatifu ambao wamefikia ukomavu na wale vijana katika Kristo wanaweza kulielewa neno la Mungu, wanaweza kufikiri mawazo ya Mungu. Mungu daima anafanya kazi kulitimiza ***"kusudi lake la milele";*** tayari amelitimiliza kusudi lake la milele ***"katika Kristo Yesu Bwana wetu"*** **Waefeso 3:11**, na sasa ni kupitia kanisa ambapo utendakazi wa Mungu wa kusudi lake la milele utaonekana.

Ni wakati wa kufahamu siri

Kimaajabu, Mungu ameaminia ufunuo wa siri la kusudi lake la milele katika upumbavu wa kuhubiri injili. Katika siku za mwisho Mungu tena anaachilia neema yake kwa mitume na manabii ili wajulishe ufunuo wa siri hii. Ilikuwa ni Paulo mtume ambaye Yesu alichagua kufungua ukweli mwingi wa ndani wa siri kwa kanisa lake. Hata leo, wahuduma wengi ambao wamepewa karama wanapinga kile ambacho Mungu anafanya. Wengi wanakataa wakijua kuwapokea mitume ambao Bwana anainua katika siku hizi. Wengi wanalinda taasisi za kikristo kwa njia isiyotakikana kinyume cha amri na mafundisho ya maandiko. Katika siku zake Paul aliwaita wahubiri kama hao Judaizers/ wa dini ya kiyahudi. Walikuwa wakijaribu kufunga kanisa

jipya la kikristo katika taasisi na tabia za uyahudi. Waalimu wa dini wa miaka mingi ambao wanawasikia wanapitwa na ufunuo wa siri ambayo ni ya muhimu kwa sababu ya kutukuzwa kwa kanisa. Watu kama hao hawana maono ya kanisa ila tu kwa kile wanachokijua.

Kuna MOJA …

"Mwili mmoja na Roho mmoja,
Kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu;
Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja;
Mungu mmoja; naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote
***na ndani ya yote"* Waefeso 4:4-6.**

Kunukuliwa huku katika maandiko kunastahili kufanyika jambo la kuzingatia sana la kila muumini na kila ushirika wa kikristo katika taifa mpaka wakristo waamini ujumbe wa neno la Mungu, kwamba kuna kanisa moja tu.

Umoja wa imani

Alama ya kwanza ya kanisa lililokomaa kulingana na **Waefeso 4:11-16** ni ***"umoja wa imani"* aya 13.** Umoja huu wa imani wazi unazungumza habari ya nia yetu katika biblia. Kama tuna ufunuo ya kwamba biblia ni neno la Mungu na kwa uaminifu tunahubiri Yesu, aliye Masihi, kutoka kwa neno, mafundisho ya imani ya neno yatafundishwa kwa kila muumini, sio hitikadi au ukweli wa juu juu wa vikundi vya dini kanisani. Umoja wa imani hauji kwa wale ambao wanakubaliana na neno la Mungu, wakitilia maanani mafundisho ya kanisa na tabia ambazo sio za kimaandiko. Mageuzi ya karne ya kumi na sita yalionyesha kwamba 'Maandiko ndio tu mamlaka yetu katika imani na utendaji'. Kwa bahati baya, ni kwamba hawakuzingatia hata walioyatangaza. Hata hivyo, kukiri kwa imani katika neno la Mungu na utiifu kwa neno la Mungu ni ya msingi na ya muhimu kwa mageuzi ya kanisa siku ya leo.

Lengo la Mungu ni kanisa lililotimilika

Mungu anawapenda watu wake wote milele na kulingana na neema yake, rehema na hekima, ameinua viongozi na miondoko kote kote katika historia kuleta toba (mabadiliko), ikiburudisha, maisha mabichi na mwelekeo na ufifio wa watu wake. Lakini sasa tunaishi katika siku za mwisho ambapo Bwana peke yake "***anatakasa na kulisafisha kanisa kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu"* Waefeso 5:26-27**. Hakuna nafasi ya wahuduma washoga katika kanisa la Kriso. Lengo la Mungu ni kanisa kamilifu na Yesu mwenyewe baada "***ya kushuka na kupaa akawapa wanadamu vipawa"* Waefeso 4:8-10*. "Naye alitoa wengine kuwa mitume … kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu … hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani … na kuwa mtu mkamilifu"* Waefeso 4:11-16.**

Mitume wanahitajika ili kulifikia lengo

Wengine wanasema '*hatuhitaji mitume', 'hakuna mitume wengine tangu kanisa la kwanza'* na mambo kama hayo. Hata hivyo biblia inasema kwa wazi tunahitaji mitume leo:

- ***"kukamilisha watakatifu"* waefeso 4:12;**
- ili kanisa lipate *"**kujengwa katika misingi ya mitume"* … Waefeso 2:20;**
- kuleta ***"ufunuo wa siri"* Waefeso 3:5;**
- kuwa uongozi / uelekezi wa kanisa **1 Wakorintho 12;28.**

Katika biblia uongozi wa kanisa kwa jumla uko mikononi mwa mitume na katika mahali pamoja uko mikononi mwa wazee ambao wamewekwa wakfu na mitume. Na huu ni muundo wazi katika maandiko. Kama ilivyokuwako mwanzo, ndivyo itakavyokuwa.

Siri ya karama ya huduma tano

Ujumbe wa msalaba

Ujumbe wa kawaida wa msalaba ambao tumesikia na tumehubiri vyema ni kwamba Kristo "***alitolewa kwa ajili ya makosa yetu; na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki"*** **Warumi 4:25.** Katika kuhubiri injili ili tuokoe nafsi Paulo anasema, ***"maana niliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa"*** **1 Wakorintho 2:2.** Hii ni siri kubwa: Kupitia kufa na kufufuka kwa Yesu, tunaweza kuokolewa milele.

Kristo aliyepaa alipatiana karama za huduma

Paulo pia anatufundisha kupitia kifo cha Yesu – aliteremka hata maeneo ya chini ya dunia – na kupitia kupaa kwake **(Waefeso 4: 9-10).** Alipatiana kanisani karama ya huduma tano ya mtume, nabii, mwinjilisti, mchungaji na mwalimu **(aya 11).** Huduma hizi ni za muhimu sana katika kuinua ***"mtu mkamilifu"*** **Wefeso 4:13**, ikiongea kuhusu kanisa likikua na kufikia utimilifu. Yesu hakufa tu msalabani kwa sababu ya wokovu wetu kutoka dhambini na kuzimu na kifo, lakini alikufa kwa sababu ya kutukuzwa kwetu **(Warumi 8:29-30).**

Kanisa litafikia utukufu tu wakati huduma zote zinafanya kazi. Huduma hizi lazima zifanye kazi "***Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata mwili wa Kristo ujengwe"*** **Waefeso 4:12,** mpaka kanisa litakapokamilishwa pamoja. Katika **1Wakorintho 2:6-8,** Paulo anafundisha ***"ambayo wenye kuitawala dunia hii, wasingemsulibisha Bwana wa utukufu"*** kama wangelikuwa na ufahamu wa siri. Sehemu ya siri ambayo utawala wa mapepo hawakuifahamu wala kwa bahati baya waumini wengi leo, ni kwamba Yesu alirudisha kwa njia ya siri karama ya huduma tano kwa kushuka kuzimu na kuwateka mateka. Hapa kuna siri.

Yesu Kristo alipatiana kila kitu kwa kanisa Lake.

Yesu Kristo, mwana wa Mungu, alipitia kunyenyekeshwa kwa kufanyika mwanadamu, *"**bali alijifanya hana utukufu",*** na akapitia kifo, ***"hata kifo cha msalaba"*** **(Wafilipi 2:7-8**) ili ajiletee kanisa. Yeye ni mwokozi wa mwili **(Waefeso 5:23).** Kupitia kushuka na kupaa kwake, Yesu alijichukulia ushindi wa ajabu ambao ulibadilisha historia milele na kama matokeo ya kazi yake ya ukombozi alipata kulipatia kanisa lake karama ya huduma tano.

Bila karama hizi kanisa halingeletwa katika ukomavu na utimilivu. Kusudi la karama ya huduma tano ni ya namna nyingi katika mwili uliokomaa ndani ya Kristo, "***katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo"*** **Waefeso 4:16**.

Huu ni mwili uliokomaa ambao Bwana analeta hapa duniani
na anatenda haya kwa kuachilia karama
ya mtume, nabii, mwinjilisti, mchungaji na mwalimu.

Sura ya tatu (b)

SIRI YA KANISA – Sehemu ya Pili

NEEMA YA KUKUA HADI UKOMAVU, WAEFESO 4:7-16

Lengo ni ukomavu [utimilifu]

Lengo la Mungu kwa kanisa la Yesu Kristo ni kanisa likue katika ukomavu na pia likamilishwe. Kutakuwa na kanisa tukufu bila ila wala kunyanzi wala kitu kinachofanana na hayo chafaa kushirikiana milele kwa Mwana wa Mungu! **Waefeso 4:7-16** ndipo tu mahali ambapo huduma tano zimeelezwa vyema. Ni katika mazingira haya ambapo tunapata ya kwamba neema imepatianwa kwa kila mshiriki wa mwili wa Kristo kupitia huduma ya, mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu kuwezesha kila mshiriki na hivyo mwili kukua hata ukomavu.

Kupitia kila huduma ya hizi neema inaachiliwa kwa mwili wa Kristo. Kama moja yapo ya karama hii haiachiliwi na haifanyi kazi basi mwili wa Kristo haupokei neema yote ambayo inatakiwa ili uje katika ukomavu.

Yesu Kristo ndiye huduma tano

Yesu mwenyewe ndiye utimilifu kamili wa karama ya huduma tano:

- **Mtume wa Mungu,** alitumwa duniani kujenga kanisa [nyumba ya Mungu] **(Waebrania 3:1);**
- **Nabii** aliyeinuliwa na Mungu kutoka kwa ndugu zake **(Kumbukumbu la torati 18:18)** kuzungumza maneno ya Mungu, **(Luka 24:19);**
- **Mwinjilisti** ambaye alikuja kutafuta na kuokoa kilichopotea **(Luka 19:10, Mariko 1:14);**
- **Mchungaji,** mchungaji mwema aliyetoa uhai wake kwa sababu ya kondoo, **(Yohana 10:11, Waebrania 13:20);**
- **Mwalimu** aliyetoka kwa Mungu, aliyefundisha kama mwenye mamlaka, **(Yohana 13: 13-14, Yohana 3:2).**

Kusudi la Mungu la milele

Katika kitabu cha Waefeso na kwingineko Paulo anaongea kuhusu siri ambayo imefunuliwa na anazungumzia kusudi la Mungu la milele ambalo alitimiza katika Kristo Yesu Bwana wetu. Tunastahili kuelewa ya kwamba Mungu anashugulikia kusudi lake la milele. Hajayumba yumba katika kusudi lake ambalo aliiumbia ulimwengu na ambayo alituumba kwa mfano na sura yake. Yaliyopotea katika Adam wa kwanza kupitia dhambi imepatikana na Bwana wetu Yesu Kristo, na zaidi sana. Inawezekana kuona karama hii ambayo ilikuwa ndani ya adam wa kwanza lakini ikachukuliwa mateka kupitia dhambi za Adam na kujipatiana kwa shetani. Mungu amekuwa amekusudia kanisa lenye utukufu liumbwe na liinuliwe hapa duniani kwa mwana wake. Mungu alikuwa wakati wote amepatiana msaada kwa uwezekano huu lakini ilibidi kifo cha Yesu na kushuka kwake kuzimu na kupaa kwake kwenye utukufu ili kikamilifu aachilie njia ambayo kusudi linaweza kutekelezwa.

Yesu analijenga kanisa lake kupitia huduma tano.

Yesu Kristo ndiye jiwe la pembeni la kanisa ambayo imewakilishwa kama jengo. Yeye ndiye jiwe la msingi, lililojaribiwa, jiwe la pembeni la dhamani, msingi imara **(Isaiah 28:16).** Sisi ni mawe yaliyo hai ambayo yanajengwa juu yake kujenga kuta za hekalu ya Mungu katika Roho **(1 Petro 2:5** na **Waefeso 2:22).** Yesu alipatiana huduma za mtume, nabii, mwinjilisti, mchungaji na mwalimu kuwezesha kazi yake ya kujenga iendelee na kwa kusudi la Mungu la milele kutimizwa.

Huduma tano zinaleta mwili katika utimilifu.

Makusudi matatu ya huduma tano

"Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe" **(Waefeso 4:12).**

1. Kwa kuwakamilisha watakatifu.

Huduma tano zimepatianwa kwa kuwakamilisha watakatifu.

> **Kukamilisha**, *katartismos* (kat-ar-tis-moss); S.C.# 2677. **Kiyunani***: kulainisha, kuandaa, kutayarisha, kukamilisha, kusababisha ifae kikamilifu kwa sababu ya huduma*. Katika kiyunani kilicho sawa neno linatumika kuweka mifupa sawa wakati wa upasuaji [SFLB Word Wealth P1651). Ufahamu wa neno hili unatufundisha ya kwamba mwili wa Kristo ni lazima uwekwe katika mpangilio ili kila sehemu ifanye kazi vizuri.

Mungu anakusudia kila mshiriki wa mwili wa Yesu Kristo aandaliwe ili afanye kazi katika karama na huduma ambazo Mungu amepatia kila mmoja. Kwa hakika sio kila mmoja amewekewa hatma kuwa mhuduma wa huduma tano lakini kila mtu ako na kazi ya kutimiza. Mpaka kila mtakatifu ameandaliwa kuhudumu mwili wa Kristo hautafikia ukomavu.

2. Kwa kazi ya huduma

Huduma tano zimepatianwa kwa kazi ya huduma: kila huduma katika huduma tano lazima ifanye kazi. Sehemu kubwa ya kanisa hawapokei neema ambayo imepeanwa na Yesu aliye kichwa cha kanisa kwa sababu mitume na mara kwa mara huduma tano hawajapokelewa. Kama nimeitwa kuwa mtume lakini ninafanya kazi kama mchungaji wa mahali pamoja sifanyi kazi ya huduma ambayo nimeitiwa. Moja wapo wa urejesho ambao unatendeka miongoni mwa mwili wa Kristo duniani kote ni kwamba watakatifu wameachiliwa katika huduma kwa sababu Yesu anainua mitume akiwatuma kufanya kazi ya huduma.

Watu ambao wanafanya kazi katika huduma kwa ujasiri wanaingia katika huduma tano kama vile Roho Mtakatifu anawaita nakutenga watu fulani kwa huduma hizi. Hii imeonyeshwa katika maisha ya mtume Paulo ambaye hakuwa amewekwa wakfu kuwa mtume mpaka **Mdo 13** lakini alikuwa akifanya kazi katika huduma kabla ya wakati huo. Hata hivyo wengi katika huduma leo watajua mabandiliko na wataanza kuhudumu katika karama zingine. Kwa wakati huu wengi wanafanya kazi katika uchungaji kama wazee ambao wameitwa katika huduma ya mtume na nabii katika mwili wa Kristo.

3. Kwa kujenga mwili wa Kristo

Huduma tano zimepatianwa kwa kujenga mwili wa Kristo, hivyo ni, kuujenga mwili. Yesu aliahidi katika **Mathayo 16:18** ya kwamba analijenga kanisa. Analijenga kanisa namna gani? Analijenga kupitia karama ya huduma tano ambayo amepatiana. Ndiposa urejesho wa

huduma tano ni wa muhimu sana katika kulitimiza kusudi la Mungu. Kanisa tukufu ambalo linafikia ukomavu halitajengwa bila karama ya huduma tano kurejeshwa kikamilifu na kufanya kazi. Karama ya mtume inahitaji kurejeshwa ili huduma hizo zingine zifanye kazi katika utimilifu.

ISHARA ZA UKOMAVU

"Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo" **Waefeso 4:13.**

1) Umoja wa imani

Kipimo cha kwanza cha ukomavu ni umoja wa imani. Hii inamaanisha kukubaliana kuhusu neno la Mungu. Makubaliano kama hayo yana msingi katika kupokea mafundisho ya kitume, sio kufuata mafundisho ya watu ama tamaduni zote za kanisa. Kanisa la kwanza lilijitoa kwa fundisho la mitume **(Mdo 2:42).** Petro anatuambia "***hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu"*** **1 Petro1:20.** Kwa bahati baya kanisa kihistoria imegawanyika katika msingi wa mafundisho ya viongozi na mara kwa mara mafundisho haya yanafundishwa badala ya maandiko. Msisitizo umekuwa kile ambacho huyo mtu alisema badala ya vile maandiko yanasema.

Umoja wa imani ni kushika sana neno la uaminifu ambalo limefundishwa; ni kushika mafundisho ya kweli katika imani na matendo "***akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwenye mafundisho ya uzima, na kuwashinda wenye kupinga"*** **Tito 1:9**. Umoja wa imani ni kuwa na fundisho la kweli, hivyo ni, kuamini na kuishi kwa neno la Mungu. Umoja wa imani ni imani hio [fundisho la mitume] ***"imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu"*** **(Yuda 3).** Mtume Yuda anatuhimiza tuishindanie imani: fundisho lililopeanwa na neno la Mungu kupitia mitume.

Kanisa la kwanza lilijipatiana katika fundisho la mitume.
Kanisa la siku za mwisho litafikia ukomavu tu katika imani
kama mara tena fundisho la mitume litafundishwa na kupokelewa.
Ni kupitia neno la Mungu tu ambapo tutaamua kama
fundisho fulani ni la Bwana ama hasha.

2) Kumfahamu sana Mwana wa Mungu

Twatakiwa tufike katika 'kumfahamu sana Mwana wa Mungu', tukielewa marejeo yote ya Mwana katika Waebrania sura ya kwanza. Tunatakiwa kufika kwa maarifa ya siri ya Utaua katika **1 Timotheo 3:16.** Kumfahamu sana Mwana wa Mungu ni kufahamu ya kwamba Mungu alidhihirishwa katika mwili, ya kwamba Mungu alifanyika mwanadamu katika Yesu Kristo **(Yohana 1:1 & 14).** Yesu alionyesha uhusiano wake na Baba katika injili ya Yohana, mwisho akitangaza kwa Filipo ***"aliyeniona Mimi amemwona Baba"*** **(Yohana 14:9).**

3) Hata kuwa mtu mkamilifu

Mwili wa Kristo ni lazima upate kuwa mtu mkamilifu, aliyefananishwa na Mwana wa Mungu **(Warumi 8:29)** na kulijua neno la haki **(Waebrania 5:13).** Tunastahili kuyainua macho yetu kumtazama Yesu, mwenye kuanzisha na kuitimiza imani yetu (**Wabrania 12:2),** na

"nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu" **Wafilipi 3:14.**

4) Cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo

Tunatakiwa kuwa kama Kristo, Yeye aliyepakwa, Mwana wa Mungu, "***ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi"*** **Warumi 8:29.** Kanisa ni ukamilifu wake yeye anayekamilika kwa vyote katika yote **(Waefeso 1:23).** Utukufu wa Bwana ndio utimilifu wa Kristo anapolijaza kanisa lake.

5) Sio tena kama watoto …

"Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za undanganyifu" **Waefeso 4:14.** Ni wakati wa kukua, kuishi kwa upako ambao tumepokea. Upako utatufundisha mambo yote na hautatundanganya **(1Yohana 2:20, 27).** Yesu alisema katika **Mathayo 24:5** "***kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema mimi ni Kristo; nao watandanganya wengi".*** Jilinde na walimu wa uongo; wengi watakuja na vazi la huduma ya kikristo! Tunatakiwa kuwa tumeimarika na kuwa na mizizi katika imani, tusipotoshwe na Filosofia na undanganyifu **(Wakolosai 2:6-8).** Tunastahili kuwa tumeimarishwa kwa nguvu juu ya mwamba na katika neno la Mungu. **Mathayo 7:24-27** inatufundisha nini? Tunapaswa kumtazamia Yesu, sio mwanadamu yeyote, na kulitii neno lake.

6) Kuishika kweli katika upendo

"***Lakini tuishike kweli katika upendo"*** **Waefeso 4:15a.** Wanafunzi wanaokua katika ukomavu hawajihusishi na uvumi ama masengenyo; hawasemangi, ila wanashika ukweli katika upendo! Kanisa linalokua ni mwili wa watu wanaokua katika uhusiano. Ili uhusiano ukue katika njia ya kiungu na upendo wa kikristo wa kweli, ukweli unatakiwa kunenwa katika upendo kwa moja hadi mwingine. Hakuna nafasi ya kukosoana kwa moja na mwingine. Kama tatizo likitokea miongoni mwa wandugu na lishugulikiwe kulingana na mwelekeo wa maandiko, upendo hustiri wingi wa dahambi **(1Petro 4:8).**

7) Kukua katika mambo yote katika Kristo

"*Kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo"* **Efe 4:15b.** Mkristo binafsi na kanisa kwa jumla wanatakiwa kukua. Kila sehemu katika maisha lazima ifikie kiwango cha neno la Mungu wakati kazi ya neema inakamilishwa ndani yetu. Tunatakiwa kupatikana ndani ya Kristo [Aliyepakwa] sio tukiwa na haki yetu wenyewe, bali ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo **(Wafilipi 3:9).** Kila kitu tufanyapo kwa neno ama matendo, twatakiwa kufanya "***yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye"*** **Wakolosai 3:17.**

8) Upendo wa Mungu unafunuliwa katika kanisa ambalo limekomaa

"*Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo"* **Waefeso 4:16.** Hii ni picha ya nguvu ya kanisa ambalo limekomaa; elewa tabia kuu ya kanisa lililokomaa ni UPENDO, aina ya upendo wa Mungu, wenye kujitoa, upendo wa kujipatiana! Kanisa lililokomaa ni komavu kwa kuwa kila kiungo kinafanya kazi vyema, ukiisha kuungamanishwa na kushikanishwa pamoja – umoja wa kweli, kuwa mmoja!

Kila sehemu na kila kiungo [katika mwili kiungo ni mahali ambapo washiriki wawili wanaweza kushirikiana kikamilifu kufanya kazi] inatoa uzima na kila sehemu inafanya kazi kwa kujenga mwili wote. Uzima huu wote unatiririka kutoka kwa kichwa, Bwana wetu Yesu Kristo.

KANISA LINADHIHIRIKA

Sisi ndio nyumba ya Mungu

'Sisi ni nyumba ya Mungu' **(Waebrania 3:6)** na Yesu Kristo ni Mwana katika nyumba yote ya Mungu. "***Atalijenga hekalu ya BWANA"* Zekaria 6:12**. "***Alipopaa, aliteka mateka, akawapa wanadamu vipawa"* Waefeso 4:8. Alipeana vipawa hivi** 'kuujenga mwili wa Kristo' **(Waefeso 4:12).** Kanisa lazima lifikie ukomavu [utimilifu], ili liwe uthihirisho wa utukufu wake duniani, "***ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma"* Yohana 17:22-24*. "Apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa"* Waefeso 5:27.** Mungu ana mawazo ya utukufu ya kanisa: yeye ni mwili wa Kristo.

Kupitia kanisa Mungu anakusudia kufunua Mwanawe. Ili haya yatendeke kutakuwa na urejesho kamili wa huduma ya mitume pamoja na karama za huduma. Haya yanafanyika katika siku zetu na inaharakishwa kwa maana Mungu anakusudia kazi ya haraka itendeke katika siku za mwisho **(Isaya 60:21-22).**

Moja wapo wa sababu kubwa ya utendaji kazi wa mtume na nabii ni kuweka msingi wa kanisa la Yesu **(Waefeso 2:20).** Msingi kama huo unaachilia huduma zingine za mwinjilisti, mchungaji na mwalimu kufanya kazi kikamilifu na hivyo watakatifu kuhudumiwa vyema na kuinuliwa kufanya kazi katika mwili. Mtume anawajibika kwa fundisho [hivyo ni, kufundisha neno la Mungu kwa usahihi] na kwa mikakati ya ujenzi. Paulo anasema yeye alikuwa ni mjenzi mwenye hekima **(1 Wakorintho 3:10).** Mungu huwafunulia mitume jinsi ya kuiweka misingi; wengine wanatakiwa kujenga juu yake. Nabii ana wajibu kando ya mtume na kwa pamoja wanaleta msingi thabiti ndani ya Kristo kwa kuandaa na kutayarisha watakatifu na kuinua huduma zingine. Nyumba ya Mungu itajengwa.

Imeandikwa

"*Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza; na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema"* 2 Timotheo 3:16-17. Mengi ya yale tumerithi kama 'kanisa' sio kulingana na maandiko. Mmoja wa watafsiri wa Biblia anazungumzia kanisa katika kitabu cha Matendo kama 'kanisa changa'. Anapendekeza kwamba kanisa lililoenea katika historia ndilo kanisa mzee hivyo limekomaa na kwa hivyo miundo na tabia ambazo zinaendelea katika historia ya kanisa ni zile za kanisa ambalo limekomaa. Hivi sivyo ilivyo.

Kanisa la Yesu Kristo linapatikana katika utimilifu wote katika
Agano Mpya, kutoka kanisa la kwanza katika Mdo 2
hadi kwa muundo wa kanisa lililokomaa katika kitabu cha Waefeso

Tunapimwa na neno la Mungu

"*Hizi saba* [ikiongea kuhusu Roho Mtakatifu] ***watafurahi, nao wataiona timanzi katika mkono wa Zerubabeli"* Zakaria 4:10.** Zerubabeli ndiye mjenzi wa hekalu; yeye ni mfano wa Mtume – mjenzi wa kanisa. Timanzi inazungumzia chombo cha kupima - neno la Mungu.

Huduma tano za **Waefeso 4:11** lazima zihudumu ***"hata na sisi sote tutakapofikia … kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo".*** Tena, kuna chombo cha kupima! Hapa ni ***"utimilifu wa Kristo",*** lakini hakika ni neno la Mungu**.** Kristo anafunuliwa kuwa Neno la Mungu. Ni wakati tu tutakaporejelea maandiko na kwa bidii kulitii neno la Mungu ambapo ***"tutakuwa wanafunzi wake, tukizaa sana, tukimletea Baba utukufu"*** **Yohana 15:8.**

Kuondoa chachu

Kanisa la kuunganisha la Australia kwa wazi linatangaza katika msingi wake wa maungamo kwamba 'Biblia ina neno la Mungu'. Mkristo wa kiutume anaamini na kujua kwamba Biblia ndilo neno la Mungu! Kwa hivyo, kanisa lakuunganisha limeamua kuhifadhi haki za kuamua ni andiko lipi ni neno la Mungu. Mtazamo kama huo una makosa **[ona 2Timotheo 3:16 na 2Petro 1:19-21**] na imeelekeza kudharauliwa kwa hali ya sasa ambapo wengi wa wasimamizi wa kanisa la muungano la kitaifa, haswa viongozi walichagua mno [julai 2003] katika kukubaliana kusimika wahuduma mashoga na walawiti kwa makundi yao. Kumekuwa na kusimikwa wazi kwa mtu mshoga kuwa askofu wa Episcopalian [Anglican Church] USA. Huyu mtu aliacha mke na watoto afanye ushoga, wakati wote akiwa mshoga. Wandugu, wakati umepita tuamke. Paulo anasema "***Basi, jisafisheni mkatoe ile chachu, kwa maana pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani Kristo"*** **(1 Wakorintho 5:7)**. Hali hii katika Merikani hata ni baya zaidi kuliko ambayo mtume Paulo alikuwa akikabiliana nayo katika kanisa la Korintho.

Toka miongoni mwao.

Bwana anajitayarishia "***Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa"*** **Waefeso 5:27.** Ni wakati wa kuamua kama tunamfuata Yesu na kutamani na mioyo yetu yote kuwa sehemu ya bibi arusi kanisa Lake tukufu.

Bwana Yesu, aliye kichwa cha kanisa, anawaita watu wake watoke! Neno la Mungu liko wazi sana "***Msifungwe nira pamoja na wasioamini"*** **2Wakorintho 6:14.** Wasioamini ni wale watu wasioamini kwamba Biblia ni neno la Mungu. "***Pana urafiki gani kati ya haki na uasi?*** **2 Wakorintho 6:14** ***"Wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu"*** **1Wakorintho 6:9,** kwa maana ufalme wa Mungu ni "***haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu"*** **Warumi 14:17.** Ni wakati wa wakristo kuwa wazi/kweli! Kuona neno la Mungu kama lilivyoandikwa.

Toka miongoni mwao na utenganishwe

Wakristo wa kweli ni ***"hekalu la Mungu aliye hai*** na Mungu anasema ***Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu"*** **2Wakorintho 6:16.** ***"Kwa hivyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha"*** **aya 17.** Mungu anawaambia watu wake kujitenga na kila kilicho kichafu. Utakuwa ni ushuhuda mkubwa sana wakati watu wa Mungu watatoka kutoka kwa mambo yote ya kujichanganya na kukubaliana. Sasa ndio wakati! Usizidishe zaidi. Mungu anatuahidi kwamba tukijitenga kwa ajili yake, kuwa watiifu kwa injili, ***"Atakuwa Baba kwetu, nasi tutakuwa kwake wanawe wa kiume na kike, Asema Bwana Mwenyezi"*** **2Wakorintho 6:18.**

Siri ya Kristo na kanisa Lake

Katika **Waefeso 5:22-33**, Paulo anazungumzia siri kuu; analinganisha uhusiano wa Kristo na kanisa Lake na uhusiano wa mme na mke wake. Anatuonyesha kwamba kuwa mme, Yesu hakufa tu kwa ajili ya kanisa lake lakini sasa kama Bwana harusi aliye fufuka asubiriye,

analiandaa kanisa lake kuwa bibi arusi mwenye utukufu. Maandiko yako wazi: "***Atajiletea kanisa tukufu"* aya 27.** Kila alitazamaye kanisa kama vile imekuwa katika historia ya sasa anaweza kusema, 'hili haliwezekani!'

Kuoshwa kwa maji kupitia neno

Hata hivyo, Paulo anasema kwamba anazungumzia siri! Ambacho hakiwezekani na mwanadamu, kinawezekana na Mungu. Funguo ambazo maandiko yanatupatia ni kwamba Yesu atayatenda haya: Atajiletea kanisa likiwa kamilifu. Yesu atatenda haya kwa njia gani? Tayari Yesu amewahesabia haki wale watu amewaita, na Yesu amewatukuza wale aliwahesabia haki **(Warumi 8:30).** Haya yote yalifanyika kupitia kufa kwake, kufufuka na kupaa.

Sasa "***analitakasa na kulisafisha kanisa kwa maji katika neno"* Waefeso 5:26.** Ni wakati neno linazungumzwa na Yesu katika maisha ya watakatifu, kwa mtu binafsi na kanisa kwa jumla, ambapo mabadiliko yanatekelezwa. Kwa hivyo Bwana anapolihuisha neno lake leo kuhusu kutukuzwa kwa kanisa kupitia kukamilishwa kwa watakatifu, wale watakaolisikia neno lake kwa imani watabadilishwa.

Wale ambao wanajua uhusiano wa kweli na Yesu Kristo, wale ambao hawajafungwa na tamaduni na kujipatiana kwa makanisa ya kitaasisi, wanaweza kusikia neno Lake. Tumewekwa kusikia na kutii neno. Neno lake linatutakasa kutoka kwa mawazo ya kidini ambayo tumepokea kutoka kwa ujuzi tofauti wa 'kanisa'. Kwa wakati huu mojawapo ya mawazo ya kidini ambayo inazuia kanisa kukua, na kuenenda kutoka utukufu hadi utukufu, ni ile hali ya kutowapokea mitume, hata kama huduma ya mitume ndio imefundishwa sana na huduma iliyoonekana katika Agano Jipya.

Kanisa kudhihirika

Kujua uhakika wa kanisa la Yesu Kristo inawezekana tu kupitia ufunuo wa siri. Kanisa ni siri, sio kwa njia ya 'kanisa fumbo', ambayo lilitiliwa maanani na baadhi ya waalimu wa kale, lakini ni kwa wazo la mwili kweli kweli wa watu waliounganika kote kote duniani kupitia uhusiano uliopeanwa na Mungu. Mwili huu umeungwa pamoja ndani ya Kristo na yeye. Yeye ni mwokozi wa mwili – hii inafanya uwe mwili wake na sio wa mwingine - na kama kichwa cha mwili, ni haki yake na wajibu kuinua mwili kufananishwa na mwili wake uzima wake usioharibika.

Hata sasa kanisa limeshindwa kudhihirisha uzima na nguvu za Bwana. Kanisa limetupiliwa na njia zote za udini.

Kanisa ambalo tunasoma katika maandiko litafunua utukufu wa Bwana.

Kanisa linatakiwa kukua liwe mwili wenye utukufu
La watakatifu wenye haki, waliojazwa na Roho, wanaozaa matunda duniani kote,
Wakidhihirisha ufalme, nguvu na utukufu wa Kristo aliyefufuka

Ili ulimwengu upate kujua Yesu Kristo
ni Mwana wa Mungu,
kwamba alikuja kutoka kwa Mungu
na kwamba kifo chake msalabani
kimepata mazao mengi duniani.

Sura ya nne

YESU MTUME WETU

Yesu Mtume, anaijenga nyumba - Waebrania 3:1-6 *"kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu, aliyekuwa mwaminifu kwake yeye aliyemweka, kama Musa naye alivyokuwa, katika nyumba yote ya Mungu, kwa maana huyo amehesabiwa kuwa amestahili utukufu zaidi kuliko Musa, kama vile yeye aitengenezaye nyumba alivyo na heshima zaidi ya hiyo nyumba. Maana kila nyumba imetengenezwa na mtu; ila yeye aliyevitengeneza vitu vyote ni Mungu. Na Musa kweli alikuwa mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu kama mtumishi, awe ushuhuda wa mambo yatakayonenwa baadaye; bali Kristo, kama Mwana, juu ya nyumba ya Mungu; ambaye nyumba yake ni sisi, kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho.*

Yesu alitumwa na Baba – Yohana 20:21"*Basi Yesu akawaambia tena, amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi."*

Yesu anatutuma tufunue utukufu Wake – Yohana 17:18 "*kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni,"* **aya 20-22** *"Wala si hao tu ninao waombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja".*

Katika Septemba 2002 Bwana alinionyesha katika maono ya kwamba upako wa kiutume umeachiliwa kulijenga kanisa lake la siku za mwisho. Yesu anasema wazi katika **Mathayo 16:18** ***"Nitalijenga kanisa langu".*** Kupitia urejesho wa mitume na manabii kwa kanisa kwa wakati huu Yesu ameachilia karama na upako wa kulijenga kanisa lake. Ni kupitia kanisa ambapo utukufu wa BWANA utafunuliwa. ***"Na utukufu wa BWANA utafunuliwa, na wote wenye mwili watauona kwa pamoja; kwa kuwa kinywa cha BWANA kimenena haya"*** **Isaya 40:5.**

Mtafakarini Yesu Mtume

"Kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wetu wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani mkuu wa maungamo yetu, Yesu Kristo" **Waebrania 3:1**. Katika aya hii tumeambiwa tutafakari mambo mawili makuu ya Bwana wetu Yesu Kristo: yeye ndiye Mtume na Kuhani mkuu wa *'maungamo yetu'*. Alifanyika Mtume halisi na Kuhani halisi tunapoelewa na kumkiri kuwa hivyo. Kwa hivyo ni jambo la muhimu sana kuwa na ufamu kamili wa Yesu Mtume, ili tuweze kumkiri.

Kukiri katika KJV SC Kiyunani. #4671*, homologia, kihalisi* ikimaanisha *neno moja; homologia ni hali ya kutambua kuhusu ukweli,* ikitoka kwa *SC # 4670, homologeo, halisi…kuongea jambo moja; kutangaza wazi kukiri kulio na msingi wa ushawishi wa uhakika.*

KUHANI MKUU

Wakristo wengi wanamfurahia Yesu na yale aliyoyafanya kama Kuhani wetu, hivyo ni, sadaka yake iliyo kamili msalabani ambayo imefanya upatanisho wa dhambi mara moja na ya kutosha. Hata hivyo, wakristo wachache wameshawahi kumtafakari Yesu aliye Mtume. Kwanza hebu tutazame tena huduma ya Ukuhani Mkuu.

Alitoa sadaka iliyo kamilifu

Sadaka ya Yesu ya kujitoa msalabani, sadaka kamilifu kwa ajili ya dhambi, ni jambo la kueleza ya huduma ya Kuhani Mkuu, "***Lakini sasa, mara moja tu, katika utimilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake"*** **Waebrania 9:26.** Kufuatia kufufuka na kupaa kwa Bwana Mbinguni ambapo "***kwa damu yake mwenyewe aliingia, mara moja tu katika patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele"*** **Waebrania 9:12,** ndiye utimilizo wa huduma ya Ukuhani mkuu wa Kristo, akishughulikia dhambi kwa kuimwaga damu yake mwenyewe. Yesu alitimiza siku kuu ya upatanisho kwa kufanyika mbuzi ya kuzibeba dhambi na mbuzi ya kutolewa sadaka. **[ona Mambo ya Walawi 16]**

Anafanya maombezi

Yesu **"*maana yu hai siku zote ili awaombee"* Waebrania 7:25,** akiisha kuingia kwenye uwepo mle mlimo ndani ya pasia kama mtangulizi wetu, "***Amekuwa kuhani Mkuu hata milele kwa mfano wa Melkizedeki"*** **Waebrania 6:19-20. [ona pia Warumi 8:34** kuhusu Yesu mwombezi] "***Kwa kuwa hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha rehema kwa ujasiri"*** **Waebrania 4:15-16.** Kama mwombezi Yesu anatuwakilisha katika enzi na kuachilia neema kwetu kutoka kwa Mungu.

Yuko mbinguni

Yuko wapi Yesu kuhani Mkuu? *"**Ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu"*** Waebrania **12:2;** Yeye ni, "***Kuhani mkuu, aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu"*** **Waebrania 4:14*. "Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi, bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili Yetu"*** **Waebrani 9:24.**

Kwa kuwa Yesu ni Kuhani mkuu wetu mbinguni, tunaweza kusongea kwa ujasiri katika enzi ya neema. Hivyo tukiwa na kukiri 'kwema' hivyo ni, kuongea kwa makubaliano na kulingana na neno la Mungu, ni ya muhimu katika kupokea jawabu kwa maombi yetu. Yesu Kristo amefanyika Kuhani mkuu aliye na ufanisi kwa kila mmoja kulingana na kukiri kwake. Kama kuhani mkuu Yesu anawakilisha watu wake kwa Mungu **(Warumi 8:34),** akiisha kutoa dhabihu kamili kwa ajili yetu.

Yesu Kuhani wetu Mkuu yuko mbinguni,
akiisha kuupokea ukombozi wa milele
kupitia damu yake na sasa anadumu akituombea.

YESU MTUME WETU

Mtume ni nini?

Mtume* SC Gr. *# 652 apostolos, kutoka* SC *# 649 apostello: kutenga, kutuma; mjumbe; mtume ni *Balozi wa injili kirasmi mwakilishi wa Kristo akiwa na nguvu za miujiza; ikitafsiriwa mtume, mjumbe, aliye tumwa* [SFLB word wealth p. 1598]. Kihalisi mtume ni *aliyetumwa.* Mtume ni yule aliyetumwa kwa niaba ya mwingine akiwa na mamlaka ya aliyemtuma kutimiza kikamilifu ambacho ametumwa, na kuwakilisha kikamilifu na kufanya aliyemtuma ajulikane.

Tafakarini mtume wa maungamo Yetu Yesu Kristo

Yesu anaitwa mtume wa maungamo yetu. Kukiri kwetu kunaongea kuhusu Yesu mtume kulingana na neno la Mungu. Yesu ndiye yule aliyetumwa kumwakilisha Baba kwetu.

Kama Mtume wa Mungu, Yesu anamwakilisha Mungu kwetu.
Katika yeye, Mungu anafunuliwa; kupitia yeye ufalme wa Mungu
unaachiliwa na mamlaka ya Mungu inafanya kazi duniani.

Ni nani aliyemtuma Yesu?

"*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee"* Yohana 3:16*. "Basi Yesu akawaambia tena, Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi"* Yohana 20:21. Ni wazi kwamba Mungu Baba alimtuma Yesu duniani toka mbinguni. Yesu alikuja kama Mtume, Balozi wa mbinguni; alikuja na mamlaka ya yule aliyemtuma.

Yesu alitumwa kufanya nini?

Yesu alikuja kufanya nini kama mtume aliyetumwa na Mungu? Kazi rasmi ya mtume ni gani? Yesu alitangaza katika **Mathayo 16:18, *"Nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda".*** Katika **Waebrania 3:3** ni wazi kuwa Yesu ndiye mjenzi wa nyumba ya Mungu. Mungu daima ametafuta kudumu na watu wake. Alituumba katika dunia na kila wakati ametamani na kukusudia kuishi nasi na hiyo ni mojawapo ya tangazo la mwisho katika kitabu cha ufunuo ***"Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao"*** **ufunuo 21:3.**

Paulo anasema kujihusu katika **1Wakorintho 3:10** "***Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake".*** Paulo tayari alikuwa amesema kwamba kanisa ni jengo la Mungu na Yesu ndiye mjenzi, "***yeye aitengenezaye nyumba ana heshima zaidi ya hiyo nyumba"*** **Waebrania 3:3.** Kisha **Waebrania 3:6** inatuambia kwamba sisi ni nyumba ambayo Mungu anajenga: "***Kristo, kama Mwana juu ya Nyumba ya Mungu; ambayo nyumba yake ni sisi".*** Kanisa ambalo Yesu anajenga ni nyumba ya Mungu na inajengwa na watu wanaoamini. Petro anaonyesha kanisa kuwa nyumba ya kiroho ikijengwa kwa mawe yaliyo hai ambao ni waumimi **(1Petro 2:5).**

MAHALI PA MUNGU PA KUDUMU ULIMWENGUNI

Kazi ya msingi ya mtume ni kujenga nyumba ya Mungu

Mungu atakuwa na mahali pazuri pa kukaa duniani. Mungu ametamani kufanya mahali pake pa kudumu na wanadamu. Wakati Mungu alipomuumba mtu kwanza, mke na mme, katika

dunia, alifurahia ushirika wazi nao. Mti wa uzima ulikuwa katikati ya bustani na mwanadamu alikuwa na uweza wa kuwasiliana na Mungu. Mtu aliumbwa kama Mungu, na alikuwa aishi milele katika ushirika wa Mungu, akikuwa katika ukomavu ndani yake.

Adamu alikuwa mtume wa kwanza, aliyeubwa na Mungu na akawekwa duniani kumwakilisha Mungu na kuleta utawala wa ufalme wa Mungu na akibeba dunia yote. Adamu na watoto wake walikuwa wajaze dunia wakirejesha na kujaza dunia, wakionyesha utukufu wa Mungu. Imekuwa ni makusudi ya Mungu kuijaza dunia na utukufu wake.

Baada ya anguko, kulikuwa na patakatifu duniani

Kwa sababu ya kutotii kwa mwandamu, ilimpasa aondoke kwenye bustani. Hata hivyo Mungu aliacha madhabahu ya ukuu duniani ili mwanadamu amkaribie Mungu na ashirikiane naye. **Mwanzo 3:24** inasema "***akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima".*** Makerubi wanalinda ama kufunika uwepo wa Mungu: hii inamaanisha kwamba uwepo wa Mungu ulikuwa duniani. Lakini mwanadamu aliendelea kwenda mbali.

Madhabahu yalikuwa mahali pa kukutana na Mungu.

Baada ya gharika, Nuhu alijenga madhabahu na Mungu akanena naye, akifanya upya maagano na mwanadamu kupitia Nuhu. Lakini mwanadamu alizidi kwenda mbali.

Wakati Mungu alimwinua Ibrahimu na akamwita aende nchi ya mbali, kitu cha kwanza ambacho Ibrahimu alifanya ilikuwa kuyajenga madhabahu na kuliitia jina la Bwana. Mungu alimtokea Ibrahimu na akafanya maagano naye na kupitia yeye kwa wote ambao watakuja kwa imani katika Mungu wa Kweli. Mungu amezidi kutafuta ushirika wa mwanadamu duniani.

Mungu alichagua kuishi katika hema

Mungu alimtokea Musa na akamuonyesha jinsi ya kujenga hema ambapo uwepo wa Mungu ungedumu ili awe na watu wake na Mungu akafanya maagano na Musa na watu wa Mungu. Hema hii ilikuwa na patakatifu na madhabahu.

Mungu alimruhusu Daudi ajenge hema ambapo Mungu alifurahia kudumu ili awe na ushirika na watu wake na Mungu akafanya maagano na Daudi na nyumba yake daima.

Hekalu: mahali pa kudumu zaidi

Mungu alimwezesha Sulemani kumjengea nyumba, hekalu, katika hali ya Agano la Kale hekalu ni mfano wa mahali pa Mungu pa kudumu duniani, sio tena mahali pa muda katika hema, na inaonyesha makao ya kudumu ya baadaye ya Mungu duniani ndani ya watu wake.

Mahali pa kudumu katika Agano Jipya

Yesu Mtume aliweka misingi ya nyumba ya Mungu kupitia huduma zake duniani kwa kuwainua mitume kumi na wawili ambao kupitia hao angeanza kujenga nyumba ya Mungu. Hatimaye mwisho wa kitabu cha Ufunuo mji mtakatifu umekamilika na unashuka duniani ili Mungu adumu miongoni mwetu kikamilifu.

Mtume anajenga nyumba ya Mungu

Katika Agano la Kale, Zerubabeli, liwali wa Yerusalemu baada ya uhamisho wa Babeli alikuwa ndiye aliyeruhusiwa kuijega tena nyumba ya Mungu (Hekalu) katika Yerusalemu **(Zakaria 4:6-10).** Maandiko yanasema "***mikono yake Zerubabeli imeiweka misingi ya nyumba hii, na mikono yake ndiyo itakayoimaliza"*** **aya 9.** Zerubabeli ni mfano wa Kristo Mtume, aliyepewa jukumu la kuijenga nyumba ya Mungu. Katika siku hiyo ilikuwa ni nyumba iliyokuwa

imejengwa na mbao mwerezi lakini nyumba ya Mungu leo ni kanisa la Yesu Kristo likijengwa na mawe yaliyo hai, hivyo ni, watu wa Mungu. Yesu aliweka msingi wa kanisa mwanzo wa nyakati na sasa mwisho wa nyakati ataikamilisha jengo la kanisa.

YESU ANAJENGA AJE NYUMBA YA MUNGU LEO?

Kupitia karama ya huduma tano

Katika **Waefeso 4:7-16**, mitume, manabii, wainjilisti, wachunganji na waalimu wanatakiwa kufanya kazi ya huduma kujenga kanisa, wakiileta katika ukomavu. Karama hizi zinahitajika kufanya kazi ya huduma ili kwamba kila mtakatifu ameandaliwa akiwekwa kwenye mpangilio akiweza kutenda kazi, akijengwa katika mwili akiungamanishwa vyema na kushikanishwa vyema, ili mwili ukue hata ukomavu.

Kwa kuiweka misingi

Katika maandiko kuna vipengele viwili vya muhimu katika msingi wa nyumba ya Mungu:

- **Msingi wa kwanza ni Kristo mwenyewe**

"*Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo"* 1Wakorintho 3:11. Yesu amekuja kujenga kanisa na yeye mwenyewe ndiye msingi. Yeye ndiye mwamba ambaye kanisa linajengwa juu yake **(1Wakorintho 10:4).**

- **Msingi wa pili ni huduma ya mitume na manabii.**

***"Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni"* Waefeso 2:19-20.** Msingi wa mitume na manabii inashikanisha kanisa mwamba, aliye Kristo.

Kwa Yesu Kristo akiwa ndiye njiwe kuu la pembeni

"*Yesu Kristo mwenyewe ndiye njiwe kuu la pembeni"* Waefeso 2:20.Kuta zinaweza tu kujengwa kama jiwe kuu la pembeni limewekwa vyema. Kuta zinafanyika na "***mawe yaliyo hai"* 1Petro 2:5.** Hawa ni watakatifu ambao wameunganishwa na kichwa na wamewekwa katika mwili wafanye kazi. Nguvu za kanisa zinategemea na kiwango ambacho limeungana na Kristo,

Kwa jengo lote likishikanishwa na kuungamanishwa

"*Katika yeye jingo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana"* Waefeso 2:21. ***Nyumba*** inajengwa ndani ya Mungu kupitia Kristo katika kila mahali. Wakati kanisa litakuwa limejengwa katika kila mahali litadhihilika kama mji wa Mungu katika kitabu cha ufunuo. Hili ni kanisa la duniani kote ambalo Bwana anajenga duniani.

Kupitia Roho ambaye anajenga watakatifu pamoja

"Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho" **Waefeso 2:22.** Katika kila mahali kunatakiwa kuwe na kanisa linaloeleweka ambalo waumini ni sehemu yake, ili Mungu akae. Kanisa ni nyumba ya kiroho, iliyojengwa na Roho. Mara tena tunatakiwa kusema kwamba kanisa ni nyumba ya Roho ambayo imejengwa na mawe yaliyo hai ambao ni watakatifu. **1Petro 2:10** inasema "***Ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema"*** ndio wale wamefanyika hekalu ya kiroho.

TUNAMPOKEA AJE YESU KAMA MTUME WETU LEO?

Kwa kuwapokea mitume/mtume ambao amewatuma

"*Awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi, ampokea yeye aliyenituma"* Mathayo 10:40. Tunampokea Yesu Mtume kwa kuwapokea mitume ambao Yeye ametuma. Hivi ndivyo Mungu aliamua kujifunua kwetu kwa dunia – kupitia mitume, hata kama Mungu alivyo jifunua kupitia Yesu, mtume wa Mungu aliyetumwa kutoka mbinguni.

Kwa kumfahamu Yesu kama Baba yetu

"*Jina lake ataitwa … Baba wa milele"* Isaya 9:6. Moja wapo wa Jina la Yesu ni ***'Baba wa milele'*;** Yeye ni Baba kwetu na sisi ni watoto wake. *"**Tazama, mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu"* Waebrania 2:13**. Kwa sababu ya majaribio ya kumueleza Mungu kupitia mafundisho ya Utatu, wakristo wengi hawafahamu kwamba Yesu ni Baba yetu; yesu na Baba ni umoja. **"*Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso"* Waebrania 2:10.** Tunafanyika wana kwa njia ya Yesu. Yeye ni Baba yetu na anatuleta kama wana kwa Baba yake.

Kwa kupokea ufunuo kwamba Yesu na Baba ni umoja

Yohana 14:4-6 inatuambia kwamba Yesu ndiye njia ya kwenda kwa Baba. Yesu anasema, "***Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba"* Yohana 14:7.** kisha Yesu anamwambia Filipo "*Aliyeniona mimi, amemwona Baba"* **Yohana 14:9.** Wakati unafikia ufahamu uliokomaa wa Yesu ni nani, utatambua kuwa Yesu na Mungu ni umoja. Baba anafunuliwa kupitia Kristo Yesu. "***Hamsadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu"?* Yohana 14:10.**

Ni Roho Mtakatifu anayeleta ufunuo huu kwetu. Wakati tunampokea kikamilifu Yesu kama yule aliyetumwa kutoka mbinguni, tunauona uso wa Mungu. "***Kwa maana nawaambia, Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana!"* Mathayo 23:39.** Ni wakati tutakapompokea aliyetumwa na Mungu ambapo tutauona uso wake. "***Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo* 2 Wakorintho 4:6.**

Kwa kumruhusu Yesu atuhudhulishe kwa Baba

Katika Yohana **17:6-18** Yesu anawaombea wanafunzi wake, akiwahudhurisha mbele ya Baba na katika Yohana **17:22-23** anaomba "***ili wawe na umoja kama vile sisi tulivyo umoja, Mimi ndani yao, nawe ndani yangu".*** Huu ndio ufunuo wa mahali ambapo Bwana analielekeza kanisa lake. Anataka kanisa lake liwe ***'umoja'*** hata kama vile yeye na Baba walivyo umoja. Kanisa linaweza tu kuwa umoja kama mwili wakati msingi wetu uko katika Kristo na hivyo kuwa na umoja na Baba. Huu ni umoja wa ndani kuliko wachungaji na viongozi wakija pamoja na kufanya kazi pamoja katika miondoko ya kushirikiana.

Kama vile Yesu na Mungu walivyo umoja, hivyo hivyo kanisa linatakiwa kuwa mmoja na mwingine. Tunaweza tu kuwa mmoja kwa kumpokea Yesu Kristo, ambaye Mungu alimtuma. Kama hatuna Mwana hatuna Baba **(1Yohana 2:23).** *Mtu akilitazama kanisa, wanatakiwa kumwona Kristo, na katika kumwona Kristo watakuwa wamemwona Baba. Hii ni kazi ya kitume ambayo Yesu anafanya katika kanisa lake leo kwa kurejesha asili ya kitume.*

Ni nini kinakosekana kanisani leo?

Kanisa kwa jumla halijamtafakari Yesu mtume wa maungamo yetu. Kihistoria na sasa, tumemtafakari Yesu Kuhani Mkuu na tumemkiri kama mwokozi na mkombozi lakini hatukuwahi kumtafakari kama Mtume wetu.

- **Kanisa linajengwa duniani**

Hatujafahamu kwamba kanisa linajengwa duniani: mwili wa washindi ambao wanaigeuza jamii ambayo wanaishi ndani yake kwa nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo; ambaye alifanyika mahali pa kuishi pa Mungu.

- **Watakatifu ni kama mawe yaliyo hai yanayojengwa pamoja.**

Hatujafahamu watakatifu ni mawe yaliyo hai yakijengwa pamoja, nyumba ya roho ya Mungu ya kukaa **(1 Petro 2:5).** Baba zetu katika Agano la Kale waliyajenga madhabahu ya mawe ya asiri na hapo wakapatana na Mungu. Katika Agano Jipya Mungu ametufanya kuwa mawe yaliyo hai na tunapojengwa pamoja kama nyumba ya Mungu, uwepo na uhakika na nguvu za Mungu zitafunuliwa duniani.

- **Mwili ulioungamanishwa na kushikanishwa pamoja katika Kristo**

Hatujafahamu kwamba kanisa sio tasisi ama idara lakini mwili, ulioungamanishwa na kushikanishwa katika Kristo. Yesu aliye mtume ndiye msingi wa kanisa; yeye ndiye jiwe la pembeni ambaye jengo lote limejengwa juu yake **(Waefeso 2:20);** Yeye ndiye kichwa ambaye mwili wote unakua katika mambo yote na unaungamanishwa na kushikamanishwa **(Waefeso 4:16).**

- **Kuwakubali mitume ambao wametumwa na Yesu kulijenga kanisa**

Hatujaelewa wala kupokea mitume ambao wametumwa na Yesu Kristo katika siku hizi kulijenga kanisa, nyumba ya Mungu, kwa kuiweka misingi, kufundisha hekima ya Mungu ya ndani ya neno la Mungu na kuachilia neema ili kanisa lipate kukua. Mitume hawa wanatumwa na Yesu, wamepewa mamlaka na yeye na kupitia hao Yesu anafunuliwa. Kupitia hao Yesu atatimiza kazi yake ya kitume ya kujenga kanisa.

Yesu kama Baba yetu

Umoja wa Mungu

Wengine hawafahamu jinsi Yesu anaweza kuwa Baba yetu lakini hii ni kwa sababu ya ufahamu wenye utatanishi wa asiri ya utatu wa Mungu, ambapo utu wa Mungu umetenganishwa kutokuwa umoja katika ufahamu wetu kwa sababu ya elimu ambayo tumepokea. Yesu anasema wazi kwamba yeye na Baba ni umoja. Umoja huu unaweza kujulikana tu kwa njia ya ufunuo; haitaeleweka kwa kujaribu kueleza Mungu ni nani kwa fundisho la kiakili ya Utatu. Fundisho la utatu ilitangulizwa mamia ya miaka baada ya maandiko kuandikwa. Mtu aliongezea maandiko, akijaribu kumueleza Mungu. ufunuo wa Mungu unapatikana tu katika maandiko na maandiko yanasema kwamba Mungu ametangazwa (kujulishwa) kupitia Yesu Kristo. "***Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua"* Johana 1:18.**

Tukimjua Yesu tunaweza kumjua Baba; kama kwa hakika tumemwona Yesu, sio katika mwili lakini katika Roho, tumemwona Baba kwa hakika. Ufunuo wa Mungu uko katika Kristo: "***Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake"* 2 Wakorintho**

5:19, na Katika Kristo "***Unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili"*** **Wakolosai 2:9.**

Kama kanisa linapokuja katika ukomavu, ufunuo wa Ubaba wa Mungu unapatianwa kanisani katika Yesu Kristo – ana ukuu katika mambo yote **(Wakolosai 1:18);** Yeye ndiye chapa ya nafsi yake **(Wabrania 1:3);** yeye ni mfano wa Mungu asiyeonekana **(Wakolosai 1:15).** Yohana anasema akina baba (waliokomaa) "***wanamjua Mungu tangu mwanzo"*** **1Yohana 2:12-14.** Hii inaongea kuhusu uhusiano uliokomaa na ufahamu wa Mungu – kuwa yeye hakika ni nani!

Kila kitu cha Mungu kinakuja kwetu kutoka kwa Baba kupitia Mwana kwa Roho Mtakatifu: hivi ndivyo Mungu hujifunua kwetu. Yesu ametuambia tayari katika **Mathayo 10:40** kwamba tukiwapokea mitume aliowatuma, tunampokea yeye. Katika **Yohana 20:21** Yesu anasema kwa wazi ya kwamba anawatuma mitume kwa njia ile ile ambayo Baba alimtuma. Hivyo anawatuma mitume walete ufunuo wa Mungu. Tunapompokea Yesu Mtume kupitia mahubiri na mafundisho ya mitume wake, tutapokea ufunuo wa Ubaba wa Mungu, ukituleta kikamilifu katika hali ya kufanyika wana. Lengo la Mungu ni wana wengi wakiufikia utukufu. Mungu atafunuliwa duniani kupitia wana wake.

Ni wakati wa kumpokea Yesu Mtume wetu

Uwana ndilo jambo kubwa

Kuna umri ambapo mtu anakubalika kikamilifu katika Uwana, kupokea urithi wa neema na ufunuo kupitia utimilifu wa Roho Mtakatifu. Huu ni umri wa ukomavu. Katika historia ya Israeli mtu alifika ukomavu na tayari kupokea urithi ["***sehemu ya mali inayoniangukia"*** **Luka 15:12]** katika umri wa miaka thelathini. Wakati Yesu alikuja kwa ubatizo, alikuwa "***Amepata umri wake kama miaka thelathini"*** **Luka 3:23.** Wakati Yesu alitoka katika maji ya ubatizo "***Mbingu zilifunuka; Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua"*** **Luka 3:21-22.**

Roho mtakatifu analeta urithi

Roho Mtakatifu alikuwa ni ahadi ya Baba na ilikuwa ni kwa Roho Mtakatifu Yesu alitembea katika urithi wake. Kutoka siku ya ubatizo wake alikuwa ni mtu tofauti.

Wakati Roho Mtakatifu alikuja siku ya Pentekosti, mitume ambao Yesu alikuwa amechagua walikuwa tayari kupokea urithi; walikuwa tayari kupokea Roho huyo ambaye Yesu alikuwa amepokea na wakawa watu tofauti – watu waliotiwa nguvu! Watu walio na uwezo wa kuongozwa na Roho! Wakiweza kuzifanya kazi za Baba! Yesu alitembea katika urithi wake kuanzia wakati wake wa ubatizo. Yesu aliingia katika utimilifu wa uwana wakati wa ubatizo wake, akisha pokea Roho Mtakatifu.

Wakati Yesu alimaliza kazi yake duniani,
Alisema 'naenda kwa Baba'.

Yesu alienda kwa Baba.

Sasa Mungu anafanya kazi kupitia mitume na watakatifu
Ambao ameinua
Kuonyesha na kumwakilisha yeye duniani.

Tunaokolewa kwa kumpokea Yesu kama Mwokozi wetu

Tutapata ujuzi wa uwana kwa kumpokea
Yesu Mtume wetu

Ni wakati wa kanisa kukua hadi
Ukomavu, kufanyika wana.

Ni wakati wa kumpokea Yesu Mtume wetu,
Kufanyika wana kwa Baba.

Sura ya tano

KUTEMBEA KATIKA URITHI WETU

Urithi wa Yesu

Zaburi 2:6-8 "*Nami nimemweka mfalme wangu Juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu. Nitaihubiri amri, BWANA aliniambia, ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa. Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, Na miisho ya dunia kuwa milki yako".*

Roho wa Mungu

Mathayo 3:16-17 "*Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamuona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye".*

Baba anapeana urithi kwa wana

Luka 15:22-23 "*Lakini baba aliwaambia watumwa wake, Lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike; mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni; mleteni ndama yule aliyenona mkamchinje; nasi tule na kufurahi"*

Aya 31 *"Akamwambia, Mwanangu, wewe u pamoja nami sikuzote, na vyote nilivyo navyo ni vyako".*

Kuja katika utukufu

Waebrania 2:10 "*Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwako, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso".*

Urithi uko duniani

Juzi nilikuwa nikifundisha semina ya wachungaji na viongozi katika afrika ya kati na nikauliza swali, 'Urithi wetu ni nini?' jawabu ikaja mara moja 'mbinguni!' Wakristo wengi wanafikiria urithi ni mbinguni. Kwa hakika petro alisema ya kwamba kuna urithi uliohifadhiwa mbinguni **(1Petro1:4)** lakini anaendelea kusema urithi huu "***utafunuliwa siku za mwisho"* aya 5.** Mbinguni ni thawabu yetu sio urithi wetu. Tunahitaji urithi sasa ata kama katika asili, urithi unapokelewa hapa na sasa. Urithi ni kitu ambacho kinaongeza na kinaleta faida na utajiri kwa maisha yetu sasa.

Thawabu iko mbinguni

Inashangaza ya kwamba Musa hakutembea katika urithi wake. Biblia inasema Musa *"**alikuwa mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu kama mtumishi"*** **Waebrania 3:5**, lakini katika aya hii katika waebrania inamlinganisha Yesu kama Mwana, ambaye anamiliki nyumba kwa njia ya urithi. Musa aliruhusiwa kuiona nchi, ambayo ilikuwa ni urithi wake, lakini hakuruhusiwa kuingia katika nchi ya ahadi. Musa alikuwa amepokea dhawabu mbinguni, lakini ilikuwa ni Joshua, mwana wake wa kiroho, ambaye alirithi.

Yesu aliahidiwa urithi

Ushindi dhidi ya shetani

Kuna maandiko mengi katika Agano la kale ambayo inatuambia urithi Wake ni nini. Inaanza na mwanzo **3:15** ambapo Mungu, akisungumza habari ya Hawa, anamtabiria shetani, "***nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino".*** Huu ndio mwelekeo wa kwanza unaoonyesha jinsi Masihi atafanya duniani, ya kwamba kama mwana wa adam, atapokea ushindi ambao ulitekwa na shetani.

Kuna 'mifano' mingi ya Kristo katika agano la kale. Kwa hakika viongozi wengi waliochaguliwa na Mungu na manabii walimwakilisha Yesu kwa njia moja. Kwa mfano, Yoshua ni mfano wa Kristo akiwaongoza watu wa Mungu katika ushindi juu ya adui na kurithi nchi. Daudi ni mfano wa Kristo akitawala na akitamalaki kama mfalme.

Mataifa na dunia yote

Ahadi maalum ilipatiwa Yesu ya urithi wake Katika **Zaburi 2**. Katika **aya ya 6** Baba Mungu anaongea "Nami ***nimemweka mfalme wangu Juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu".*** Kisha katika **aya ya 7-8** Yesu anazungumza habari ya kile ambacho Mungu anatangaza, "***Nitaihubiri amri, BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa. Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, Na miisho ya dunia kuwa milki yako".*** Mataifa yote ya dunia yaliahidiwa yesu kama urithi. Urithi ni kitu ambacho kinapokelewa duniani.

Kuyatawala mataifa

Katika **Zaburi 110** Baba Mungu anaongea kwa Mwana, "***Neno la BWANA kwa Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwafanyapo adui zako Kuwa chini ya miguu yako. BWANA atainyosha toka Sayuni Fimbo ya nguvu zako. Uwe na enzi kati ya adui zako"*** **aya 1**. Sehemu ya urithi ni kuketi na kutawala kati ya mataifa na kuwa na ushindi juu ya adui zake. Pia *"**atahukumu kati ya mataifa"*** **aya 6.**

Kuna vipengele vingi vya ahadi ya Mungu kwa Yesu katika zaburi na manabii ambazo zinazungumzia kuhusu urithi wake. *"**Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye; mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye; nimetia roho yangu juu yake; naye atawatolea mataifa hukumu"*** **Isaya 42:1**. Katika **Isaya 45:1** Bwana anazungumzia mfalme wa Uajemi, lakini maneno haya yanaweza kuwa yakizungumzia ahadi aliopewa Masihi: *"**Haya ndiyo BWANA amwambiayo Koreshi, masihi wake, … ili kutiisha mataifa mbele yake, nami nitalegeza viuno vya wafalme; ili kufungua milango mbele yake, hata malango hayatafungwa".***

Yesu alipokea urithi

Yesu alizaliwa kama mtoto wa kawaida, akiwa na mahitaji yote ya mtoto. Alikua kutoka utoto hadi ubarehe na akawa mtiifu kwa wazazi wake. Wakati alifanyika kijana barubaru pengine alifanya kazi na Yusufu kama seremala. Ilikuwa ni desturi yake kwenda kwa masinagogi na kusoma maandiko **(Luka 4:16).** Lakini jambo lilitendeka katika umri wa miaka 30, ambao ulikuwa ni umri wa ukomavu katika tamaduni za Kiyahudi. Huu ndio umri wa kijana katika Israeli kuingia katika urithi wake kikamilifu.

"***Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yorodani kwa Yohana ili abatizwe. Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kutimiza haki yote. Basi akamkubali"*** **Mathayo 3:13-15.** Ubatizo wa Yesu ulikuwa wa kutimiza haki

yote ya sheria. Alioshwa na mwana wa kuhani, ambaye alikuwa ni wa jamii ya kweli ya kikuhani, ili awe kuhani mkuu milele. Huu ndio wito wake wa mbinguni.

Urithi unapokelewa duniani

Yesu kuja katika ubatizo wake ilikuwa pia kupokea urithi wake; huu ulikuwa wito wake wa duniani. "***Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye"*** **Mathayo 3:16 -17.** Hii pia imeandikwa katika **Luka 3:21-22**, na **aya ya 23** inasema "***Na Yesu mwenyewe, alipoanza kufundisha, alikuwa amepata umri wake kama miaka 30".***

Yesu alijua Mungu alikuwa na wito wake maalum wa kutimiza na kutoka wakati huo wake wa kubatizwa ilianza kufunguka. Alikuwa ametumwa na Mungu na sasa ametimiza umri wa kutosha wa kupokea urithi wake. Alikuwa amekomaa, lakini tangia umri wa miaka 12 alikuwa ameanza kuandaliwa kwa sababu ya kazi yake ya maisha. Hata katika umri wa miaka 12 walishangaa kwa ufahamu wake.

Roho Mtakatifu bila kipimo

Yesu alipokea Roho Mtakatifu bila kipimo kwa ubatizo wake. Hangepokea Roho Mtakatifu akiwa mtoto; hakupokea Roho Mtakatifu akiwa na umri wa miaka 12; hata kama kijana akishiriki maandiko katika sinagogi, Hakupokea Roho Mtakatifu bila kipimo. Alikuwa angali mwana wa Yusufu, kijana wa Miriamu.

Yesu aliingia aje katika urithi wake?

Yesu alikuja katika ubatizo kwa utiifu wa Baba Yake. Hii ilikuwa ndio jambo kubwa la Yesu kutembea katika urithi wake. Alikuja katika utiifu wa mapenzi ya Baba Yake, "***kutimiza haki yote".*** Kupokea Roho Mtakatifu bila kipimo ilimwezesha Yesu kutembea katika urithi wake. Roho Mtakatifu alikuja juu ya Yesu akimpatia Uwana; sauti ya Baba ikaongea ikidhibitisha Uwana.

Sehemu ya urithi ni ushindi juu ya shetani

Hatua ya kwanza ilikuwa kuongozwa jangwani akakabiliane na shetani. Yesu alikuwa na uweza wa kushinda majaribio, hivyo ni kumshinda shetani duniani. Shetani tayari alikuwa amepoteza mahali pake mbinguni. Sehemu ya urithi wetu ni ushindi juu ya shetani hapa duniani. Kama matokeo Yesu alitoka jangwani akiwa amejazwa kuhubiri injili kwa ishara na maajabu, akiwa na mamalaka ya kuponya na kutoa mapepo **(Mathayo 4:1-25)**.

Urithi unajulikana kwa kukumbatia mateso

"*Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwepo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso"* **Waebrania 2:10.** Watoto hawapaswi kuteseka; hata na vijana hawapaswi kuteseka. Watoto katika kristo wanastahili kukua katika mahali salama chini ya kivuli cha baba. Lakini wana, ambao wameingia katika ukomavu, wanaweza kukumbatia mateso na kukomaa kupitia mateso.

"*Na, ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliompata; naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii"* **Waebrania 5:8-9.** Yesu hakuteseka mpaka wakati alikomaa na akaingia katika uwana. Hakuweza kukabiliana na shetani mpaka baada ya ubatizo wake. **Waebrania 12:5-8** inasema wana wanarudiwa na Baba.

Baba harudi watoto wachanga; anashugulikia wana waliokomaa, ili wafikie lengo la utimilifu. Ni kwa njia ya msalaba na kufufuka kwa Yesu ambao Yesu alipokea utimizo wa urithi wake ambapo wana wengi watembee katika utukufu wake.

Urithi wetu:

Tunapoanza kutembea katika urithi wetu katika Kristo, anaachilia wengine wengi katika wana kupitia sisi. Urithi wetu unafunuliwa na Roho mtakatifu, ni kutembea kikamilifu na Roho Mtakatifu.

Roho mtakatifu aliahidiwa na ni baraka ya Ibrahimu. "***Ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani"*** **Wagalatia 3:14**. Tunaingia katika ufalme kupitia kuzaliwa mara ya pili na Roho lakini tungali watoto bila kupokea urithi. Kisha tunapokea Roho Mtakatifu kwa nguvu na karama za kutuwezesha kukua lakini bado hatujapokea urithi.

Ujuzi wa pentekosti wa karne ya 21, hivyo ni, kuongea kwa ndimi ama kuwa na ujuzi wa karama za Roho Mtakatifu, haitoshani na kile kilicho watendekea mitume 12 na wanafunzi wengine katika chumba cha juu walichopokea siku ya Pentekosti. Wapendwa hawa walikuwa wamefanywa wanafunzi na kuandaliwa na Yesu. Mitume haswa walikuwa wamefika kiwango cha ukomavu katika kukua kwao kiroho na walikuwa tayari kupokea Roho bila kipimo. Ni wakati tunapofika umri wa ukomavu ya kuwa sisi kama wana tunapokea urithi wetu ambao ni kupokea Roho katika utimilifu, na hivyo kuwa na uwezo wa kufanya kazi ambazo Yesu alifanya **(Yohana 14:12).**

Ufalme ni urithi wetu

Ni wakati ambapo tunaongozwa na Roho Mtakatifu uwana unadhihirika. "***Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu"*** **Warumi 8:14.** Kutembea katika urithi wetu ni kuongozwa na Roho Mtakatifu katika maisha haya, sio kuishi kulingana na mwili. Urithi ni kutembea katika ufalme wa Mungu**,** katika haki, amani, na furaha ndani ya Roho Mtakatifu **(Warumi 14:17).**

Viumbe vinatakiwa kurejeshwa

Viumbe vyote vinatakiwa kurejeshwa kama sehemu ya urithi wetu. Neno la Mungu linaahidi ***"kwa kuwa viumbe vyenyewe vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa watoto wa Mungu"*** **Warumi 8:21.** Hii inaonekana ikiwa ya ajabu! Wakristo wachache wametafakari athari ya mafundisho ya Paulo. Tunaiona kuwa vingumu kufikiria itakuwa namna gani kwa hakika wakati wana wa Mungu watadhihirishwa kikamilifu hapa duniani, tukionyesha utukufu wa Yesu Kristo kikamilifu. Wakati yesu kwa dakika chache aligeuzwa, *"**sura yake mbele yao, uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe"*** **Mathayo 17:2.** Kubandirishwa huku kwa kiungu kulifanyika kwa Yesu akiwa na mwili wake wa asili, duniani. Wakati utukufu wa Mungu unafunuliwa kupitia wana wa Mungu kila kiumbe kitageuzwa.

Kuhubiri utajiri wa Kristo usiopimika

Njia ambayo Mungu amechagua ya kufunua utukufu wake katika dunia ni kupitia kuhubiri kwa injili. Injili inatakiwa ihubiriwe duniani kote. Neno kumhusu Yesu lazima lisikike kote duniani. Wote wapate kusikia! Wakati injili itahubiriwa kote katika mataifa, kila mmoja duniani atakuwa amepata nafasi ya kumchagua Yesu Kristo na atakuwa na hatima na yeye katika dunia mpya ambayo haki inatamalaki. Paulo anatuambia katika **Waefeso 3** ya kwamba kupitia

kuhubiriwa kwa Kristo, "***hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho"* aya 10.**

Wakati nilitembea Kenya mwaka wa 2000, ulikuwa ni ujuzi wangu wa kwanza kuona ufifio kwa njia kubwa. Nilikuja nyumbani Australia nikisema 'Yesu ana umaarufu sana Kenya'. Ilionekana ni kama kila mtu alikuwa akisema juu ya Yesu. Idadi ya makanisa na mikutano ya kuwafikia watu ilikuwa imeongezeka. Hata hivyo, kanisa Kenya, kama kwingineko, sasa linatakiwa kukua na kuufikia ukomavu na litembee katika urithi. Matokeo itakuwa ni kuyageuza mataifa, kijiji kwa kijiji.

Kurudi kwa Bwana ndicho kilele

Kilele cha urithi wetu duniani ni kurudi kwa Bwana Yesu Kristo. Anarudi kwa kanisa tukufu. Kurudi kwake kunafutiwa na utawala wa Kristo duniani na watakatifu wake kutawala na kutamalaki naye.

Upepo mbichi wa Roho wa Mungu unavuma kote katika mataifa

Watu wa Mungu wanaitikia kila mahali. Kuna kilio cha uhuru, kutoka kwa utumwa wa tabia za utamaduni wa kanisa. "***Basi 'Bwana' ndiye Roho; walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru"* 2 Wakorintho 3:17.** Injili ni ya Bwana na kupitia injili himaya ya mbinguni, huo ndio ufalme wa Mungu, unafunuliwa. Mungu anawakomboa watu wake kutoka kwa laana ya udini na taasisi na kulifunua neno kulingana na ahadi zake.

Katika **Waefeso 3**, katika **1 Wakorintho 2:6-10** na katika **Wakolosai 1:24-29**, mtume Paulo alizungumza kuhusu siri iliyofichwa kwa vizazi. Kanisa la kwanza ambalo liliongozwa na mitume ambapo karama zote na huduma za Agano Jipya zilifanya kazi, zilibadirishwa na njia zilizopangwa za mtu na ufunuo wa siri kwa watakatifu, ikiwawezesha kutembea katika urithi.

Kuna hali mpya inaanza kushika waumini

Kuna shauku ya uhakika katika watakatifu; shauku ya kuhusika kwa kibinafsi katika maisha ya kanisa na kazi ya huduma. Kuna shauku ya kufanya kazi katika mwili na kutembea katika ushindi. Kuna hali ya kukosa saburi kwa wachungaji na viongozi ambao wanawafunga watakatifu katika mawazo ya kidini, na ambao wametawala mikutano ya kanisa, wasiwaruhusu watakatifu kufanya kazi.

Kwa hakika ni furaha kubwa kuwa katika mikutano ambapo kila mshiriki, wakiwepo watoto, wanapokelewa na karama zao na huduma kupata nafasi. Kuna haja kubwa ya usahihi, mahubiri yaliyo wazi na mafundisho kutoka kwa maandiko. Kuna haja ya watakatifu wote kufanywa wanafunzi wa neno, wakiweza kuhubiri na kufundisha, na kuonyesha maisha ya ukristo.

Ni wakati wa ushirika [ushirika wa Roho] na udhehebu ukome miongoni mwa wale ambao wameziacha miundo ya dini lakini wamejilainisha upya katika miundo, mitandao iliyoainishwa. Hawa hawajafahamu kwamba kanisa la kwanza kimaandiko na kihistoria lilikuwa halijapangwa vile lakini lilikuwa ni mwili wa watu waliojengwa pamoja kupitia mahusiano na mitume wa kweli wa Bwana Yesu Kristo.

Ukristo wa kiutume una msingi kikamilifu katika neno la Mungu

Ukristo wa kiutume sio wa kidini, sio wa kitaasisi, msingi wake kikamilifu uko katika neno la Mungu, sio utamaduni wala mapenzi ya mtu. Kama vile mtu mmoja amesema, ***"hakuna***

kitu cha kumiliki, hakuna kitu cha kujiunga", lakini pana maisha ya kuishi, neema ya kupokea, na ushirika wa upendo wa kukuza katika wote, tunapotumika kwa furaha katika kusudi la Mungu linalofunuliwa katika kizazi chetu.

Mwana fulani apokea urithi wake

Urithi

Urithi umekwisha pokelewa na Yesu Kristo kwa ajili yetu. Biblia inatuambia sisi ni warithi pamoja naye **(Warumi 8:17).** Wakati wote alikuwa na urithi ambao Baba yake alikuwa amemuahidi. Aliupokea urithi huu katika ubatizo wake na akaanza kutembea ndani yake. Ubatizo wake ulikuwa ndio mwanzo wa kazi yake ya utimilifu. Kisha ***"Alikamilishwa kupitia mateso"*** **Waebrania 2:10,** mwishowe akafanya sadaka iliyo kamili msalabani, hivyo akihakikisha urithi kwetu. Yesu anawaongoza wana wengi katika utukufu **(Waebrania 2:10).** Mungu ametupatiana kwa Yesu; tumepokea roho wa uwana. Unafikia wakati [*'kairos'* wakati: wakati wa neema] wakati tupo tayari kupokea urithi - ni urithi wa neema, unaopokelewa kwa imani tunapo tembea katika utiifu wa neno la Mungu.

Urithi umewekwa kwa sababu ya wana

Katika **Luka 15:11-32**, tuna hadithi ya mwana mpotevu. ***"Mtu mmoja alikuwa na wana wawili; yule mdogo akamwambia babaye, Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia. Akawagawia vitu vyake"*** **aya 11-12.** Huyu Baba alikuwa na wana wawili; wote wawili walikuwa wamefikia umri wa ukomavu – walikuwa wamewekewa urithi. Katika tabia za Kiyahudi, Baba alikuwa anamwekea mwana sehemu ambayo ingemwezesha mwana kujiimarisha katika maisha, pasina kumtegemea baba.

Mwana alitapanya urithi wake kwanza

Yule mwana mdogo alikuwa mpumbavu; hakuuliza mashauri afanye nini na urithi; hakuhesabika. Mwisho alitubu, akitambua kwamba ambacho alikuwa akitenda kilikuwa hakina mazao, hakina maana na hakipendezi. Huyu mwana alimjua baba yake na alikuwa amepokea urithi wake lakini alikuwa amekosa maarifa. Kisha akatubu akageuza mawazo yake; lakini ni lazima pangekuwa na ushahidi wa kutubu. Alikumbuka jinsi nyumbani kulikuwa, na kuanzia wakati huo alijua jinsi ingelikuwa kwake sasa, kwa kuwa alikuwa mtoto aliyekuwa akikomaa katika nyumba ya baba yake.

Alidhania kwamba sasa angekuwa mtumwa

Aliazimu kurudi nyumbani lakini alitaka awe mtumwa. Alijihisi kutofaa kama mwana. Alikuwa na mawazo ya mtumwa; wazo la mtumwa kuadhibiwa baada ya kufanya kosa na kupewa dhawabu kama ametenda vyema. Hata kama alikuwa amekua katika nyumba ya baba, hakuwa amejua moyo wa baba.

Mawazo ya mtumwa yametawala kanisani

Wengi wetu hawajakua katika nyumba ya baba; badala yake wamekua katika makanisa yanayoongozwa na watumishi [wahuduma]. Wahuduma wanaweza kujikataa ama wakataliwe, lakini mwana ni mwana na hakuna jambo ambalo linaweza kuyabadirisha hayo.

Uwana ni hakika

Baba alimwona na akamhurumia [akina baba wa kweli wana rehema]. Wengi hawajaelewa kwamba hao ni wana kwa hivyo wanatarajia kuadhibiwa, kulipiza kizazi na kutohitimu badala ya kukemewa na kurudiwa na baba ili kuwaleta kikamilifu katika urithi wao. Kuna uhakika wa kutembea katika kufanyika mwana, kuna uhakika kwamba haijalishi

yatokeayo, mtu hawezi kutohitimu. Wakati muumini anafikia umri na kuuliza wapewe urithi, uhusiano ambao muunini ako nao na Bwana ni wa Baba yao, na uhusiano walionao kanisani, inaleta uhakika wa hatima yao.

Kuna usalama na kupatianwa ambayo inaletwa na Baba
ambayo haijulikani kikamilifu mpaka mtu afanyike mwana.

Baba wa kitume hupatiana urithi

2 Timotheo 2:2 inaongea kuhusu urithi ikipatianwa kutoka kizazi hadi kizazi kanisani. Mtume Paulo kama baba alimfundisha Timotheo pamoja na wengine wengi na sasa anamuagiza Timotheo apitishe kwa watu '*waaminifu'* ambacho alikuwa amepokea kutoka kwa Paulo. Watu waaminifu nao wawapitishie wengine. Kumekuwa na kukosekana kwa urithi ambao unapitishwa kutoka kwa kizazi kimoja cha uongozi wahuduma kwa kizazi kingine kanisani. Tumekuwa wepotevu; lakini zaidi tumekuwa yatima. Ni kama tumekuwa nchi ya mbali; kwa hakika tumepoteza urithi wetu. Wengine hata hawakujua kwamba wana urithi. Kama hatujakuwa katika nyumba ya Baba, hatujui nyumba ya baba inakuwa aje.

Baba alipiga mbio, akamwangukia mwanawe akambusu. Huu ni moyo wa baba ukidhihirika. Alikuwa na shauku ya mwanawe kurejea nyumbani. Mwana alijaribu kuzungumza na baba, akijitoa kama mtumishi lakini baba hakusikiza. Alimpokea mwanawe.

Vazi, pete na viatu

Baba alimfunika mwanawe na **vazi**, akamtia na **pete** kwa kidole na **viatu** miguuni mwake.

Vazi linazungumza kuhusu kufunikwa na baba. Sisi sote tunahitaji kufunikwa, na sasa Mungu anarejesha mitume ambao wanaweza kueneza kifuniko cha Kristo mwenyewe kwa watoto wake. Wana haswa wana kuelewa kuliko komaa kwa maana ya kufunikwa na baba wa kitume. Kuna kitambulisho hapa vile vile. Wakati wowote ambapo mwana alikuwa akionekana katika vazi la baba angelitambulikana kwa vazi kuwa mwana wa baba. Ufahamu wa 'mwana' kuwa umoja na sawa na 'baba' ni jambo la kitamaduni ambalo wengi wetu hatulielewi leo ila hali kuelewa kule ni kwa muhimu katika kumuelewa Yesu na Baba yake.

Pete inawakilisha mamlaka ya Baba ikipewa mwana. Farao alimpatiaYusufu pete kama hiyo **(mwanzo 41:42)** na katika **Hagai 2:23,** YAHWEH alimchagua Zerubabeli kama ***"Pete yenye mhuri"*** kama mwakilishi wa YAHWEH wa kitume

Viatu ni vya kutembea katika urithi, hivyo ni kutembea katika urithi uliopeanwa na Baba. Kupatianwa kwa vazi, pete na viatu ni uhakika wa urithi wa kiroho. Mwana alipoteza urithi katika asili lakini baada ya kujifundisha somo, alitubu na akarudi katika nyumba ya Baba, na akafikia urithi mkuu zaidi.

Kifuniko cha Yesu kinaachiliwa kupitia mitume

"***Na mwanadamu atakuwa kama mahali pa kujificha na upepo, na mahali pa kujisitiri na dhoruba; kama mito ya maji mahali pakavu, kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi yenye uchovu. Tena macho yao waonao hayatakuwa na kiwi, na masikio yao waskiao yatasikiliza. Tena moyo wa mtu mwenye hamaki utafahamu maarifa, na ndimi zao wenye kigugumizi zitakuwa tayari kunena sawasawa"*** **Isaya 32:2-4.** Hii ni picha ya ajabu ya kiunabii ya ni nini kinachofanyika kuwa katika kikundi cha kitume, kuwa na baba wa kitume na kujua uhakika wa uwana. Kwa njia nyingine, aya hizi zinatuonyesha vipengele muhimu za urithi ambao tunastahili kutembea juu yake.

- Usalama na ulinzi: mtume anapatiana usalama – ***"kama mahali pa kujificha",*** na mahali pa kujistiri – ***"mahali pa kujificha na dhoruba".***
- Kinywaji cha kiroho na kivuli: ***"mito ya maji"*** inaachiliwa kupitia Yesu mtume; hii inafanyika katika vikundi vya kitume; ***"kama kivuli cha mwamba mkubwa":*** hii inazungumza habari ya Kristo, mwamba, unaofunuliwa kupitia mitume kama alivyosema katika **Mathayo 10:40**; inaongea habari ya kivuli. Tuko chini ya kivuli cha Kristo tunapowekwa katika mpangilio wa kitume.
- Siri imefunuliwa: ufunuo wa siri utaonekana ***"macho… hayatakua na kiwi",*** na ufunuo utaeleweka ***"masikio… yatasikiliza".***
- Ufunuo unapokelewa na kunenwa: nidhamu ya Mungu inaleta ufahamu: ***"moyo wa mtu mwenye hamaki utafahamu maarifa",*** na pia wale ambao hawakuwa na uhakika watapata uwezo wa kunena siri, ***"na ndimi za wenye kigugumizi zitakuwa tayari kunena sawasawa".***

Tunashuhudia ya kwamba vipengele hizi ambazo zimeachiliwa kupitia baba wa kiroho ni za kweli na zinajulikana katika kikundi cha kitume kilicho SHILOH

Mungu anarejesha akina baba kanisani

Akina baba wana kushughulika kwa mzazi kwa sababu ya watoto. Mzazi aliye na moyo wa kweli anafurahia wakati mwana anafanya vizuri na atajitoa kwa sababu ya watoto; na atafurahia akiona wamefanya vyema kuliko yeye alivyofanya. Baba hufurahia ufanisi wa wana, hata hivyo wakati mtumishi anafanya kazi kama bwana katika nyumba, huyo anahakikisha hakuna mwingine anayeinuka ili ampe changamoto katika nafasi yake. Hivi ndivyo imekuwa kwa wachungaji wakuu wengi na maaskofu kanisani mpaka sasa. Akina baba wanaporejeshwa kanisani, kuna furaha kuu! Kila mtakatifu anajua ako na nafasi, anakubalika na anahimizwa kukua na kufanikiwa.

Baba wa mwana mpotevu aliona moyo uliobadilika hakutizama vile mwana alikuwa amefanya. Katika macho ya ulimwengu huyo mwana angekuwa hajastahili. Machoni pa makanisa mengi siku ya leo, mtu kama huo kwa hakika hastahili kuwa 'mzee'. Lakini kwa baba huyu alikuwa mwana. Sisi hua tunafanya jaribio kwa yale tunayaona kwa nje lakini baba huona moyo.

Kuja nyumbani

Katika **Luka 15:23** kuna 'kuja nyumbani'. Kuja katika uwana ni ujuzi kama huo: ni kupokelewa na baba. Hio ndio ilikuwa njia pekee niliyoijua ya kuelezea ujuzi wangu wa kufikia uwana. Niliwaambia marafiki zangu, '*nina ujuzi wa kushangaza, nimefika nyumbani'* ujuzi huu ulikuja kwa sehemu kwa matokeo ya kupokelewa wazi na mtume mwingine katika kongamano.

Kuna kufurahia wakati mwana anakuja nyumbani. Baba aliamrisha yule ndama aliyenona sana aandaliwe kwa heshima ya mwana wake. Kumbuka katika **mwanzo 18,** wakati Bwana alitembelea Ibrahimu, alimuandalia ndama aliyenona; imehifadhiwa ya wageni waheshimiwa. Baba wa kweli anaheshimu wana wake.

Yule mwana mkubwa alikuwa hajauliza baba urithi lakini alipokea wakati yule mwana mndogo alipoomba. Yule mwana mkubwa alikuwa hajafurahia urithi wake; alikuwa akitawaliwa na mawazo ya mtumishi, akiwa na shughuli mingi kutumika awe mwana **(Luka 15:29)**.

Sisi sote ni wazaliwa wa kwanza katika ufalme wa Mungu. Yule mwana mkubwa alikuwa amerithi lakini alikuwa haelewi. Yule mwana mndogo aliomba urithi wake lakini hakuufurahia wala kuuelewa. Yule mwana mndogo alirejeshwa na baba. Kama alikuwa

mtumishi tu na akawa ameenda na pesa za baba, baba angemtumania na akamatwe. Kwa sababu alikuwa mwana baba alitamani arudi na alirejeshwa kikamilifu. Kwa hakika alipokea hata zaidi.

Mtumwa afanyika mwana

Katika kitabu cha Filemoni kuna habari za ajabu za mtumwa mmoja mkimbizi ambaye angehukumiwa kifo kama angeshtakiwa. Alizaliwa katika uwana kiroho na mtume Paulo. Alitumwa nyumbani kwa bwana wake, sio kama mtumwa lakini mwana. Paul anamsihi Filemoni, Bwana, asimwadhibu, lakini ampokee Onesimo tena kama mwana wa mtume na atakaekuwa na faida kwa Filemoni vile vile. Paul anasema "***nakusihi kwa ajili ya mtoto wangu niliyemzaa katika vifungo vyangu, yaani, Onesimo; ambaye zamani alikuwa hakufai, bali sasa akufaa sana, wewe na mimi pia; niliyemtuma kwako, yeye mwenyewe, maana ni moyo wangu hasa"*** **aya 11 -12** "***maana, labda ndiyo sababu alitengwa nawe kwa muda, ili uwe naye tena milele"*** **aya 15.**

Paulo alikuwa **"*amempata"*** Onesimo kama mwana wa kiroho. Mtu huyu kwanza alikuwa hana urithi, hana hatima, hana tumaini! Alikuwa mtumishi kwa maisha hata kama pengine alikuwa muumini na sehemu la kanisa la Kolose ambayo ilikuwa ikikutanika katika nyumba ya Filemoni. Na pia alikuwa akijulikana na Paulo kwa maana alikuwa ameenda njia yote kule Rumi kumhudumia paul akiwa korokoro.

Kupitia huduma yake kwa Paulo ambaye alikuwa ni baba wa kitume, kwa haraka alikuwa akifikia ukomavu, akafanyika mwana, akapokea urithi wake. Wakati Paulo alimtuma amrudie Filemoni alisema ***"mpokee huyu kama mimi mwenyewe***". Paulo anahakikishia Filemoni ya kwamba huyu kijana atakuwa baraka kwa Filemoni ***"milele".*** Urithi tulionao katika Kristo haujui vifungo na haujui kikomo.

Uhusiano wa Baba na mwana

Hadithi hii inaonyesha kwa nguvu sana uhusiano wa uwana wa kiroho na baba wa Kiroho. Inaonyesha tofauti katika maisha ya mtu mara anapofanyika mwana na anaanza kutembea katika urithi wa neema ya Mungu. Baba wa kitume, Paulo, alichukua jukumu la kuwajibika mwenyewe kwa sababu ya mahitaji ya mwana wake wa kiroho, hata kwa kiwango cha kujitoa kulipa deni yoyote ambayo huyu kijana alikuwa nayo. Kuna mapendekezo ya nguvu katika waraka huu ya kwamba alikuwa amemuibia Filemoni wakati alitoroka.

Uhusiano wa mtume na mzee

Hadithi hii pia inaonyesha uhakika wa uhusiano wa mtume na mzee wa kanisa la mahali pamoja. Paulo na Filemoni walifurahia uhusiano wa pande zote wa kiurafiki; walikuwa wafanyikazi na wanjori. Paul anazungumza habari ya ushuhuda wa Filemoni katika **aya ya 5-6**, na anashiriki jinsi Filemoni amekuwa furaha kwake na amekuwa akimburudisha katika maisha. Paul anamuuliza Filemoni amuandalie chumba ili atembee. Kulikuwa hakuna kufanyisha kazi mamlaka ya uongozi; walifanya kazi pamoja sio kwa sababu walitoka kwa taasisi moja ama mtandao lakini ni kwa sababau walikuwa na uhusiano katika Bwana.

Paulo anasema katika **aya ya 8** ya kwamba angemuamuru Filemoni ampokee Onesimo tena bila adhabu kama mwana ndani ya Bwana, lakini katika **aya ya 9** anasema "***lakini, kwa ajili ya upendo nakusihi".*** Ni wazi kwamba Filemoni "***ni mpendwa wetu, mtenda kazi pamoja nasi"*** **aya ya 1** pamoja na Paulo, lakini hakuna dalili yoyote ya kwamba ana uhusiano na Paulo kama mwana na baba. Ni wazi ya kwamba Filemoni ni mzee wa kanisa katika nyumba yake na anahusiana na Paulo kama mtume wa kanisa hilo na kwake. Baba wa kitume wa kweli

anaonyesha upendo na anafanya mambo kutokana na upendo, ambapo mwangalizi anaweza kuwa akiamuru akifanyisha mamlaka ya kiroho kazi kutokana na nafasi yake. Paulo anatuonyesha jinsi mamlaka ya kiroho yanatumiwa –katika upendo.

Kutembea katika urithi wetu

Urejesho wa baba wa kitume kanisani kwa jumla ni wa juzi. Wengi wetu tumekuwa katika makanisa bila baba wa kiroho. Hata kama kumekuwa na kujua urithi unapeanwa, kwa sababu ya mifumo ambayo imekuwa ikifanya kazi kanisani na ukosefu wa usalama na kukosa kitambulisho miongoni mwa viongozi wa huduma urithi haujapatianwa. Kwa hakika wakati mwingine kinyume na hayo yanatendeka ambapo ‘wana’ wamenyimwa urithi wao sio kwa sababu ya makosa walioyafanya kwa upande wao lakini ni kwa sababu ya shinda ya uongozi.

Sasa tunaishi katika nyakati za urejesho.

Tunatambua ya kwamba kuna baba wa kweli wa kiroho.

Kama matokeo tumeanza kupokea urithi wetu.

Hatujakuwa kwa njia hii hapo mbeleni.

Sura ya sita

SIKU YA WATAKATIFU

Ufalme ndio urithi wa watakatifu

Daniel 7:18 *"Lakini watakatifu wake Aliye juu wataupokea ufalme, na kuumiliki huo ufalme milele, naam hata milele na milele".* ***Aya 27*** *"Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele, na wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii".*

Tumeitwa wote tuwe watakatifu

1 Wakorintho 1:2 *"Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakatifu, pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu: Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo"* **1 Wakorintho 1:3**.

Washirika wa kanisa ni watakatifu

Waefeso 1:1 *"Paulo mtume wa Yesu Kristo, kwa mapenzi ya Mungu; kwa watakatifu walioko Efeso wanaomwamini Kristo Yesu".*

Watakatifu watakamilishwa

Waefeso 4:12 *"Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, ata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe".*

Yesu anakuja kwa watakatifu wake

2 Wathesalonike 1:10 "*Yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile, (kwa sababu ushuhuda wetu ulisadikiwa kwenu)".*

Ufalme wa Mungu unatawala watu wote duniani

"***Nikaona katika jozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya bingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo haitapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa"*** **Danieli 7:13-14**. Ufalme ni ufalme wa Mungu duniani. Ni ufalme wa Mungu ukitawala watu wote na mataifa duniani. Ni ufalme ule ambao ulihubiriwa na Yesu kupitia injili alipokuja duniani.

Kumbuka injili ni injili ya ufalme wa Mungu.

Hatimaye ufalme wa Mungu unachukua nafasi ya falme zingine zote

"Wanyama hao wakubwa walio wanne ni wafalme wanne watakaotokea duniani. Lakini watakatifu wake Aliye juu wataupokea ufalme, na kuumiliki huo ufalme milele, naam

hata milele na milele" **Danieli 7:17-18**. Watakatifu hupokea ufalme kwanza kwa kusikia injili ikihubiriwa na kwa kuzaliwa mara ya Pili. Yesu alisema wazi ya kwamba tunaingia katika ufalme kwa njia ya kuzaliwa mara ya pili **(Yohanna 3:5-6)**. Ufalme huu sio wa dunia hii lakini tunauingia tukiwa katika dunia hii na hatimaye ijaze dunia yote na utukufu wa Mfalme **(Danieli 2:44).**

Ufalme huo unapewa watakatifu

"*Nikatazama, na pembe iyo hio ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda; hata akaja huyo mzee wa siku, nao watakatifu wake Aliye juu wakapewa hukumu; na majira ya kawadia watakatifu waumilki ufalme"* **Daniel 7:21-22**. Unakuja wakati, na sasa umefika, wakati watakatifu watamiliki ufalme. Waumini wengi wana nia kinyume, ya kushindwa kwa habari ya nyakati za mwisho wa dunia. Mnyama alishinda kwa kipindi tu. Danieli anatabiri miaka 2600 iliopita. Hukumu imefanywa [itafanywa] ikiwapendelea watakatifu. Watamiliki ufalme. Yesu anatuambia tuombe ufalme uje! Unakuja duniani. "ni mapenzi ya Baba yalio mazuri kuwapa ufalme" **(Luka 12:32).**

Mnyama atakuwa na mamlaka juu ya watakatifu kwa muda

"Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uweza juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa" **Ufunuo 13:7**. Inaonekana **ufunuo 10** inasungumzia mnyama yule tu ako katika **Danieli 7**.

Mamlaka aliopewa mnyama ni ya muda mfupi, "***hapa ndipo penye subira na imani ya watakatifu"*** **Ufunuo 13:10**. Mnyama ameruhusiwa kuwashinda watakatifu kwa muda lakini watakatifu watakuwa washindi kupitia imani na subira. Kumbuka **Waebrania 6:12** inatuambia ni kupitia imani na subira tutarithi ahadi. Hakuna njia ya mkato. Imani sio kama kufungua kahawa ilio tayari; Imani ni kama kupanda mbengu kwenye mchanga ambayo itakua iwe mmea na uvune punje za kahawa na usiage ndio upate kutumia. Imani na subira zinafanya kazi sambamba. Subira inawakilisha vipengele tunaposubiri neno la imani lilete matunda yaliyoahidiwa.

"***Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati"*** **Daniel 7:25.** Kuna watakatifu na kuna mnyama na kuna vita.

Historia ya karne ya ishirini inaonyesha hesabu ya madikteta wengi wakiinuka kutoka kwa mataifa kama waliotangulia ama mfano wa mnyama, hata kama katika utawala wa kirumi ambapo walikuwa ni mfano wa mnyama katika mwanzo wa nyakati. Adolph Hitler na Nazisim, Joseph Starlin na starinizim katika USSR, Mao Tse Tung na ukomunisti katika China na mifano mingine michache kama Idi amini katika Uganda wote ni mfano wa mnyama akitawala. Hawa wote waliwatesa wakristo na wakaongea maneno ya majivuno kinyume cha Mungu, na wakatengeneza utamaduni ili waabudiwe wao wenyewe na wakabadilisha majira na sheria. Hata pia walibadilisha lugha katika USSR; kwa mfano, katika Kazachstan, ilibidi biblia itafsiriwe tena baada ya miaka sabini ya communism/ukomwinisti kwa sababu watawala walikuwa wamebadirisha lugha ili wapate nguvu juu ya watu. Hali ya wakati huu katika Kaskazini mwa Korea inathihilisha matunda ya, utawala wa 'mnyama'.

Mwishowe mnyama anapoteza utawala

"***Lakini hukumu itawekwa, nao watamwondolea mamlaka yake, kuyapoteza na kuyaangamiza, hata milele"*** **Danieli 7:26.** Utawala na mamlaka ya shatani ulimwenguni umewekewa kuangamizwa milele.

Na Kristo atamiliki

"Ufame wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele" **Ufu 11:15.** Yesu Kristo ana mamlaka yote mbinguni na duniani **(Mathayo 28:18),** na amepatiana mamlaka yake kwa kanisa la kiutume. Injili ya ufalme itahubiriwa katika dunia yote kwa kila taifa **(Mathayo 24:14).** Majira haya yanafikia mwisho kwa haraka. Wakati wa shetani kutawala unafikia mwisho. Wakati wa mpinga Kristo umeisha. Kuna jalibio la mwisho la mnyama sasa, duniani kote, kujaribu kabadili nyakati na majira kupitia dini za uzushi na ibada ya miungu ya uongo. Mungu kwa jina tofauti na nabii asiye wa kimaandiko ameinuka, "***yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila chote kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu"*** **2 Wathesalonika 2:4**. Hii inaonyeshwa na dini za dunia leo ambazo zinajioa na kutii njia zao za kuabudu na sheria.

Kisha watakatifu watatawala duniani

"Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele, na wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii" **Danieli 7:27**. Hii ni siku ya watakatifu!

Siku ya watakatifu ni siku hiyo ambayo kila mshirika wa mwili wa Kristo amekamilishwa, hivyo ni, akiwa amelainishwa kikamilifu na kutayarishwa kufanya kazi akiwa huru na kikamilifu kama mtakatifu wa Mungu Aliye juu, akiubeba utukufu na kuzibeba nguvu zake, na akiongea ukweli wa neno lake, akiwawezesha wengine wengi waje katika uhuru ambao watakatifu wanao kama wana katika ufalme wa Mungu.

Kuelewa wito wa Mungu

Hata baada ya Yesu kufufuka kutoka wafu, mitume wake hawakuelewa ufalme wake ama vile injili inatakiwa kufanya kazi majira haya, kati ya kufufuka na kupaa kwa Bwana na kurudi kwake. Katika **Mdo 1:6**, walikuwa wangali wakiuliza maswali yenye msingi wa mambo ya ulimwengu, mambo ya muda ya Yesu na ufalme wake.

Leo katika mengi ya kanisa nia ya wengi katika uongozi katika mwili imeingizwa kufikiri mambo ya dunia, mambo ya mda mfupi. Wengi wana uoga kuuliza maswali ya msingi ya Mungu na neno lake. Badala ya hayo wengi wanaonyesha utamaduni wao na njia ya kutenda mambo, haswa katika taasisi zao na miundo yao ya nguvu kinyume cha neno la Mungu. Wengi hawataki kuuliza maswali, kutoa changa moto, kuongea neno la Mungu pekee, na kutopenda kuondoka katika utiifu kwa wito wa Bwana. Utafanya nini dini ambayo umekuwa ukiifuata imetoka kwa maandiko kuingia kwa dhambi ya hathara? Yesu anataka kupeana kwa watakatifu walioshinda nguvu juu ya mataifa, juu ya watu; fimbo ya chuma ambayo inakiharibu chombo cha mfinyanzi; hili ni neno la Mungu lisilo kubaliana **(Ufu 2:26-27).**

Wakati Yesu aliwaita wanafunzi wa kwanza, wito Wake ulikuwa sio wa kukosea na haungeepukwa: "***Njoni mnifuate, nani nitawafanya kuwa wavuvi wa watu"*** **Mariko 1:17.** Simoni na Andrea "***Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata"*** **aya 18.** Yesu anasema, 'nitakubadilisha; niweke miundo mipya katika maisha yako'.

Ni wakati wa huduma tano kuwaandaa watakatifu

Katika dunia yote ya kanisa, kuna kiwango cha juu cha kutokutoshereka. Watakatifu wengi na viongozi wengi wachanga kanisani, hawajaandalika kuendelea na miundo, iwe ni mipangilio ya makanisa makubwa, ama makanisa yanayodhaniwa kuwa yamefaulu ya kipentecosti. Kanisa Australia limejaa wakristo katika 'majificho', wakiniginia mahali walipo ilahali wakijua kwamba kanisa la mahali pamoja kama lilivyo, halitaleta mazao

Asiri ya kibiblia ya washiriki wa kanisa ni gani?

Kumekuwa na kuna njia badala zinazokubalika za washirika wa kanisa. Swali la msingi ambalo linawatatiza viongozi wa kanisa ni hili la 'washirika wa kanisa'. Watakatifu wanaitwa 'washirika wangu' ambayo haionyeshi mahali pao waliopewa na Mungu kama washiriki katika mwili wake **(1Wakorintho 12:18),** lakini wanazungumza kuhusu washirika wa kanisa la mahali pamoja. Wachungaji wanaongea kama watu wa Mungu ni wao. Tuko mbali na maelezo ya Paulo katika **Mdo 20:28** ambapo anaonyesha ***"Kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe"***. Kwa wakati huu wachungaji wengi wameligawa kanisa katika kila mji na jiji kwa mashirika 'yao' wenyewe, wakijitwekea jukwa zao, wakitaka Mungu abariki maono yao wenyewe, kazi zao.

Yesu alisema tufanye wanafunzi

Kunaonekana kupuuza maagizo ya Yesu ya kufanya wanafunzi **(Mathayo 28:19-20),** na kuwainua wafanyi kazi kwa ajili ya mavuno **(Luka 10:1-2).** Makosa ya miondoko ya wamishonari katika Afrika na Asia ni kwamba walipanda makanisa ya kidini: hawakufanya wanafunzi. Baada ya wokovu waumini wapya wanahitaji kufundishwa neno la Mungu, sio kufundishwa katika miundo ya kanisa. Kazi kuu ya kanisa ni kufundisha, kufundisha, kufundisha katika kila zama, sio kwa saa moja kwa juma lakini kila siku katika hekalu na kutoka nyumba kwa nyumba **(Mdo 2:46-47, 19:9, 28:31).**

Haijalishi ni nafsi ngapi ambapo kanisa letu ama dini yetu ama huduma yetu inapata kwa BWANA, haitatimiza agizo la Yesu, kwa sababu maagizo ya Yesu huenda zaidi ya kuvuna nafsi kujaza viti katika majengo ya kanisa. Kuhubiri kwa injili katika utiifu wa maagizo ya Yesu inamaanisha zaidi ya kuwakusanya waliogeuka **(Mariko 16:15-16).** Kanisa la Yesu Kristo ni zaidi ya uinjilisti; ni ya kitume! ni ya kinabii! ni ya kichungaji! Uinjilisti wa umati uko kwa njia kubwa, lakini ni watu wangapi ambao hufanya maamuzi hufanyika wanafunzi.

Huduma ya kufundisha

Kanisa linatakiwa kufanya huduma ya kufundisha ambayo inabadilisha waumini wapya kuwa wanafunzi waliojipatiana, kila mmoja wao; kisha kuwaandaa kuenenda kuhubiri injili na kufanya wanafunzi! Tuendeleapo kufanya kujenga makanisa ya mahali pamoja ambapo waumini wamekusanyika pamoja, wamehubiriwa, wamefundishwa kwa sehemu, lakini hawajafundishwa na kuandaliwa kwa sababu ya huduma, hatutimizi maagizo wazi ya Yesu, na waumini hawatakua wawe watakatifu wa Mungu Aliye juu, wa umri, kurithi ufalme. Ufalme duniani ni urithi wetu lakini waumini wengi wamewekwa daima hawajakomaa kwa sababu ya miundo iliyopo. Kuna hali katika vikundi vya makanisa kusoma masomo yale yale mwaka baada ya mwingine, lakini hakuna kutuma nje, bila kupewa nafasi yoyote ya kufanya mazoezi ya mafundisho.

Watu wa Kitume katika Kitabu cha Matendo

"Siku ile kukatukia adha kuu ya kanisa lililokuwa katika Yerusalemu; wote wakatawanyika katika nchi ya Uyahudi na Samaria, isipokuwa hao mitume" **Mdo 8:1.** ***"Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno"*** **Mdo 8:4.**

Mdo 11:19 Inazungumzia watu wale wale "***Basi wale waliotawanyika kwa sababu ya ile dhiki iliyotukia kwa sababu ya Stefano, wakasafiri hata Foinike na Kipro na Antiokia, wasilihubiri lile neno ila kwa Wayahudi peke yao".*** Wote walikuwa wakihubiri neno. Walikuwa wanafunzi wa wale mitume kumi na wawili ambao kwa hakika walikuwa wamewafundisha vyema katika maagizo yote ya Yesu **(Mathayo 28:20).**

Wanafunzi ni mfano wa watakatifu ambao
wamerithi ufalme waMungu, wakienda kama
mabalozi wa ufalme, wakitembea katika
uhusiano kama wana.

"***Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho. Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu"*** **2Wakorintho 5:18-20.** Mungu ametukabithi hii huduma ya upananisho kwa kila mmoja wetu. Siku ya watakatifu ni wakati kila moja anaondoka akilihubiri neno, akiwa na uweza wa kusimama katika imani na saburi katika uso wa mateso, kusimama hata upinzani mkali unawajia watakatifu na kujaribu kuwashinda.

Neema ya Mungu ilionekana

"Lakini baadhi ya hao walikuwa watu wa Kipro na Kirene, nao walipofika Antiokia wakasema na Wayahudi wa Kiyunani, wakihubiri habari njema za Bwana Yesu. Mkono wa Bwana ukawa pamoja nao; watu wengi wakaamini, wakamwelekea Bwana. Habari hizo za watu hao zikafika masikioni mwa kanisa lililokuwako katika Yerusalemu; wakamtuma Barnaba, aende hata Antiokia. Naye, alipokwisha kufika na kuiona neema ya Mungu akafurahi, akawasihi wote waambatane na Bwana kwa kusudi la moyo" **Mdo 11:20-23.**
Neema ya Mungu ilionekana kazini. Neema ni nini? Twaweza kuiona, kuihisi, kuguzwa nayo. Inabadilisha maisha yetu. Neema inaweza kuguzika na matokeo kuonekana katika mtu akiwa mwepesi, akinyenyekea sana na wenye uwezo wa kuwapenda wengine. Injili inaenea kwa sababu ya neema ya Mungu kazini. Jamii ya wakristo inafanyika kikundi tofauti cha watu. Neema hii imepeanwa kwetu "***Katika Kristo Yesu tangu milele"*** **2 Timotheo 1:9.**

Shemazi anafanya kazi kama mwinjilisti

Mdo 8:5-40 inatuambia kuhusu huduma ya Filipo ya ajabu, ambayo iliguza mji wote **(aya 8)** na baadaye ikafikia ufalme wa Kushi kupitia towashi. Baada ya kuachana na towashi "***akahubiri injili katika miji yote, hata akafika Kaisaria"*** **aya 40.** Filipo alikuwa amewekwa wakfu kama shemazi katika **mdo 6,** lakini sasa anafanya kazi kama mwinjilisti. Huu ni mfano mwingine wa siku ya watakatifu: watu wa kawaida wakifanya mambo yasio ya kawaida.

Mwanafunzi fulani ambatiza mtume wa baadaye

Katika **Mdo 9,** mwanafunzi fulani Dameski aitwaye Anania anapokea maono. Bwana alimchagua ‘mwanafunzi fulani’ hakuwa mtume wala hakuwa na huduma yoyote lakini mwanafunzi. Ilikuwa ni mwanafunzi huyu ambaye Bwana alituma kumwekea atakayekuwa mtume Paulo baadaye, kumponya, kumbatiza na kuachilia Roho Mtakatifu kwake. Ni wakati wa wanafunzi kutiwa nguvu kumtumikia Bwana aliyefufuka Yesu Masihi. Katika **aya 17** alienda jia yake katika utiifu kwa maagizo ya Bwana, akamuekea mikono Sauli, akanena kiunabii juu yake, na akambatiza. Kanisa lilikuwa na amani; walijengwa na wakaongezeka **(aya 31).** Kwa nini? Kwa sababu mpinzani wao mkuu ameokolewa. Yesu alisema mapenzi yake yalikuwa kufanya mapenzi ya Baba. Tunatakiwa kumwamini yeye, kumngonjea kwa mikakati yake; ataitekeleza.

Kiriba kipya

Upepo mbaya unavuma kinyume cha miundo ya kanisa ya kidini kama vile imekuwa. Mungu amepeana kiriba kipya, kivuli kipya cha kanisa lake, mwili wa Yesu. Kiriba kipya haswa ni uhusiano wa kitume ambapo Mungu anarejesha akina baba na kuwainua wana; kivuli kipya ni neema ambayo inaachiliwa Mungu ainuapo akina baba na kupeana uwana kwa watakatifu. Kivuli hiki kipya ni katika uhakika sio kipya: ni kivuli cha Kristo; ni upako ambao Bwana wetu alipatia kanisa wakati alimtuma Roho Mtakatifu katika siku ya pentekosti kwa mitume ambao alikuwa amechagua na kuwafundisha.

Uhusianao wa baba na mwana sio tu wa viongozi lakini viongozi wanapopokea neema ya uwana, kisha watakatifu wengi wanapokea neema ya uwana. Watakatifu wanapoingia katika kutembea huku katika ukomavu, wanafanyika ‘akina baba’ kama katika **1Yohana 2:12-14** na akina baba wana watoto. Waliokomaa wanapatiana uangalizi wa baba na maelekezi na usalama wa uhusiano kwa waumini wote. Upendo unaongezeka ili watakatifu wote waje katika usalama katika wito wa Mungu. Kumekuwa na ukosefu wa akina baba kanisani; ukosefu wa viongozi wenye fadhili; kumekuwa na kutendwa vibaya na kufunzwa vibaya. Mabadiliko makali huja kwa ufunuo wa kufanyika wana na kupokea neema ambapo Mungu hufanya kazi kwa kila mtu binafsi, akizaa katika kiwango cha ndani ufunuo. Hii ndio hisia ya ‘kuja nyumbani kwa nyumba ya baba’.

Moyo kwa walio ‘kamili’

Bwana anafurahishwa tunapotembea katika utiifu kwa neno lake na ataachilia utukufu wake katika watu watiifu ambao wanampenda na kuendelea katika neno lake. Katika siku hizi Mungu anaunganisha pamoja wahuduma wenye nia moja na watakatifu ambao wana moyo wa walio ‘kamili’ (watakatifu wanaotembea katika ukomavu, wakikamilishwa katika utayari kwa kuja kwa Bwana).

Ni wakati wa kuumbwa kwa mahusiano ya ndani
kati ya watu wenye nia moja na Mungu anafanya
haya kwa kuunganisha watu kwa vikundi vya kitume ambapo
kila mtu anapokelewa; ambapo kila mtu ana usalama,
ana nidhamu na kuachiliwa atimize wito na
kusudi la Mung katika maisha yao binafsi.

Uthihirisho wa Utukufu wa Mungu

Ni wakati wa kuwa halisi kuhusu Yesu kuwa Yeye ni nani kwa hakika! Yeye ni nani halisi! Ni wakati wa kuwa halisi kuhusu asemayo katika neno lake! Ni nini anafanya ndani ya kanisa lake! Ni wakati wa Mungu kuwainua watakatifu na kuachilia kwao kuonyesha na kudhihilisha kwa yale ambayo yanakuja: utukufu halisi wa utukufu wa Mungu ukifunuliwa katika dunia yote; kuinuliwa kwa kanisa iliyojaa nuru na utukufu! **(Isaya 60:1-7).** "***Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake"*** **Yohana 14:21**. Ni kujidhihirisha kwa Yesu ndani ya watu wake.

Ni wakati

Ni wakati wa baraka za tumbo – mazao, wana wengi wakipatikana **(Filemoni 10).** Baraka za Yusufu ni wana wengi kuzaliwa.

Ni wakati wa baraka za maziwa - kulea { sio watoto, lakini wana wakikuzwa], kuwalisha na kuwaelekeza mitume wachanga, manabii, na kila mtakatifu ambaye anapata nafasi yake katika mwili na huduma zao zikionekana duniani! **(Mwanzo 49:25).** Huduma ya Yusufu ni ya kuwakuza wengine katika huduma.

Ni vyema na nafsi yangu! Kufanyika mwana ni kufikia kila kitu ambao ulitakiwa uwe ulipoubwa; kutanguliwa kujulikana, kupangwa mbele; kuja kutimizwa, kutimiza kusudi lako; kutengwa kutawala na kutamalaki na Kristo.

- Wewe si wa kawaida – lakini asiye wa kawaida!
- Wewe sio wa asili lakini asiye wa asili!

Ni wakati wa kusimama wima na mwenye nguvu katika Bwana – nguvu! Serekali itakuwa juu ya mabega yake! **(Isaya 9:6)** kuwa na nguvu! Kulihubiri neno la Mungu bila uoga ama kipendeleo! Yavute mabega yako nyuma; inua kichwa chako, tembea vizuri hapa duniani, ukitarajia kutawala katika milenia/miaka elfu kama mwana wa Mungu. Ni wakati wa kutembea katika mamlaka yake na neema yake – '*sisi hatuzimiki!'*

Neema ya MUNGU inapatikana kwa kila muumini!

Ni kulinganana kipimo cha karama ya Yesu. Kwa kuwapokea mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu ambao Kristo alipatiana katika kupaa kwake kanisani, tunapokea kipimo kamili ya neema ambayo Mungu amepatiana kupitia Kristo ili kanisa lije katika urithi wake **(Waefeso 4:7-16).**

Sasa ni wakati wa kumwomba Mungu akupe neema yake!
Sasa ni wakati wako wa kuwapokea mitume ambao Mungu anainua!

Wewe hauwezi kuzimika!

Kwa pamoja katika Injili hatuzimiki! Upako wa kitume umeachiliwa juu ya kanisa duniani kuleta urejesho, matengenezo na kuachilia kwa watakatifu [sio kubadilisha taasisi lakini kuachilia watakatifu katika uhuru wa Roho Mtakatifu kukua na kufanya kazi kikamilifu]. Watu watamjua Mungu wao na kufanya maajabu kwa sababu Kristo yuko ndani yetu, tumaini la utukufu **(Danieli 11:32)!** Sio vile tunafanya wenyewe lakini ni Kristo ndani yetu. Maandiko yanasema, "***Aliwapa uwezo [haki] wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake [jina la Bwana Yesu Kristo] waliozaliwa na Mungu"*** **Yohana 1:12-13.** Kuna jina moja tu

ambalo limepeanwa chini ya mbingu **Mdo 4:12**; hakuna jina lingine **Wafilipi 2:9-11**. Nguvu huja kupitia imani, kuamini jina la Yesu!

Sio kile tumefanya lakini ni kile tumefanyika ama tunafanyika.
Tunatakiwa kuwa tukikua na kugeuka kila wakati,
tukifanyika kile ambacho Mungu ametuwekea tuwe,
kufananishwa na mfano wa Mwana wake.

"Tena waokozi watakwea juu ya mlima Sayuni ili kuuhukumu mlima wa Esau; na huo ufalme utakuwa mali ya BWANA" **(Obadia 21).** Kristo atafunuliwa katika mwili wenye viungo vingi; Atafunuliwa kwa watakatifu wakati kila mmoja anafanya kazi ya huduma ambayo waliumbwa kuzifanya katika Kristo Yesu **(Waefeso 2:10).** Siku inakuja na sasa imefika wakati Kristo ataonekana ndani ya watu wake. "***Na ishara hizi zitafuatana na wale waaminio"*** **(Mariko 16:17-18).**

Kuitwa ili tumfuate YESU

Ni wakati wa kuondoka kutoka kwa taasisi, dini, na miundo ya ukristo wa kitamaduni. Ambacho kimeitwa kanisa ya wakati huu kwa upana haitambuliki kimaandiko. Neno *'kanisa'* katika maandiko inazungumzia 'wale ambao wameitwa kutoka ulimwengu kuwa watu wa Mungu'. Tunatakiwa kwenda ***"kutoka nje ya kambi, tukichukua shutumu lake"*** **Waebrania 13:13.** Wakristo wengi wanakaa kati ya yale wanajua na wanastarehe nayo. Hata kama dini zao zikiondoka nje ya mipaka ya maandiko, wangali wanabaki kwa mambo yasio wazi wakidhania kila jambo litakuwa sawa, bila kujua kwamba hukumu imekuja katika nyumba ya Mungu.

Katika Antiokia mara ya kwanza waliitwa Wakristo **(Mdo.11:26).** Katika mwaka wa 2001 hesabu ya watu Australia, 68% ya watu wa Australia walijiita wakristo. Sio lahisi kuwa wakristo kulingana na Agano Jipya! Wale waliokuwa Antiokia hawakuwa kitengo cha Wayahudi lakini sasa kusanyiko la waumini wakiwemo Wayahudi na Wayunani, wakiwa wamewekwa wakfu na injili, wakitabulishwa kweli kama wafuasi wa Yesu. Yesu mwenyewe "***akilitakasa na kulisafisha kanisa*** [wale walioitwa] ***kwa maji katika neno"*** **Waefeso 5:26.** Hili ni neno 'lililohuiswa/Rhema', neno ambalo linaleta imani **(Warumi 10:17).** Unasikia neno gani? Na je unalitii neno?

Ni wakati wa watakatifu kuchukua nafasi yao katika mwili na kuanza kufanya kazi katika karama walizopewa na kwa kushikilia mwili wote". Yesu lazima aonekane na kila mtu kupitia kanisa mwili wake. "***Na utukufu wa BWANA utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja; Kwa kuwa kinywa cha BWANA kimenena haya"*** **Isaya 40:5.** Mungu anawainua watakatifu wake duniani ili waonyeshe utukufu wake. Juma la Mitende makaribisho ya Yesu Yerusalemu, iliyonakiliwa katika maandiko, wakati ilichochea mji wote, alikuwa mpole wa kulinganishwa na kule kuingia kwenye ushindi kwa Mfalme akirudi mwisho wa nyakati.

"Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme,
chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu
wake Aliye juu; Ufalme wake ni ufalme
wa milele, na wote wenye mamlaka watamtumikia
na kumtii" **(Danieli 7:27).**

Ni watakatifu watakaorithi ufalme katika dunia.
Wakati kanisa linafanya kazi kikamilifu katika kutimiza maandiko,
Kisha …

"Na mataifa mengi watakwenda na kusema,

'Njoni, twende juu mlimani kwa BWANA,

Na nyumbani mwa Mungu wa Yakobo;

naye atatufundisha njia zake,

nasi tutakwenda katika mapito yake;

kwa maana katika Sayuni itatoka sheria,

na neno la BWANA litatoka Yerusalemu"

Mika 4:2.

Sura ya saba

KUTAWALA NA KUTAMALAKI NA KRISTO

Ufalme wa Mungu duniani – Mathayo 6:9-10 "*Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni"*

Kuzaliwa mara ya pili kuona na kuingia ufalme – Yohana 3:3, *5* *"Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufame wa Mungu. Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu".*

Kutawala katika uzima – Warumi 5:17b *"Zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki; watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo".*

Wafalme na makuhani – Ufunuo 1:5-6 *"Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, na kutufanya kuwa wafalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una yeye hata milele na milele".*
Ufunuo *5:10* *"Akatufanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi".*

Kwa miaka elfu moja – Ufunuo 20:4 "*Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya neno la Mungu ... nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu"*

Kutawala na kutamalaki na Kristo

Maandalizi ya mwisho ya kuja kwa Bwana ni kwa watakatifu waanze kutawala na kutamalaki katika Kristo sasa, ili wawe watumishi waliofaulu na watenda kazi na Yeye katika utawala wa umri ujao. Ushawai kufikiria kuhusu ni nini kingine katika mpango na kusudi la Mungu? Watakatifu wengi na wahuduma wameweka juhudi zao zote katika kuelewa kuja kwa Yesu mara ya pili. Na mawazo wanayoendana kama Kunyakuliwa na utawala wa Mpinga Kristo duniani wamejaza vitabu na wamejipatiana kwa mikutano mingi na mafundisho. Mawazo machache ama mafunzo yamepatianwa kwa uhakika na matarajio ya kizazi kijacho.

Kutawala na kutamalaki na Kristo imewekwa iwe ya hapa na sasa pia ni maandalizi ya watakatifu kuupokea ufalme hapa duniani ambao Mungu ameahidi na kutawala na kutamalaki na Kristo katika kuja kwake.

Mfano wa magugu

Katika **Mathayo 13:24-30**, Yesu anapeana mfano wa ngano na magugu na kisha kutoka **aya 36-43**, Yesu anatafsiri mfano huo. Ni mfano wa "*Ufalme wa mbinguni",* ambayo ni sawa na ufalme wa Mungu. Wakati mtu analinganisha maandiko, mtu anaona ya kwamba ufalme wa mbinguni katika Mathayo unaitwa ufalme wa Mungu katika Luka katika aya za kulinganisha. Wakati kunaweza kuwa na tofauti nzuri, kwa jumla maandiko yanasungumzia ufalme mmoja. Kuna ufalme mmoja tu.

Mbegu nzuri – wana wa ufalme – wamepandwa na Mwana wa Adamu katika dunia [konde], na magugu ni wana wa yule muovu, waliopandwa na ibilisi. Mavuno ni siku za mwisho na wavunaji ni malaika [wajube]. Hata kama vile magugu yalichomwa wakati wa mavuno, kwa hivyo mwisho wa nyakati Mwana wa Adamu atakusanya kutoka kwa ufalme wake vitu vyote vilivyo machukizo, na wale watendao maasi. ***"Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao"*** **Mathayo 13:43a.**

Ufalme wa Mungu ni ufalme halisi

Kama kulivyo na mafundisho mengi ya Bwana Yesu katika injili, katika mfano huu Yesu anaongea kuhusu ufalme hakika ukifunuliwa duniani. Wenye haki watabaki duniani.

Wana wa ufalme

Katika mwisho wa nyakati ufalme wa Mungu [mbinguni] utadhihirishwa duniani, ndani na kupitia watakatifu wenye haki ambao wamefikia ukomavu kikamilifu katika kukua kwao kiroho, wakiwa watiifu kwa Bwana, Mwana wa Adamu. Kwa kweli hawa ndio wana wa ufalme.

Ufalme wako uje

Katika ombi la Bwana Yesu alitufundisha wazi kuomba kwa matarajio ili ufalme wa Mungu uje duniani na mapenzi ya Mungu yatendeke hapa duniani kama ilivyo Mbinguni. Wakristo wengi wa kidini wameomba ombi hili kwa mamia ya miaka lakini ni wachache wameona uhakika wa ufalme ukija na ukiimarishwa hapa duniani. Hata hivyo, kwa hakika haya ndiyo mapenzi ya Mungu.

Kuvumilia katika dhiki

Wengi badala wanaomba kunyakuliwa kuje, wakiwa na matumaini kwamba wataondolewa duniani na kwa matarajio kwamba shetani ataimarisha ufalme wa mpinga Kristo duniani. Hii ni kinyume na mafundisho ya Bwana katika ombi na mifano. Hii pia ni vingumu kuiweka kwa watakatifu ambao wamekuwa wakipitia mateso mazito kwa makumi ya miaka, ikihusisha kufia imani, mikononi mwa serekali za mpinga Kristo leo.

Mapenzi ya Mungu duniani

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuomba. Akawaambia ***"salini hivi [kwa njia hii]"*** **Mathayo 6:9**. Tunatakiwa kuomba namna gani ufalme wa Mungu uje? Tutakiri kwa njia gani mapenzi ya Mungu duniani katika hali fulani, shinda za watu, mambo ya kijamii, hoja za kitaifa, majaga ya kimataifa? Kwanza ni kwa kuelewa kwamba injili ni injili ya ufalme wa Mungu; kwa njia ingine kuna mfalme ambaye ni Mungu na ana ufalme ambao anamiliki na ambao mapenzi yake yanatakiwa kutekelezwa. Kwa mfano, **Ufunuo 1:5** yasema ya kuwa Yesu ni ***"mkuu wa wafalme wa dunia".*** Hii inamaanisha kwamba Yesu ndiye mtawala wa Raisi Mugambe wa Zimbabwe; Yesu ndiye mtawala juu ya Raisi Bush na juu ya kila kiongozi mwingine wa kila

Taifa. Kwa hivyo tunaomba kwa mamlaka tunaposikia mambo ya mataifa, tukijua kwamba Tumuombaye ana mamlaka ya kusikia maombi yetu na kuyajibu.

Changamoto ingine ni kuomba mapenzi ya Mungu yatendeke kama jawabu ya mambo hayo mazito. Tunatambua aje mapenzi ya Mungu? Kiwazi, mapenzi ya Mungu yanafunuliwa kupitia neno la Mungu. Kote katika maandiko neno la Mungu linazungumzia mtu binafsi, jamii, taifa, mambo ya kimataifa. Kama wanafunzi wa neno, tunatarajiwa kulifahamu neno na kuwa na uwezo wa kuomba kwa mapenzi ya Mungu yatendeke hapa duniani kama ilivyo mbinguni.

Kanisa limetenganishwa na ufalme

Jambo moja ambalo limewakamata watakatifu katika utumwa kwa maono yaliofinyika ni hali ya kutokuwa na ufahamu wa asiri ya kweli ya kanisa. Katika historia kanisa limekuwa kama taasisi likiwa na nguvu za miundo na utekelezaji wa serekali zenye uhuru kutoka kwa ufalme wa Mungu. Kanisa halijahusishwa na ufalme na injili imekuwa injili ya wokovu ambayo watu wanaweza kuokoka kwayo na wawe sehemu ya kanisa lakini wasielewe maana ya ***"kuingia*** **kwenye** ***ufalme wa Mungu"*** **Yohana 3:5.**

Balozi wa ufalme

Kwa hakika kanisa ni balozi kwa pamoja wa ufalme! Kanisa limepewa huduma ya upatanisho kwa dunia **(2Wakorintho 5:19-20**). Yesu hakukusudia kanisa lake kuwa idara yenye uhai wake binafsi, kando na ufalme. Ufalme uko ndani ya Roho Mtakatifu **(Warumi 14:17)** na kanisa, kupitia watakatifu binafsi, na kupitia huduma ambazo Mungu amepatiana, wanatakiwa kuhubiri injili ya ufalme ili wengine wapate kusikia na kuzaliwa mara ya pili ili waingie katika ufalme. Hatujazaliwa mara ya pili kuingia kanisani, lakini kwa sababu kanisa limekosa ufahamu huo wa ufalme, tumehubiri injili ya ufalme tu na hatujafahamu mamlaka na utawala na ufalme wa Bwana wetu Yesu Kristo.

Kuja kwa Mfalme

Katika **Mathayo 23** Yesu anashtumu na kuleta katika kikomo miundo ya dini ya Kiyahudi na utendanji wa waandishi na Mafarisayo na kisha katika **Mathayo 24**, Anatuambia ishara za mwisho wa nyakati na kuja kwake. Moja wapo ya ishara ambayo lazima itimizwe kabla ya mwisho wa nyakati ni kuhubiriwa kwa injili ya ufalme "***katika ulimwengu wote, kama ushuhuda kwa mataifa yote"*** **aya 14.** Mfalme atakuja katika mazingira ya ulimwengu ulio tayari: Ufalme wa Mungu umehubiriwa kikamilifu. Kama injili ya ufalme ikihubiriwa ulimwenguni kote kama ushuhuda kwa mataifa yote, basi kila mwanadamu duniani atakuwa amesikia kumhusu Yesu Kristo na haki yake ya kutawala. Kila taifa litakuwa limeonywa kuhusu hukumu ambayo mataifa watapitia Yesu akija **(Mathayo 25:31-46).**

Chakula kwa wakati wake

Yesu anaongea mfano wa mtumwa mwaminifu na mwenye hekima akilinganisha mtumwa na yule mdhalimu. Yule mtumwa mwaminifu amewekwa juu ya nyumba ya Bwana wake **"*awape watu chakula kwa wakati wake"*** **Mathayo 24:45**. Kuna makanisa mengi leo ambao wamesahau kabisa onyo hii na sasa tuna tabia za kitaasisi zenye tabia ya dhambi katika nyumba ya Bwana. Vile vile, mafundisho mengi [chakula] yanayo patianwa katika makanisa mengi hayawaandai watakatifu kwa mwisho wa nyakati na kuja kwake.

Kupakwa na kuwa tayari

Katika **Mathayo 25** kuna mifano miwili na onyo za nguvu kuhusu hukumu ya mataifa, zote zikituhimiza kuwa tayari kwa kuja kwa mfalme. Mfano wa wanawali **(aya 1-13)** inapendekeza wote walimjua Kristo katika majira haya - walikuwa na ***'taa',*** lakini watano walikuwa na mafuta ya kutosha kuwawezesha kungojea hadi saa ya mwisho. Wapumbavu iliwapasa waondoke kutafuta mafuta yaliyofaa saa ya mwisho na walipitwa na kuja kwake. Kumbuka Bwana arusi yuaja! Watakatifu walio tayari, walioandalika na wanamngojea yeye wanaenda kwa arusi naye. Hawaenendi mahali pengine naye.

Kutumika kwa faida sasa

Mfano wa pili **(Mathayo 25:14-30)** unahusu mfalme wa ufalme akienenda katika nchi ya mbali, akiisha kuvigawa vitu vyake katika hali ya taranda. Kutakuwa na kumtambua ajapo vile watu walitumia taranda ambazo walipewa. Bwana anarudi, sio kuwaondoa watumishi wake mara moja, lakini kutoa hesabu ya vile waliendesha mambo ya ufalme wake wakati hakuwepo. Himizo ni wakati wa kurudi kwa mfalme, sio kwa kanisa kwenda.

Kuurithi ufalme duniani

Kisha Bwana anayaonya mataifa kuhusu hukumu ambayo wataipata. Yesu anatuhakikishia kwamba mwana wa Adamu atakuja ***"katika utukufu wake, na malaika watakatifu, wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake"*** **Mathayo 25:31.** Mataifa watakuja mbele zake kuhukumiwa. Hii inazungumzia mataifa duniani na watahukumiwa kulingana na vile waliwachukulia ***"ndugu"*** wa Yesu, hivyo ni wakristo. Walio haki – taifa za kondoo – ***"urithi ni ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu"*** **aya 34**. Ufalme huu umetayarishwa na Mungu ili ufanye kazi kikamilifu duniani.

Ni wakati wa kumfanya Yesu Mfalme

Ulikuwa ni wakati wa kufanya Daudi kuwa mfame juu ya Israeli

Katika kitabu cha mambo ya nyakati, tunasoma vile Daudi alifanyika mfalme juu ya Israeli. Jambo kuu katika kutendeka kwa haya ni kwamba baadhi ya viongozi ***"wenye akili za kujua nyakati".*** **"*Na wa wana wa Isakari, watu wenye akili za kujua nyakati, kuyajua yawapasayo Israeli wayatende, vichwa vyao walikuwa watu mia mbili na ndugu zao wote walikuwa chini ya amri yao"* 1Mambo ya nyakati 12:32.** Mazingira ya aya hii ni kwamba, baada ya kifo cha Sauli, Daudi alifanywa mfalme wa Yuda, ambayo ilikuwa ni kabira lake. Lakini mojawapo wa wana wa Sauli alikuwa ameuchukua ufalme badala ya Sauli. Hii haikuwa kulingana na mapenzi makamilifu ya Mungu. Mungu alitangaza hukumu juu ya Sauli na Daudi alikuwa amepakwa kuwa mfalme. Sasa ni miaka kumi na mitatu tangu Daudi apakwe kuwa mfalme. Ameshakuwa mfalme wa Yuda kwa miaka saba, lakini sasa ni wakati wa Daudi kufanyika Mfalme wa Israeli yote.

Ulikuwa ni wakati wa mabadiliko makubwa, wakati wa kihistoria, historia ikijiandika katika taifa la Israeli kulitimiza kusudi la Mungu. Ulikuwa ni wakati wa ufalme wa Mungu kujionyesha kupitia Daudi na taifa la Israeli.

Walikuwa na akili za kujua nyakati

Hawa wana wa Isakari **"*walikuwa na akili za kujua nyakati".*** Walikuwa wakisikiza sauti ya Mungu; walijua palikuwa na jambo ambalo lilikuwa litendeke na walijua **"*Waisraeli walitakiwa kufanya nini".*** Waisraeli wafanye nini kwa wakati huo? Ulikuwa ni wakati wa kumfanya Daudi Mfalme juu ya Israeli yote.

Ni wakati wetu wa kuzifahamu nyakati

Ni wakati wa kusikiliza Mungu: maombi ya kusikiza ni kutumia wakati mbele za Bwana, kujinyenyekesha mbele yake bila agenda na kumruhusu ajifunue na kusudi lake kwetu kupitia neno lake. Ni kumngonjea Bwana, kupokea kauli la Mungu, ambapo kazi zake kuu zitatokea. Tena kama kanisa linapotii mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa kusudi lake litaimarishwa.

Waisraeli wote wanaweza kuwakilisha kanisa lote na ni wakati wa kumfanya mtu mfalme leo. Ni wakati wa kumfanya Yesu mfalme!

Yesu amekuwa kuhani wa kanisa

Ukuhani wa Yesu wa kanisa umefunuliwa katika maombezi, maombi, ibada, uponyaji; nyakati nyingi nzuri zimejulikana katika uwepo wa Bwana. Lakini **Waebrania 3:1** inatuambia "***Mtafakarina sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu".*** Kwa miaka elfu moja mia nane Yesu amekuwa kuhani wa kanisa na kwa waumini, akipeana wokovu, msamaha, kusafisha na kila wakati akifichwa ndani ya vifungu vya kanisa.

Sasa anatakiwa kujulikana kama Mfalme

Wakati tunamtafakari Yesu kama Mtume tunasongea katika himaya ya upako wa mfalme. Yesu ni "***Kuhani kulingana na mpangilio wa Melkizedeki".*** Katika **Mwanzo 14:18-20** na **Waebrania 7:1-10** tunatabulishwa Melkizedeki, Mfalme wa haki na Mfalme wa Amani na Kuhani wa Mungu Aliye juu. Kutoka kitabu cha Mwanzo mpaka kitabu cha Ufunuo, tuna ufunuo wa Yesu kama Mfalme, Kuhani Mfalme.

Yeye ni Mfalme Kuhani

"*Maana ameshuhudiwa kwamba: 'wewe u kuhani milele Kwa mfano wa Melkizedeki'"* Waebrania 7:17. *Melkizedeki* ni mfalme na tena vile vile **"*Kuhani wa Mungu Aliye juu".*** Kwa hivyo Yesu ni Mfalme Kuhani milele. Huyu Milkizedeki hakuwa amefanyika kama mwanadamu; hakuwa na baba wala mama, hana mwanzo wa siku, wala mwisho wa uhai. Alifanyika kama Mwana wa Mungu. Yeye ndiye ambaye Ibrahimu baba wa Imani alimtolea fungu lake la kumi **(Waebrania 7:3-4).**

Yesu, mwana wa Daudi

Chini ya sheria za Musa kulikuwa na utofauti mkubwa kati ya huduma ya kikuhani na huduma ya kifalme. Mfalme Uzia alikiuka katika huduma ya ukuhani katika hekalu na akapigwa na ukoma kama matokeo **(2 Mambo ya Nyakati 26:16-21).** Hakuheshimu mgawanyiko wazi ambao Mungu alikuwa ameweka. Mfalme Daudi alikuwa tofauti ya kwamba alikuwa na kipindi spesheli cha neema kuhudumu kama nabii, kuhani na mfalme, akiwa mfano wa Kristo; lakini hata hivyo huduma yake ilikuwa ya kimsingi ilikuwa ya mfalme. Yesu ndiye anatakiwa kukalia enzi ya Daudi milele. Enzi ya Daudi kila mara ilimlika Yesu akitawala na kutamalaki kama Mfalme, na ufalme wa Mungu ukiimarishwa kikamilifu duniani.

Makuhani hutoa sadaka na wafalme wana mamlaka ya kutawala

Chini ya sheria wakati watu walipita mipaka iliyowekwa na Mungu ya huduma zao na wakatoa sadaka walihukumiwa. Mfalme Sauli hakumsubiri Samweli ambaye alikuwa kwa ofisi ya kuhani, kutoa sadaka mbele ya Mungu **(1Samweli 13).** Samweli alikuwa amechaguliwa kama kuhani kutoa sadaka. Wafalme walikuwa wamepakwa kutawala; walikuwa wamechaguliwa

kutumia mamlaka. Mara tu yule nabii kijana alimpaka Yehu kuwa mfalme juu ya Israeli, wakuu wa majeshi mara moja walitambua ufalme wake **(2 Wafalme 9:4-13).**

Kuhani atavikwa taji kama mtawala [mfalme]

"*Naam, pokea fedha na dhahabu, ukafanye taji, ukamvike kichwani Yoshua, mwana wa Yehosadaki, kuhani mkuu; ukamwambie, ukisema, BWANA wa majeshi asema hivi, ya kwamba, Tazama, mtu huyu ndiye ambaye jina lake ni Chipukizi; naye atakuwa katika mahali pake, naye atalijenga hekalu la BWANA. Naam, yeye atalijenga hekalu la BWANA; naye atachukua huo utukufu; ataketi akimiliki katika kiti chake cha enzi; na kutakuwa na kuhani katika kiti chake cha enzi; na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili"* Zakariah 6:11-13.

Hapa kuhani mkuu anavikwa taji kama mfalme! Huyu kuhani atalijenga hekalu la Bwana, kazi ya kitume, na kuuchukua utukufu. Wafalme haswa huuchukua utukufu. Ukuu ni wa wafalme. Yesu ni kuhani na mfalme, na analijenga kanisa, hekalu la Mungu, na ameubeba utukufu. Hataki tu tuhudumu kama makuhani lakini tutawale na kutamalaki na Yeye kama wafalme, na hivyo tuchukue utukufu Wake. Amewachagua mitume kuwaongoza watakatifu katika kujenga nyumba ya Mungu, kutimiza mwito wake wa kulijenga hekalu la Bwana. Kujenga nyumba ya Bwana ni kazi ya kifalme.

Zakaria ni mmoja wa manabii wa mwisho katika Agano la Kale na anaongea kuhusu mabadiliko kutoka kwa migawanyiko kati ya kuhani na mfalme chini ya Sheria kuja kwa urejesho wa mpangilio wa kwanza wa ukuhani ambao ni wa mpangilio wa Melkizedeki.

Katika Yesu Kristo, mpangilio wa Melkizedeki
umeimarishwa kikamilifu na sasa watakatifu wanaingia
katika urithi kutawala na kutamalaki kama wafalme.

Yesu ametufanya wafalme na makuhani

***"Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, na kutufanya kuwa wafalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele, Amina"* Ufunuo 1:5-6.**

Tanatakiwa kutawala kama wafalme

Sisi ni "***ukuhani wa kifalme"* 1 Petro 2:9.** Hiyo inamaanisha sisi ni wafalme na makuhani. Bwana anataka kutia nguvu mikono yetu leo katika ufalme, katika utawala. Ukuhani wa kifalme haumaanishi ukuhani ambao unatumikia wafalme lakini ukuhani wa mfano ule wa Bwana wetu Yesu: wa mpangilio wa Melkizedeki, mpangilio huu wa milele **(Waebrania 7:3)** unaonyeshwa. Katika Yesu Kristo mpangilio huu unatimilika kwa kanisa. Sio kwamba wengine ni makuhani katika kihuduma kwa Bwana, na wengine ni wafalme katika hali ya kutawala katika jamii kwa kiwango kikuu. Hapana!

Tumefanywa ukuhani wa kifalme
wa mpangilio wa Melkizedeki ambaye ndani yake kuna
"Shauli la amani kati ya hao wawili".

Watakatifu wote ni wafalme na makuhani

Wengine wamefundisha kimakosa kwamba kuna mugawanyiko kati ya wale wanahudumu kama makuhani, wakipendekeza huu ni wajibu wa kikundi cha wahuduma, na wale wanaohudumu katika biashara, wanasiasa na kadhalika katika jamii, wao wakiwa wafalme. Hakuna msingi wa kimaandiko kwa mambo kama hayo na fundisho hili baya linawakilisha vibaya mpangilio wa ukuhani ambao umefundishwa wazi katika maandiko. Ukuhani wa mpangilio wa Melkizedeki ulitangulia mpangilio wa ukuhani ule mwingine na wakipekee katika maandiko, hivyo ni, ukuhani wa Aroni. Mpangilio wa Melkizedeki sasa wazi umechukuwa nafasi ya mpangilio wa Aroni.

Jambo lingine tatanishi ambalo linatiliwa maanani na baadhi ya nakala za Biblia ambazo zinanukuu vibaya **Ufunuo 1:6** kusema Yesu ametufanya ***"ukuhani wa kifalme"***, inawanyima watakatifu nafasi ya ufalme, ambayo ni kutawala na kutamalaki katika Kristo Yesu. Ukuhani wa kifalme unamaanisha kwamba kila raiya katika ufalme ni kuhani anayetawaliwa na mfalme; hii inaonyesha kwamba nafasi tu ya wahuduma ya watakatifu ni kuhudumia Mfalme kama makuhani. Hii iko mbali na ukweli wa maandiko na kwa hakika ukweli usioeleweka wa makusudi ya Mungu kuwapatia watakatifu ufalme ambao wanatakiwa kuwa wakitawala na kutamalaki na Kristo sasa.

Ni watu wa namna gani waliokuja kumfanya Daudi mfalme?

Kwa kujifundisha tabia za watu ambao walikuja kumfanya Daudi mfalme tunaweza kuelewa watakatifu wanatakiwa kuwa watu wa namna gani kuingia katika maandalizi ya mwisho kwa kurudi kwa mfalme wetu, Bwana Yesu Kristo. Walikuwa watu waliojihami, watu wa vita. Katika historia ufalme uliimarishwa kupitia vita. **"*Na hizi ni hesabu za vichwa vya watu wenye silaha za vita, waliokuja Hebroni kwa Daudi, ili kumgeuzia ufalme wa Sauli, sawa sawa na neno la BWANA* 1Mambo ya Nyakati 12:23**. Katika nyakati za Agano la Kale ni wafalme ambao walikuwa wakiongoza jeshi katika vita; ambao waliongoza taifa katika vita dhidi ya adui.

Katika kuja kwa Daudi katika ufalme juu ya Waisraeli wote, serekali [ufalme] wa Mungu ulikuwa umepitia Waamuzi hadi kwa mfalme aliyechaguliwa na Mungu. Samueli mwamuzi wa mwisho, alikuwa amefanya kazi kama kuhani lakini sasa ni lazima kungekuwa na utofauti wa majukumu ya ukuhani na majukumu ya mfalme katika taifa.

Mashujaa wenye uwezo

Kabila zote walituma hesabu fulani ya watu wenye silaha kusaidia kilichokuwa kikitendeka lakini wana wa Isakari kila mwanaume alikuja; viongozi wao wote -200 walikuwa katika makubaliano, na ndugu zao wote walikuwa chini ya maagizo yao **(1 Mambo ya Nyakati 12:32).** Kabila lote lilikuja! Kabila lote walienda Hebroni kuandaa njia kwa ajili ya mfalme. Hata Yuda, kabila la Daudi, ni kikundi kindogo tu waliofika. Hesabu ya makuhani walifika, lakini kabila lote la Isakari walikuja kwa kuwa walikuwa watu wenye ufahamu wa nyakati! Walijua ambacho Israeli walitakiwa kufanya!

Tabia za makabila haya ya watu yaliyotajwa katika **1 Mambo ya Nyakati 12: 24-37** inaonyesha aina ya watakatifu ambao watainuliwa siku za mwisho. Watu hawa walikuwa wamejihami kwa vita; walikuwa mashujaa wenye nguvu waliojiandaa kwa ajili ya vita. Sadoki anaitwa shujaa mwenye nguvu **(aya 28);** watu wa Efraimu walikuwa shujaa wenye nguvu. Walikuja na silaha za vita; walikuwa watu wenye mioyo migumu ambao waliweka cheo; waliweka malezi ya vita; walikuwa wamejihami na kila aina ya silaha kwa ajili ya vita. Walikaribia watu 350,000 wa vita waliokusanyika. Hawa ni zaidi ya watu waliokusanyika kuenenda katika Iraq mwaka wa 2003.

Kanisa la kitume linampokea Yesu kama Mfalme

Katika kanisa leo kuna watu wanaitwa mitume, ambao wanajua kanisa linapaswa kufanya nini. Mungu anainua vikundi vya kitume ambao wanapatia kanisa uongozi ili kuja kumfanya Yesu kuwa mfalme. Ujumbe huu wa kitume unaenda kote katika mataifa. Mungu anaunganisha watu muhimu pamoja katika uhusiano wa kujipatiana na kunyenyekeana. Mwondoko wote wa kanisa unapokea ujumbe wa kitume na wanaleta mabadiliko ili kanisa la kimaandiko lionekane kikamilifu.

Tabia za watakatifu wa Siku za mwisho

Sifa muhimu za watu hawa zimetamatishwa katika **aya 38** "***Hao wote, watu wa vita, askari wastadi, wakaja Hebroni wenye moyo mkamilifu, ili kumtawaza Daudi awe mfalme juu ya Israeli wote; tena wote waliosalia wa Israeli nao walikuwa na moyo mmoja kwamba wamtawaze Daudi".*** Sifa hizi lazima zionekane katika kanisa la siku za Mwisho.

Ni wakati ambapo kanisa litafanyika kanisa la kijeshi, likiwa kwenye mpangilio, wakitambua uongozi wa kitume ambao Bwana anaweka, wakijipatiana kwa yale ambayo Mungu anafanya na kumpokea Yesu kama Mfalme, ambapo watakatifu watakuwa tayari kuupokea ufalme.

i. WATU WA VITA

Watu hawa walikuwa wamejihami na wenye ujuzi. Sisi pia tuko katika vita na tunatakiwa kujihami na kuwa na ujuzi wa kuzitumia silaha zetu. "***Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi wa pepo wabaya katika ulimwengu wa roho"*** **Waefeso 6:12.**

Tabua wito wa kujihami kikamilifu, ikiwezeza kanisa kusimama kinyume cha nguvu za shetani, inakuja katika **Waefeso 6.** Sura za kwanza tano za waefeso, zinatwambia vile tunastahili kuwa tayari na kuandaliwa kwa vita hiyo kubwa.

Silaha zetu ni gani?

Waefeso 6:14-18 inaelezea silaha ambazo zinapatikana kwa mkristo na zinatakiwa "*kuvaliwa".*

- **Mshipi wa kweli:** ukweli ni neno la Mungu kulingana na Yesu: "***neno lako ndiyo kweli"*** **Yohana 17:17.** Petro anatuagiza "***vifungeni viuno vya nia zenu"*** na kweli **(1Petro 1:13).** Mshipi wa kweli kama sehemu ya silaha inahusu kulipokea neno la Mungu katika nia zetu na kuweka mawazo yetu juu ya neno la Mungu.
- **Dirii ya haki:** inafunika moyo; tunatakiwa kuamini ukweli wa neno katika moyo. "***kwa moyo mtu huamini na kuhesabiwa haki"*** **Warumi 10:10.** Tunapaswa kuamini ukweli katika mioyo yetu na tuifahamu kweli katika nia zetu.
- **Viatu vya injili ya amani:** Inaongea habari ya kutembea kwetu. Mara tumesikia kweli na kuamini katika roho zetu, tunatakiwa kutembea katika kweli hiyo.
- **Ngao ya imani:** kutumia imani na kutambua mishale mikali; inashughulikia shaka za mawazo. Kumbuka imani huja kwa kusikia neno "***neno linalotoka katika kinywa cha Mungu"*** **Mathayo 4:4***;* hilo ndilo neno ambalo latakiwa kusikilizwa ili liachilie imani katika maisha ya waumini **(Warumi 10:17).**
- **Chepeo cha wokovu:** kupata kuzamishwa katika neno la Mungu kuelewa mafundisho ya neno. Kichwa kinawakilisha mamlaka; inawakilisha maamuzi. Kuvaa chepeo ya wokovu inamaanisha kwamba utafanya maamuzi kulingana na neno la Mungu, kwa kuwa neno la Mungu linadumu ndani yetu.

- **Upanga wa Roho:** kutumia neno la Mungu kumshinda shetani, kama vile Yesu alifanya jangwani **(Mathayo 4:1-11).** Hii ni neno litokalo katika kinywa cha Mungu, huja kwa nguvu na kuachilia imani.

Vita zetu ni gani?

"Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; (maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;) tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo; tena tukiwa tayari kupatiliza maasi yote; kutii kwenu kutakapotimia" **2Wakorintho 10:3-6.**

Mungu anataka tuwe 'watu wa vita', tukiwa na ujuzi wa kuzitumia silaha zetu, tukijua kuangusha ngome. **"*Wakati kutii kwetu kutatimia",*** tunatakiwa ***"kuadhibu kila maasi".*** Haya sio yale kanisa inafanya kwa wakati huu. Hatutembei katika utiifu wala kukabiliana na maasi yaliyo tuzunguka. Wala hatuishi ndani ama kuhubiri kikamilifu ufalme wa Mungu.

Ushindi katika Vita

"***Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana – Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa"*** **Ufunuo 12:11.** Watakatifu wanastahili kushinda! Wanastahili kumshida shetani! Ushindi ni kwa watakaoshinda!

ii. WALIJUA KUWEKA CHEO

Walijua sehemu yao, na waliwajua viongozi wao. Tunapaswa kujua sehemu yetu [cheo] katika mwili wa Kristo, tuwe salama mahali pale na tusitoke hapo! Jengo la mwili wa Kristo, kanisa, halina viwango, lakini kuna mpangilio. Mungu ameuweka mwili wake katika mpangilio. "***Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka"*** **1Wakorintho 12:18.** Mungu ameweka kila kiungo katika mwili na kila kiungo kinatakiwa kufanya kazi kikamilifu katika mahali ambapo Mungu amepeana. Kwa hivyo, ni ujinga kufikiri kidole cha mguu kujaribu kuwa shingo ama kinyume chake.

Yesu ameandaa mahali pa kila mmoja

Yesu alizungumza kuhusu kuwekwa ama mahali pa kudumu katika **Yohana 14:2**. Msitari huu umekuwa haueleweki na umetumiwa nje ya mahali pake na watu wameota wakiwa na nyumba ya mtu tajiri mbinguni.

> Neno la Kiyunani ni SC #3438 '*mone' kutoka 3036 ambayo inazungumzia 'kudumu'; mone inamaanisha 'mahali pa kudumu' kwa mfano 'makao' [kitendo cha kudumu ama mahali pa kukaa].* Neno hili limetumika tu mara mbili katika Agano Jipya: katika **Yohana 14:2** kama '*mansion'* na katika **Yohana 14:23** kama '*abode',* katika biblia ya King James. Pia imetafsiriwa 'mahali pa kudumu' katika tafsiri zingine.

Yesu ameandaa mahali kwako na kwangu; mahali ambapo ni petu; mahali ambapo tunatoshereka na tunaweza kufanya kazi. La kusikitisha, wakati ambao umepita wengi wetu wamezaliwa mara ya pili kuwa yatima, watoto bila baba. Matokeo yamekuwa ni mwili mzima wa watu wasiounganishwa na kushikamanishwa, na kwa hivyo hawawezi kufanya kazi, hawawezi kukua katika yote ambayo Mungu ametupangia kila mmoja, kwa sababu hatujafika mahali ambapo Yesu amatuandalia.

Huduma zilizowekwa

"Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha" **1 Wakorintho 12:28.** Kuna mpangilio pia katika huduma zilizowekwa ambazo zinafanya kazi katika uongozi kanisani. Mpangilio huu ulio wazi umebadilishwa katika historia ya kanisa kwa mipangilio mingine kulingana na mifumo ya wanadamu, sio kulingana na neno la Mungu. Kama matokeo, sehemu kubwa ya kanisa iko nje ya mpangilio na haifanyi kazi vizuri.

Mpangilio katika kanisa la mahali pamoja

"*Maana nijapokuwa sipo kwa mwili, lakini nipo pamoja nanyi kwa roho, nikifurahi na kuuona utaratibu wenu na udhabiti wa imani yenu katika Kristo"* **Wakolosai 2:5.** Kanisa linarejeshwa tena katika mpangilio mwema kuiwezesha kufanya kazi. Mpangilio huu hauendani na shirika la taasisi lakini msingi wake ni "kuimarika katika imani ndani ya Kristo" na uhusiano na mtume ambaye Yesu ameweka kwa kanisa la mahali pamoja, wakiwepo wazee katika kanisa la mahali pamoja [kwa kusema kanisa la mahali pamoja ninamaanisha kanisa la mji ama jiji yakiwemo mashirika mbali mbali].

Mpangilio katika Meza ya Bwana

"*Mtu akiwa na njaa, na ale nyumbani kwake; msipate kukutanika kwa hukumu. Na hayo yaliyosalia nijapo nitayatengeneza"* **1 Wakorintho 11:34.** Kunapaswa kuwa na mpangilio katika meza ya Bwana

Mpangilio katika ujuzi wa kimsingi

Kuna mpangilio katika ujuzi wa kimsingi wa imani: Petro alisema "***tubuni mkabatizwe… na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"*** **Mdo 2:38;** Yesu alisema "***fanya wanafunzi katika kila taifa, mkiwabatiza … na kuwafundisha"*** **Mathayo 28:19-20.** Kanisa limepuuza mpangilio uliotolewa katika sehemu nyingi katika maandiko; kwa mfano, makanisa mengi yamesisitiza kuwafundisha waumini wapya kikamilifu kabla ya kuwabatiza – huo sio mpangilio mwema! Mpangilio ni sawa na muundo. Mungu alimuagiza Musa kujenga hema ya makutano kama vile alivyokuwa ameonyeshwa. Mtume Paulo aliweka mpangilio na muundo wa kanisa la Agano Jipya na kumekuwa na viongozi wa kanisa la sasa ambao wametii kujenga kulingana na muundo.

Kulikuwa na mpangilio wa makuhani

Katika **Waebrania 5, 6 &7** mpangilio wa Melikizedeki unatajwa mara kadhaa na mpangilio wa Aroni mara moja. Katika **Luka 1:8** Zakaria alikuwa akihudumu katika Hekalu. Alikuwa ni kuhani katika *'taratibu ya zamu'.* Hata kama vile kulikuwa na mpangilio na taratibu za zamu katika ukuhani hivyo kuna mpangilio na taratibu katika uongozi wa huduma ya kanisa leo. Hata hivyo kanisa lililopangwa kitaasisi linakwepa na kupuuza mipangilio hii na taratibu ambayo Roho anataka kuimarisha.

iii. WALIKUJA HEBRONI.

Walijua mahali pa kukutanika; walijua mahali pa kuja. Hebroni palikuwa ni mahali pa kihistoria katika hitoria ya Israeli. Ibrahimu aliishi kwa muda katika eneo hilo. Ingekuwa ni mahali pa muhimu ambapo Ibrahimu alitembea katika nchi. Walitambua kwamba mabadiliko yalikuwa karibu kutendeka na walitaka kuwa sehemu yake. Mioyo yao iliambatana na yale

Mungu alikuwa akitenda. Kwa hivyo wakakusanyika kwa kusudi moja. Mungu alikuwa ameandaa mioyo yao na walitaka kuwekwa wawe tayari kwa yale Mungu alitaka watende.

Hebroni ndipo mtu wa Mungu alikuwa

Tayari Daudi alikuwa anaishi Hebroni. Alikuwa amekusudiwa kuwa mfalme katika Sayuni lakini kulikuwa hakuna mtu aliyetambua hayo bado.

Walikuja mahali ambapo mamlaka yaliyopakwa ya Mungu yalikuwa yamewekwa na kufanya kazi. Mamlaka ya Mungu yaliyopakwa yanaakilisha upako wa kifalme. Mungu ainuapo mitume leo na watakatifu wanaanza kukusanyika kwa mtume ili wawekwe kwenye mpangilio ili kufanya kazi kikamilifu, upako huu wa kifalme unaachiliwa.

Ni wakati ambapo watakatifu wanaanza kufanya kazi katika upako wa kifalme wa Yesu Kristo ambapo kutakuwa na matayarisho halisi ya kuja kwa Mfalme Yesu. Neno la Mungu linaahidi kwamba tutatawala na kutamalaki duniani na kwamba ufalme utapatianwa kwao. Yesu haji kuwaokoa 'kikundi kilicho na mawazo ya mbinguni cha 'kikuhani' na kuwapeleka mbinguni. Anakuja kama Mfalme wa Ufalme ambao tayari unafanya kazi duniani kupitia watakatifu ambao wanatawala na kutamalaki. Wakristo wanatakiwa kuinuka duniani, wakitembea katika haki katika kila eneo ya maisha. Wakristo hawatakiwi kuwa mafarisayo wakiamua kila kitu kama sheria lakini wanatakiwa kutawala na kutamalaki katika maisha. Ni wakati wa kuinuka kwa wakristo juu ya ufisadi ambao uko duniani na ambao unakuja kinyume cha wakristo kwa kila mabadiliko.

iv. KWA MOYO MWAMINIFU

Watu hawa walikuwa wamejipatiana. Walikuwa waaminifu na wakutegemewa. Walikuwa wameandalika kuwa waaminifu kwa yule ambaye Mungu alikuwa amechagua na kuinua. Tunatakiwa kukuza mioyo ya uaminifu. Hata hivyo uaminifu wao ulikuwa kwanza kwa Mungu. Hii ndio sababu walikuja Hebroni – mioyo yao ilikuwa na uaminifu kwa Mungu.

Uaminifu

Swali la uaminifu linahitaji kuchunguzwa kwa makini. Leo watakatifu wengi wamebakia kwa dini kwa sababu ya uaminifu. Kwa miaka kadha baada ya kifo cha Sauli makabila yote ila Yuda walibaki waaminifu kwa ufalme wa Sauli hata kama Mungu alikuwa amemalizana na ufalme wa sauli. Mungu alikuwa amesonga mbele. Dini zimekuwa na mianzo ya kihistoria iliyokubalika lakini haikuwa idumu milele. Kwa sababu mianzo yake haiko katika maadiko wala haitakuweko mwisho. Yesu atakuja kwa kanisa lake. Tunaitwa kutoka kwa mashirika, dini na mengineo. Kila muumini na kila ushirika wanastahili kuendana na neno la Mungu. Wakati tunaliweka neno la Mungu kwanza, uaminifu wetu utabadilika. Hatustahili kuendelea kuaminika kwa kitu ambacho Mungu ametuita tutoke kwake.

Yoshua na watu walitakiwa kusonga mbele

Mungu alisema katika **Joshua 1:2**, ***"Musa mtumishi wangu amekufa; haya basi, ondoka".*** Hata kama vile Musa alivyo kuwa mkuu, alikufa. Yoshua na watu wa Mungu walikuwa waondoke. Makanisa za kidini na miondoko zina kipindi cha maisha lakini Mungu ni wa milele. Ni wakati wa kuondoka na kwenda na Yesu.

Kujipatiana kwa Yonathani kwa Sauli ilimaanisha kifo

Mwana wa Sauli alifanya maagano na Daudi. Alitambua kwamba Daudi alikuwa ni mpakwa mafuta wa Mungu na yule aliyechaguliwa na Mungu kuwa mfame aliyefuata. Lakini

kasoro baya ni kwamba hakuweza kujitenganisha na mpangilio wa zamani na hii ilimgharimu maisha yake. Alijua mpangilio mpya ulikuwa upi, na pia alijua kila ambacho Mungu alikuwa akitenda kupitia Daudi, lakini aliamua kuendelea kubaki mwaminifu kwa mfumo wa kale na uaminifu pasipofaa.

Leo mpangilio mpya ambao unainuka ni kanisa la kitume, isio ya taasisi, kanisa lenye msingi wa mahusiano, ambayo ina maono kwa mwili wote wa kristo ukiinuliwa; likiwa tayari kwa kuja kwa Bwana; likiisha kuhubiri injili duniani kote.

v. KUMFANYA DAUDI MFALME

Watu hawa walijua Israeli walipaswa kufanya nini. Walikuwa wakijua nyakati na maelfu walijiunga nao kutoka kwa makabila mengine kumfanya Daudi mfalme. Israeli yote walikubaliana na yale ambayo yalikuwa yakitendeka na **"*wote wakawa na moyo mkamilifu*" 1 Nyakati 12:38**. Hawangefikia mapatano hayo kama wana wa Isakari na wengine hawangejitokeza. Na hata kabla ya wana wa Isakari na wengine kutokea, kikundi kidogo cha wanaume na jamii zao walikuwa wamejitokeza mapema kuwa na Daudi na kusimama naye njangwani kwa miaka **(1Samueli 22:1-5).**

Kanisa lote walikubaliana!

Katika **Mdo 2:1** wakati waumini wote walikuwa wamekusanyika mahali pamoja, ***'kwa kauli moja'***, kisha Roho Mtakatifu akaja. Wale wanafunzi mia na ishirini walikuwa wametokea kwa utiifu kwa Yesu; walikuwa wamejitenga kikamilifu kwa kusudi la Bwana. Kulikuwa na umoja wa moyo na nia miongoni mwa waumini katika kanisa la kwanza. Walikuwa katika makubaliano. Yesu aliwaaminia hatima ya kanisa lake na ufalme wa Mungu duniani kwa kikundi hiki cha watu. Mungu anaangalia watu ambao wako umoja katika moyo na nia kulitimiza kusudi lake kwa kanisa la siku za mwisho.

Yesu yuaja kama Mfalme

Muabudu Yesu, mfanye mfalme! Yesu ni mfalme na kuhani; Anaokoa, anaponya. Kanisa linamhubiri Yesu kama Kuhani sio kama Mfalme Kuhani. Watu wengi wanafahamu huduma ya kikuhani ya Yesu na wanatembea kama makuhani. Huduma ya ukuhani inaleta wokovu na uponyaji. Tunafurahia huduma ya kikuhani na ni vyepesi kuwa kuhani kuliko kuwa mfalme.

Makuhani wanaabudu na kuhudumu na kutoa sadaka.
Wafalme wanaeneda kwa vita! Wafame wanatawala na kutamalaki!
Wafme wanauchukua utukufu!

Mungu anainua uongozi mpya

Mitume wanainuliwa wauchukue uongozi kanisani. Mungu aliweka katika mwili, wa kwanza mitume. "***Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi"* Mathayo 28:18.** Yesu alikuwa na mamlaka yote na akapatiana mamlaka hayo kwa wanafunzi wake: mamlaka juu ya maroho ya mapepo; mamlaka juu ya magonjwa; mamlaka ya ***"kufanya kazi kubwa"* Yohana 14:12**. Ni wafalme walio na mamlaka sio makuhani.

Injili ya ufalme wa Mungu

Tunatakiwa kuhubiri injili ya ufalme wa Mungu. Wakati Filipo alipoenda Samaria, "***Akazihubiri habari njema za ufalme wa Mungu"*** na wengi wakaamini na wakabatizwa **(Mdo**

8:12). Wengi wanahubiri injili ya wokovu, wakihimiza sadaka za kikuhani za Yesu kwa ajili ya dhambi. Injili ya ufalme inahimiza utawala wa Masihi. Yeye ndiye ***"Mkuu wa wafalme wa dunia"*** **Ufunuo 1:5.**

Ni nini kitatendeka Yesu akirudi?

Ni wakati wa kumfanya Yesu mfalme! Ni wakati wa kuwakusanya watu wa vita: ambao wanaweza kuweka zamu! Ambao wanazifahamu nyakati ambazo tumo ndani yake! Ambao watakuwa na moyo mmoja na nia moja kumfanya YESU MFALME! Tunatakiwa kutawala na kutamalaki naye duniani. Wakati Yesu anakuja, atakuja kwa ufalme ulioandalika na unafanya kazi.

Kanisa ni balozi wa Ufalme wa Mungu

Ni wakati wetu, kanisa, wa kutubu, kubadirisha mawazo yetu kuhusu kanisa ni nani na ni nini. Kanisa linatakiwa kuwa balozo wa ufalme wa Mungu, likiwa limetumwa naye kumwakilisha na kuwakilisha ufalme wa Mungu kupitia kuhubiri injili iliyo kamilifu na iliyojawa na Roho.

Kuhubiri ufalme wa Mungu

Ufalme wa Mungu ulikuwa ***"umekaribia"*** wakati Yohana mbatizaji alianza kuhubiri. Yesu mwenyewe alikuja akihubiri "***ufalme wa Mungu umekaribia".*** Wakati Yesu aliwatuma wale sabini katika **Luka 10**, aliwaambia kwamba wakiisha kuwaponya wagonjwa katika nyumba walipopokelewa, walikuwa wawaambie "***ufalme wa Mungu umewakaribia"*** **aya 9**. Tangu wakati huo tumeamuriwa kuhubiri ufalme wa Mungu, tukiandaa ulimwengu na watu ambao wanaishi humo kwa kuja kwa mfalme.

Ufalme wa Mungu utashinda

"Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema,
Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake,
naye atamiliki hata milele na milele" **Ufunuo 11:15**

Watakatifu ambao watashinda mnyama watatawala na kumiliki na Kristo

"Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikono yao; nao wakawa hai;
wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu" **Ufunuo 20:4.**

HITIMISHO

Kuzaliwa mara ya pili

Baada ya mwanamke kukutana na Yesu kisimani katika **Yohanna 4,** alienda mjini, akiisha kubadilishwa kupitia kukutana kwake na Yesu na akaambia watu wengi kumhusu huyu ambaye alikuwa amekutana naye. Biblia inasema wengi wakaanza kumuamini Yesu kwa sababu ya yale alioyasema lakini wakati walienda wakakutana na Yesu wenyewe nao wakasema "***sasa tunaamini, wala si kwa sababu ya maneno yako tu; maana sisi tumesikia wenyewe, tena twajua ya kuwa hakika huyu ndiye Mwokozi wa ulimwengu"*** **aya 42**. Kila mmoja anahitaji ujuzi wa kibinafsi wa kukutana na Yesu, ambao ni kuzaliwa mara ya pili.

Kupokea Roho Mtakatifu

Baada ya Filipo kuhubiri Samaria kwa kufaulu katika **Mdo 8**, Biblia inasema waume wengi na wake waliamini na wakabatizwa. Hata hivyo hawakuwa wamepokea Roho Mtakatifu. Mitume Petro na Yohana wakashuka kutoka Yerusalemu na wakaweka mikono juu ya waumini hao wapya nao wakapokea Roho Mtakatifu. Kila mmoja anahitaji ujuzi wa Roho Mtakatifu; ujuzi wa nguvu za Mungu ambazo zinawezesha muumini kushuhudia Yesu na injili.
Vivyo hivyo katika Efeso katika **Mdo 19**, baada ya Paulo kuhubiri Yesu kwa kikundi cha wanafunzi ambao walijua tu mafundisho ya ubatizo wa Yohana, walibatizwa katika jina la Yesu. Wakazaliwa mara ya pili na wakabatizwa. Kisha Paulo akaweka mikono yake juu yao na wakapokea Roho Mtakatifu. Tunajua walikuwa na ujuzi wa kibinafsi wa Roho Mtakatifu kwa sababu walikuwa wakizungumza kwa ndimi na kutabiri.

Kufanyika mwana

Mnamo oktoba 31 mwaka wa 2002 nilipata ujuzi wa kibinafsi ambao tu ninaweza kueleza kimaandiko 'kufanyika mwana'; kuingia katika ukomavu; kujua usalama mkuu ya kwamba uliyafikia maisha yangu. Njia ya kueleza marafiki zangu ilikuwa, 'nimefika nyumbani' na kuja nyumbani huko ni kwa 'nyumba ya baba'. Kuna ujuzi mwingine wa waumini wote mara umeokoka na umepokea Roho Mtakatifu. Ujuzi huu unakuja katika umri wa ukomavu; ni ujuzi wa kuingia katika uwana na uwana huingiwa na kila mtu. Ni kupokea Roho wa kufanywa wana hivyo ni, kuwekwa mahali pako kama mwana kupokea urithi.

Uhakika wa uwana

Uhakika wa uwana ni uhusiano wa ndani na Yesu Kristo. Ujuzi wa uwana ni ufunuo mkuu na wa ndani wa utu wa Bwana Yesu Kristo, ambaye kupitia ndani yake ambapo Baba Mungu anafunuliwa. Waumini wengi wakati ni wachanga katika Bwana wanadhania ya kwamba siku moja watakutana na Baba kama watakutana na mtu mwingine tofauti na Yesu. Hata hivyo wakati mtu ana ufunuo wa uwana, Mungu kama Baba anafunuliwa kwake katika Kristo Yesu. Yesu na Baba ni umoja.

Wakati tunarudi kukiri maandiko **"*mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenyu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote"*** **Waefeso 4:4-6**. Yawezekana aje Mungu mmoja na Baba kuwa ndani yetu, na juu ya yote na katika yote? Ni kupitia ufunuo wa **"*Kristo ndani yetu tumaini la utukufu"*** **Wakolosai 1:27** na Kristo yuko ndani yetu kwa uwezo wa Roho mmoja.

Yesu mwenyewe ananukuu kutoka kitabu cha kumbukumbu la torati, akidhibitisha ya kwamba Mungu aliye Bwana ni mmoja. **"*Yesu akamjibu, Ya kwanza ndiyo hii, Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote"* Mariko 12:29-30**. Ujuzi wa uwana unaleta ujuzi wa ndani wa Mungu: Yeye ni Baba ambaye anajulikana kupitia mwana kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Kutembea katika urithi wetu

Kuingia katika pumziko la Mungu katika **Waebrania 3-4** inalinganishwa na kuingia kwenye nchi katika asili. Kuingia katika pumziko la Mungu ni dhawabu na hali ya wale wanaotembea katika urithi wao; ambao "***wamepumzika kutoka kwa kazi zao"* Waebrania 4:10**. Wale wetu ambao wameingia katika ujuzi wa kufanyika wana wamepata ujuzi wa pumziko hii; tumeziacha kazi zetu; ile hali ya kuendeshwa imetuacha; kulazimishwa kuhudumu na kufanyia Mungu kazi kwa bidii imeondolewa kikamilifu. Sasa tunaweza kutumika kama wana tukijua ya kwamba sisi ni wa nyumbani; ambao tunajua tunahitaji tu kuzifanya kazi ambazo Baba alitangulia kutuwekea.

Kufanya kazi za Baba

Yesu alisema **"*ninafanya kazi ambazo ninaona baba akizifanya; ninaongea abacho baba ananiambia".*** Ni sawa kwetu sisi leo: Yesu anataka tufanye kile anachotuambia. Anatuambia ya kwamba tukitii maagizo yake, **"*nami nitampenda na kujithihirisha kwake"* Yohana 14:21** na tukiliweka neno lake, **"*Na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake"* Yohana 14:23**.

Sasa ni wakati

Tusiwe watoto tena **(Waefeso 4:14)** lakini sisi ni wana, waliokomaa ambao Baba amewapa urudi **(Waebrania 12:5-9),** ambao wamepokea hekima ya ndani ya neno ambayo ni siri **(1 Wakorintho 2:6-7).** Wito wa Mungu juu ya kanisa lake leo ni 'kukua'. Ni wakati ***"ulioamuriwa na Baba"* Wagalatia 4:2** kwa warithi ambao wamekuwa watoto sasa kama vijana ambao wamefikia umri wa ukomavu. Ukomavu sio jambo ambalo tunaweza kufikia kwa kazi lakini ni kwa imani na kwa imani **"*nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu"* Wafilipi 3:12.** Paulo anasema kwamba tunaweza kuwa na mawazo yaliokomaa na kwa hivyo **"*na tuenende katika lilo hilo"*** na **"*tuwaze hayo"* aya 14-17.**

Matokeo itakuwa kikundi cha wandugu wakitembea katika ukomavu, wakitembea katika uhusiano wa kitume na wakiwa watu kielelezo cha wengine kufuata **(Wafilipi 3:17).**

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe na mioyo yenu
mnapotafuta kuyaelewa mambo haya.

OMBI AMBALO UNAWEZA KUOMBA

Kuingia katika uwana: ujuzi wa mageuzi

Lifuatalo ni **ombi** ambalo unaweza kuomba, ukiamini Mungu adhibitishe mapenzi yake katika maisha yako kupitia ujuzi wa mabadiliko.

Baba wa mbinguni, ninakuomba uniongoze kwa neema yako na kwa Roho wako Mtakatifu kuelewa na kuingia katika hali ya kuwa mwana.

Ninatambua kwamba ni wakati wangu wa kukua, kukubali nimefikisha umri wa kupokea urithi kutoka kwa Mungu wa mbinguni kupitia Yesu Kristo.

Bwana ninakushukuru kwamba uliniita kuwa mwanafunzi wako na kwa bidii nimejifundisha neno lako.

Bwana ninakushukuru kwamba umeniita kuwa mhuduma wako na ninatafuta kukutumikia kwa njia zote.

Sasa ninajua ni wakati wangu wa kufanyika Mwana. Ninakuomba neema yako ya kuelewa; ninaomba ufunuo kuelewa; ninaomba upako wako kubadilishwa.

Bwana nataka kufanyika mwana wako. Ninataka kupokea ujasili ndani ya moyo wangu ili kwa ujasili nisimame mbele yako. Ninatamani kuwa na usalama kikamilifu kama mtoto wako na sasa, kama mwana wako; nisijisikie hisia za kung'ang'ana ama kujitambulisha; nipate usalama ndani yako na katika mwili wako.

Nimejinyenyekesha kwa 'kurudiwa na Bwana' kama mwana, nikijua kwamba kama Baba yangu utanileta katika ukamilifu kupitia urudi wako wa kiungu Bwana, dhihirisha kitabulisho changu kwangu nitembeapo katika uwana, nikipokea urithi wangu na kutimiza wito wa Mungu ambao uko katika maisha yangu.

Bwana naomba baraka zako katika maisha yangu kuniwezesha kufaulu katika maisha yangu.

Baba, 'nipe ambacho umeniwekea', kabla ya kuwekwa kwa nyakati.

AMINA